# Nipashe

Alhamisi Desemba 5, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580093

www.ippmedia.com

The Guardian digital   nipasheTZ   nipasheTZ   nipasheTZ   0745 700710



Piga simu bure

Kujifunza kuhusu Ualbino, kutoa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino

0800 75 00 50

Albinism Hotline




## Wazazi wadaiwa kuwakingia kifua watuhumiwa wa ubakaji

UKURASA 3

# Chungu, tamu za Sumaye Chadema

**AFUNGUKA** kuwa hakuna demokrasia ya kweli, aeleza alivyopoteza mali kisa kuwa upinzani, Prof. Safari abwaga manyanga ...

*Endelea ukurasa wa 2*



Waziri Mkuu mstaafu Frederick Sumaye, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, alipotangaza kujivua uanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA). **PICHA: MIRAJI MSALA**

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**MATIKO AKIRI KUMILIKI SILAHA**

SHAHIDI wa tano wa utetezi, Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko (Chadema) anayekabiliwa na kesi ya uchochezi na wenzake wanane, amekiri...

UKURASA WA 5

**HATIMA YA KABENDERA KWA DPP**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam imeuagiza upande wa utetezi katika kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili ...

UKURASA WA 7

**MAMA YAKE BILIONEA MSUYA AKUBALI KUONDOA KESI KORTINI**

MAMA wa marehemu Bilionea Erasto Msuya, Ndishu Msuya, amesema yuko tayari kuondoa kwa muda shauri...

## MIAKA 30 JELA KWA KUBAKA KIKONGWE

UKURASA 3

# Serikali yatangaza msimamo uzimaji wa laini zisizosajiliwa

UKURASA 2




Scan Hapa



**MICHEZO** AUSSEMS ASHUKIA 'VIHIYO' WA SIMBA UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Chungu, tamu za Sumaye Chadema

**Mary Geofrey na Maulid Mmbaga**

WAZIRI Mkuu mstaafu wa Awamu ya Tatu, Frederick Sumaye, ameelezea machungu na matamu aliyoyaonja katika siku 1,436 akiwa ndani ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema).

Sumaye ambaye alijiunga na Chadema Desemba 12, 2015 na kukabidhiwa kadi na Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe, jana alitangaza kukihama chama hicho kikuu cha upinzani kwa madai ya kukosekana kwa demokrasi.

Alitangaza msimamo wake huo rasmi jana jijini Dar es Salaam mbele ya waandishi wa habari, bila kuweka wazi atajiunga na chama gani cha siasa nchini.

Mwanasiasa huyo, Agosti 22, 2015, Sumaye alitangaza kujiondoa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa madai kuwa anaunga mkono mageuzi yanayofanywa na vyama vya upinzani vinavyounda Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa).

**CHUNGU CHADEMA**

Zikiwa zimebaki siku saba kabla ya kutimiza rasmi miaka minne tangu alipojiunga na Chadema, alijitokeza hadharani na kuelezea mazuri na magumu aliyopitia ndani ya chama hicho.

Alisema haikuwa rahisi kujiunga upinzani bali ilihitaji moyo kwa sababu aliwahi kuwa na nafasi kubwa nchini na muda mfupi baada ya uamuzi huo, alianza kupata matatizo kutoka serikalini.

"Mashamba yangu yalichukuliwa na hata baadhi ya huduma zangu zilianza kuwa tofauti na wastaafu wenzangu. Familia yangu ilianza kuona mateso ya mimi kuwa upinzani na walinilaumu na kusononeka sana.

"Pamoja na hali hii ya mateso, nilikaza shingo kwa vile niliamini kuwa kinachopiganiwa na wapinzani kama kitafanikiwa ni kikubwa kuliko hiki cha familia yangu," alisema Sumaye huku akiongoze kuwa aliamini hatua aliyochukua ingejenga demokrasia ya kweli ambayo itadumisha maendeleo na haki kwa wote.

"Kwa kweli familia yangu ilishaanza kuzoea hali hiyo na hatukuwa tunagombana tena kuhusu mimi kuwa upinzani," alisema Sumaye.

Sumaye alisema jambo lingine lililomuumiza ni nongwa aliyodai kufanyiwa baada ya kuamua kuchukua fomu ya kuwania nafasi ya mwenyekiti wa taifa wa Chadema.

"Pamoja na kuwa ni haki yangu kwa mujibu wa katiba ya chama chetu, pia nilikuwa na lengo la kwanza la kuondoa

INAENDELEA UK. 8



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, George Simbachawene, akizungumza na Mkuu wa Shirika la Chakula Duniani (WFP) na Kaimu Mkurugenzi Mkazi wa Umoja wa Mataifa (UN) Tanzania, Michael Dunford, alipomtembelea ofisini kwake, jijini Dar es Salaam jana, ambapo walijadiliana ushirikiano katika programu za mazingira hususan mabadiliko ya tabianchi ambayo huathiri usalama wa chakula. **PICHA: OMR**

# Serikali yatangaza msimamo uzimaji wa laini zisizosajiliwa

**Na Waandishi Wetu**

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Mhandisi Isack Kamwele, ametegua kitendawili cha kuzimwa simu ambazo laini zake hazijasajiliwa kwa vidole ifikapo Desemba 31, mwaka huu, kwa kusisitiza kuwa nia ya serikali iko pale pale.

Kamwele amesisitiza msimamo huo zikiwa zimebaki siku 27 kufika siku ya mwisho ya matumizi ya laini ambazo hazijasajiliwa kwa vidole kwa kutumia vitambulisho vya taifa.

Kabla ya waziri huyo hajaweka msisitizo wa uamuzi huo jana, kumekuwapo na kauli za kukinzana baina ya viongozi wa serikali na taasisi zinazosimamia mawasiliano nchini.

Akiwa bungeni mjini Dodoma katika mkutano uliopita wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, alieleza kuwa hakuna laini ya simu ya mtu itakayofungwa kwa kukosa kitambulisho cha Taifa.

Lugola alitoa kauli hiyo wakati akijibu mwongozo wa Mbunge wa Kavuu (CCM), Dk. Pudensiana Kikwembe, ambaye alitaka kupata majibu ya serikali kuhusu wananchi ambao bado hawajapata vitambulisho vya Taifa pamoja na kusajili laini za simu.

Lugola alisema lengo la usajili na utambuzi ilikuwa ni kuwafikia watu milioni 23.3, lakini hadi sasa Watanzania milioni 20.5 wameshasajiliwa, zimezalishwa namba za vitambulisho kwa Watanzania milioni 15.5.

"Naomba niwatoe hofu Watanzania kwamba hakuna mtu yeyote ambaye laini yake ya simu itafungwa kisa hajasajili kwa sababu hana kitambulisho cha Taifa," alisema Lugola.

Pia Lugola alisema kazi ya utambuzi, usajili na utoaji wa vitambulisho kwa wananchi ambao wana sifa za kupata vitambulisho ni endelevu na halina mwisho.

**ALICHOKISEMA KAMWELE**

Jana Nipashe ilimtafuta Waziri Kamwelwe kwa ajili ya kupata ukweli wa suala hilo na kuwaondolea hofu Watanzania wengi.

Kamwelwe alisema: "Kazi yangu ni kusajili laini za simu, lengo kuu likiwa ni kupunguza utapeli kwa njia ya mtandao, kuna watu wana laini 20 na ndiyo maana tumetoa muda wa kusajili."

"Desemba 31 tutazima laini ambazo hazijasajiliwa, na ninayezima ni mimi, Waziri wa Mambo ya Ndani kazi yake ni kutoa vitambulisho vya Nida na kama alivyosema zoezi ni endelevu," alisema Kamwelwe.

**KAULI YA TCRA**

Kwa upande wake, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imesema yeyote ambaye hatasajili laini ya simu kwa alama za vidole kwa mujibu wa kisheria, itafungiwa.

Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa Kanda ya Kaskazini TCRA, Mhandisi Emelda Salum, wakati wa kampeni ya 'Mnada kwa Mnada' ikiwa Wilaya ya Babati mkoani Manyara.

Alisema siku zilizobaki hadi sasa ni 27 ambazo zilitolewa kwa ajili ya usajili wa laini za simu kwa alama za vidole na kuwataka wale ambao

INAENDELEA UK. 8

# Profesa Safari abwaga manyanga

**Mwandishi Wetu na Juster Prudence**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chadema Tanzania Bara, Prof. Abdallah Safari, ameeleza sababu za kutogombea nafasi hiyo kuwa ni kutofurahishwa na matokeo ya Bunge la Afrika Mashariki na nia ya dhati ya upinzani kupigania Tume Huru ya Uchaguzi.

Aidha, amesema ataendelea kuwa mwanachama wa kawaida na hana mpango wa kukiacha chama hicho kwa kuwa muda wake mwingi wa maisha ameutumia kwenye upinzani.

Akihojiwa na mtandao mmoja, alisema baada ya matokeo hayo alimuita Mwenyekiti wa Chadema Taifa, Freeman Mbowe na Makamu Mwenyekiti wa Zanzibar, Issa Mohamed, na kuwaeleza kuwa amechoka na umri wa miaka 68 ni mkubwa.

"Nimekuwa kwenye upinzani kwa miaka 20, nilikuwa Mkurugenzi wa Masomo na Mipango wa Chuo cha Diplomasia na niliachishwa kazi kwa sababu ya kumtetea Prof. Ibrahim Lipumba. Nimeumizwa sana na masuala ya upinzani," alisema na kuongeza:

"Nilitegemea wapinzani wenzangu watakuwa na nguvu sana ya kutaka kupambana na CCM na agenda yangu kubwa ilikuwa Tume Huru ya Uchaguzi."

"Nilimwambia Prof. Lipumba baada ya uchaguzi wa mwaka 1995 na yaliyotokea na Tume ya Jaji Nyalali kuwa uchaguzi wa vyama vya upinzani lazima utanguliwe na Tume Huru ya Uchaguzi, tutafute nafasi tugombee, lakini aliniambia tusimwachie nguruwe shamba la mihogo.

"Hiki kitu kimekuwa kikinikatisha tamaa sana. Nimekuja Chadema sikuona kama kuna msukumo wa kutaka kupata Tume Huru ya Uchaguzi. Tunataka kwenda Ikulu bila kuwa na njia ya kwenda Ikulu, hatuwezi kwenda Ikulu, nawaambia kila siku, Prof. Lipumba alisema tusimwachie nguruwe shamba la mihogo, nguruwe amekula mpaka mihogo yenyewe," alisema.

Prof. Safari alisema aliandika kitabu mwaka 2009 kueleza haja ya kuwa na Tume Huru ya Uchaguzi na kueleza kwa kifupi kuwa bila hicho kitu hakuna uwezekano wa kwenda Ikulu.

"Huku pia wenzangu sijaona nia ya dhati ya kutafuta Tume Huru ya Uchaguzi, nimekatishwa tamaa sana. Kimsingi nataka nipumzike kabisa. CCM hawanipendi kabisa na wala msifikirie nitakwenda CCM, hiyo haiwezi kutokea," alisema.

Kiongozi huyo alisema anajua CCM hawampendi kabisa kwa kuwa walimwondoa kazini akiwa na miaka 49 wakati anafanya mipango ya kwenda Makahama ya Kimataifa, The Hague, Uholanzi

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KITAIFA

# Miaka 30 jela kwa kubaka kikongwe

**Na Juster Prudence**

MKAZI wa Kijiji cha Nange mkoani Mwanza, Shabo Marando (47), amehukumiwa kutumikia kifungo cha miaka 30 jela kwa kosa la kumbaka bibi wa miaka 60.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Misungwi mkoani Mwanza, Esther Malick, baada ya kupitia ushahidi wa upande wa mashtaka uliokuwa na mashahidi wanne.

Ilidaiwa na shahidi wa tatu, Dk. Judith Kiwango wa hospitali ya wilaya hiyo, aliyemfanyia uchunguzi bibi huyo kwamba, alikutwa na michubuko sehemu za siri.

Shahidi wa pili, Sama Luheka alidai alisikia kelele kichakani aliposogea alimkuta mtuhumiwa akimbaka bibi huyo.

Bibi huyo alidai mahakamani kuwa siku ya tukio, mtuhumiwa alimkuta shambani akikusanya kuni, akamkamata kwa nguvu na kumvutia kichakani kisha kumbaka.

Kwa mujibu wa taarifa ya uhalifu wa kibinadamu iliyotolewa na Jeshi la Polisi, kwa mwaka 2018, kati ya matukio 11,759, ya ubakaji yalikuwa 7,617, sawa na asilimia 64.7.



Ofisa Mkuu wa Uendeshaji na Utawala wa Makambi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Idara ya Huduma kwa Wakimbizi, Stephen Msangi, akifafanua jambo kabla ya kuanza uhuishaji takwimu za wakimbizi waishio Dar es Salaam, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: WMNN**

# Wazazi wadaiwa kukingia kifua watuhumiwa ubakaji

**Na Romana Mallya**

WAKATI vitendo vya ubakaji na ulawiti vikiongezeka mkoani wa Dar es Salaam kwa kipindi cha miezi 10 ndani ya miaka miwili, wadau akiwamo Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Sarah Msafiri, wameeleza tatizo la wazazi kuwakingia kifua watuhumiwa.

Takwimu zinaonyesha katika kipindi cha miezi 10, mwaka jana (2018) matukio ya ubakaji yaliyoripotiwa polisi jijini Dar es Salaam ni 608 na mwaka huu (2019) yameongezeka na kufikia 719 huku vitendo vya ulawiti vikiongezeka kutoka 259 mwaka jana na kufikia 319, mwaka huu.

Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Sarah Msafiri akizungumza katika Kampeni ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, alisema ma ipo kesi moja ilitokea Feri, Kigamboni, jijini Dar es Salaam, mlinzi wa maduka maeneo hayo aliwalawiti watoto wa kiume.

Alisema polisi iliweka mtego uliowezesha kukamatwa kwa mlinzi huyo.

Hatua ya awali iliyochukuliwa ni kwa watoto hao kupelekwa hospitali kupimwa na ilibainika kuwa walikuwa wamefanyiwa kitendo hicho.

"Baada ya wiki mbili wale watoto walikuja ofisini na wazazi wao, mzazi ananyanyuka anatetea mtoto wake hajalawitiwa, wakati ripoti ya daktari inaonyesha amelawitiwa, tukiwa na jamii ya aina hii hatuwezi kufikia malengo," alisema na kuongeza:

"Tutakuwa tunalilaumu Jeshi la Polisi na kuwaharibu watoto wetu kwa kutengeneza jamii ambayo siyo nzuri kwa sababu ya kutotoa ushirikiano matukio yanapotokea na kupoteza ushahidi wake," alisema.

Alisema ili kesi ziende, na haki itendeke lazima hatua za uchunguzi zikamilike kwa kila mtu kutoa ushirikiano.

"Matukio ya watoto kulawitiwa yanaendelea kuongezeka, baba acha kumlinda mke wako, mwanamke akirudi saa 12 umeshajua, mtoto akirudi saa nne usiku au hajarudi hujali, mna kazi ya kulindana wazee, wazazi mbadilike muwalinde watoto wenu," alisema.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni, alisema Mkoa wa Mjini Magharibi visiwani Zanzibar, jumla ya kesi 280 zinazohusiana na matendo ya udhalilishaji, ubakaji na ulawiti yameripotiwa.

"Tatizo hili linaendelea kukua kwa kasi na inasikitisha sana, jambo hili linachafua heshima ya nchi yetu, serikali tumeamua kuja na mkakati maalumu wa kupambana na changamoto ya udhalilishaji, ubakaji na ulawiti na tunaomba mamlaka nyingine zitunge mkono," alisema.

Naye, Mwenyekiti wa Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (Tamwa), Joyce Shebe, akitoa maoni kuhusu kuongezeka kwa ubakaji na ulawiti, alisema lazima serikali irudi kuzungumza na wadau ili kukomboa kizazi kijacho.

"Hali hii ikiendelea hivi ilivyo kuna uwezekano mkubwa ndoa za jinsia moja huko mbeleni kuongezeka, hatua nyingine za kuchukuliwa ni upande wa ustawi wa jamii wasaidie kutengeneza mambo ya msingi ili kulinda na kutoa elimu zaidi," alisema.

Pia aliomba vyombo vya sheria vitoe ushirikiano mtuhumiwa anapokamatwa vihakikishe hukumu inatolewa.

INAENDELEA UK. 8


## HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

## TANGAZO LA UUZAJI WA VIWANJA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma anawatangazia Wananchi wote kuwa zoezi la upimaji wa viwanja limekamilika na kuanzia **TAREHE 3/12/2019** viwanja vitaanza kuuzwa kila siku za Jumatatu hadi Ijumaa katika eneo la wazi la Manispaa ya zamani (karibu na Sabasaba) kuanzia saa 2 Asubuhi hadi saa 9.30 Alasiri.

**Viwanja vinavyouzwa ni katika maeneo ya:**

| ENEO | MATUMIZI NA BEI TSHS KWA (SQM1) |
|---|---|
| NALA (Karibu na Chuo cha IFM na Kituo cha kupaki Malori) | • Makazi 4,000/=<br>• Makazi na Biashara 5,000/= |
| CHAHWA (Karibu na Ikulu) | • Makazi 3,000/=<br>• Makazi na Biashara 5,000/= |
| Mahoma Makulu (Nyuma ya Mji wa Serikali) | • Makazi 3,000/=<br>• Makazi na Biashara 5,000/= |
| KIKOMBO (Karibu na Bandari kavu na Makao Makuu ya Ulinzi ya Taifa) | • Makazi 2,000/=<br>• Makazi na Biashara 3,500/= |
| MTUMBA (Karibu na Mji wa Serikali na Ikulu) | • ZONE I Makazi 8,000/= Makazi na Biashara 8,500/=<br>• ZONE II Makazi 6,000/= Makazi na Biashara 7,500/=<br>• ZONE III Makazi 3,000/= Makazi na Biashara 5,500/= |

**NB: Malipo yote yafanyike ndani ya Siku 90 baada ya kupata hati ya madai.**

***Kwa mawasiliano zaidi piga simu namba 0714 785513.***

**Tangazo hili limetolewa na:**
**Mkurugenzi wa Jiji,**
**DODOMA**

215542002

# Matiko akiri kumiliki silaha

**Na Hellen Mwangwo**

SHAHIDI wa tano wa utetezi, Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko (Chadema) anayekabiliwa na kesi ya uchochezi na wenzake wanane, amekiri mahakamani kuwa anamiliki silaha aina ya revolver, lakini hajawahi kuitumia. Alidai mahakamani wakati akitoa ushahidi wake mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, baada ya kuhojiwa na Jamhuri dhidi ya utetezi wake. Shahidi huyo aliongozwa na Wakili wa utetezi, Peter Kibatala.

Akihojiwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, mshtakiwa huyo alidai kuwa ingawa anamiliki silaha hiyo hajawahi kuitumia wala hakumbuki kama iliwahi hata kufyatuka mahali popote.

Alidai wakati akiongozwa na Wakili wa utetezi, Kibatala kuwa katika kampeni za uchaguzi mdogo wa ubunge Jimbo la Kinondoni, alipewa jukumu la kufuatilia nakala za viapo na barua za utambulisho wa mawakala.

Alidai kuwa yeye ni mkazi wa Tarime Mjini, Februari 15, 2018 alipofika Dar es Salaam, aliwasiliana na mmoja wa viongozi wa kamati ndogo ya uchaguzi, Benson Kigaila kwa simu kumfahamisha kuwa amefika.

"Aliniteua mimi na Mbunge wa Viti Maalum, Susan Lyimo, kufuatilia barua za utambulisho pamoja na hati za viapo vya mawakala," alidai Matiko.

Akifafanua zaidi alidai kuwa walianza kufuatilia barua hizo Februari 16, 2018, saa nne asubuhi walikwenda kumuona Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni ambaye ndiye alikuwa msimamizi wa uchaguzi huo ili awasaidie kupata barua hizo. Alidai kuwa walifika ofisini kwa Mkurugenzi na kuambiwa wasubiri mpaka walipoonana naye saa saba mchana, lakini aliwaambia anashughulikia jambo hilo hivyo wasubiri mpaka saa 12 jioni.

"Tulisubiri mpaka saa 12, lakini hatukufanikiwa kupata barua hizo na mkurugenzi aliwahakikishia watapata mpaka kufikia saa moja usiku wa siku hiyo," alidai na kuongeza:

"Tulipewa namba za simu za msimamizi wa uchaguzi na msaidizi wake na kuendelea kuwasiliana na msimamizi msaidizi wa uchaguzi aliyemtaja kwa jina la Victoria Charles, mpaka saa tano usiku na kwamba alionekana kutingwa na kazi ya kusambaza vifaa vya uchaguzi hivyo akashindwa kumpatia barua hizo na kumwahidi kuwa atawasiliana naye saa 11 alfajiri ya Februari 17, 2018 ambayo ndiyo ilikua siku ya uchaguzi," alidai Matiko.

Alidai kuwa mpaka kufikia saa 11 alfajiri barua na nakala za viapo hivyo zilikuwa hazijapatikana, alitoa taarifa kwa msimamizi wa uchaguzi na baadaye kwa viongozi wa kamati ndogo ya uchaguzi na jukumu lake likaishia hapo.

Mbali na Matiko, washtakiwa wengine ni Mwanyekiti wa Chadema Freeman Mbowe, Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Salum Mwalimu, Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche, Mbunge wa Kawe, Halima Mdee, Mbunge wa Kibamba John Mnyika na Mbunge wa Bunda, Esther Bulaya.

Pia wamo Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa na Katibu Mkuu wa chama hicho, Dk. Vincent Mashinji.

# Mikoa vinara ukatili yaanikwa

**Na Waandishi Wetu,**
MWANZA

UKATILI wa kijinsia umeendelea kuwa tatizo nchini huku mikoa ya Tabora, Kagera, Geita, Simiyu na Kigoma ikitajwa kuongoza kwa kuwa na kiwango kikubwa cha matukio hayo.

Hayo yalibainishwa jana wakati wa mkutano wa wazee wa mila kutoka mikoa tisa nchini uliofanyika jijini Mwanza kwa lengo la kujadili mchango wao na namna wanavyoweza kuondoa matukio ya ukatili, ndoa na mimba za utotoni katika jamii.

Takwimu za mwaka 2015/2016 zilizotolewa na Tanzania Demographic and Health Survey (TDHS), mikoa ya Mara na Shinyanga inaongoza orodha ya mikoa 11 vinara kwa matukio mengi ya ukatili wa kijinsia ikiwa na asilimia 78. Mikoa mingine ni Tabora asilimia 71, Kagera (67), Geita (63), Simiyu (62), Kigoma (61), Mwanza (60), Njombe (53), Dodoma na Katavi (50).

Takwimu hizo pia zinabainisha kuwa, mikoa tisa inayoongoza kwa ndoa za utotoni ni Shinyanga yenye (59), Tabora (58), Mara (54), Dodoma (51), Lindi (48), Mbeya (45), Singida (42), Morogoro (42) na Rukwa (40). Lucy Tesha, mwakilishi wa Shirika la UN Women, alisema lengo la kuwakutanisha wazee hao 225 ni kuunga mkono mpango kazi wa serikali wa kutokomeza ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto.

"Nia hasa ni wao kukaa pamoja ili wafanye tafakari, waweke mikakati ya pamoja jinsi ya kusimamia mila zile nzuri ziendelezwe na zile potofu ambazo tumeona sasa hivi ni tatizo kwa maendeleo yetu, hasa ukiangalia kuwa nchi yetu inaelekea kwenye uchumi wa viwanda, ziachwe," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Kivulini, Yassin Ally, aliwaomba wazee hao kuwa na umoja na kusimama hadharani kukemea vitendo hivyo na kuwasihi wanajamii kuenzi mila nzuri zenye kuleta maadili na malezi ili kujenga msingi wa maendeleo na uchumi wa taifa.

Ally alisema katika Mkoa wa Shinyanga, kati ya kaya 10, nane zina ukatili wa kijinsia na kwa Mwanza, kati ya kati 10, sita zina ukatili wa kijinsia.

Alisema kwa mujibu wa takwimu za TDHs, Mkoa wa Katavi unaongoza orodha ya mikoa 12 vinara kwa mimba za utotoni, ukiwa na asilimia 45.

Mikoa mingine ni Tabora asilimia 43, Dodoma (39), Morogoro (39), Mara (37), Shinyanga (34), Mbeya (33), Kigoma (32), Ruvuma (32) na Geita, Simiyu na Singida (yote asilimia 30).

Mshiriki wa mkutano huo, Thobista Ibrahim kutoka Geita, alidai wanaume ndiyo wanachangia kwa kiwango kikubwa ndoa za utotoni na kutelekeza familia kunakosababisha kuwapo kwa idadi kubwa ya watoto wa mitaani.



Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, wakichagua mananasi katika Soko la Buguruni, jijini humo, jana. Kutokana na tunda hilo, kuwa katika msimu wake, bei ya nanasi moja imeshuka na kuuzwa kwa 500/- hadi 1,500/- kulingana na ukubwa wake. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Sekou Toure yalalamikia mzigo wanaoghushi rufani

**Na Anthony Gervas,**
MWANZA

HOSPITALI ya Rufani Sekou Toure jijini Mwanza imelalamika kuelemewa na wimbi la wagonjwa wanaoghushi umri wa msamaha, miaka 60 na rufani kutoka hospitali za ngazi ya chini kuhalalisha matibabu yao hospitalini hapo.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa hospitali hiyo, Leah Linti, aliambia Nipashe juzi kuwa katika kundi la wazee hao walionaswa katika njama za kughushi msamaha, wamo watendaji wastaafu wa taasisi za umma ambao hawajafikia umri husika, baadhi wakidanganya wana uwezo duni kiuchumi. Alilitaja kundi lingine la wap

otoshaji hao ni vijana wenye umri kati ya miaka 38 na 40, wanaoshiriki katika njama za kughushi barua zinazodaiwa kutoka serikali za mitaa, wakidai nao ni wazee.

Pia alilalamika kuwapo kundi la wahitaji wa matibabu, wajawazito na watoto wengi waliojenga mazoea kama ya wazee, kufika Sekou Toure moja kwa moja bila kupitia ngazi zingine, ambayo ni kinyume cha utaratibu unaowataka kupitia ngazi za mwanzo.

"Tumekuwa na wimbi kubwa la wagonjwa hao, lakini itafika mahali tutashindwa kumudu kutoa huduma zao kama wataendelea kutofuata taratibu. Limekuwa ni tatizo na mzigo mkubwa, nawaomba wafuate taratibu zinazotakiwa," alilalamika.

Alibainisha kuwa kwa siku hospitali hiyo imekuwa inapokea wagonjwa zaidi ya 100 wasiojiweza, wakiwamo wazee wenye umri wa kuanzia miaka 60 kutoka katika maeneo mbalimbali ya Mwanza, kundi ambalo kisera linapaswa kupata huduma za matibabu bila malipo.

Kwa mujibu wa Leah, mizigo hiyo ya ziada isiyo ya lazima katika hospitali hiyo, imechangia kupunguza kiwango cha ubora wa huduma za hospitali hiyo ambayo wahitaji wake pia wanajumuisha mikoa ya jirani ya Kanda ya Ziwa.

Alisema Sekou Toure kwa sasa upatikanaji wa dawa muhimu kwa wagonjwa ni wa asilimia 96.

HABARI KITAIFA

# Jengo jipya JKCI kuongeza wagonjwa

**Na Maulid Mmbaga,** DSJ

TAASISI ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), imeongeza vifaa na kukamilisha ukarabati wa jengo la kutoa huduma ya matibabu ya moyo kwa watoto.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Profesa Mohammed Janabi, alisema jengo hilo ni utekelezaji wa ahadi ya Rais John Magufuli na kwamba kabla ya watoto walitumia jengo moja na watu wazima.

Akielezea hali halisi kabla ya kuwa na jengo jipya, alisema watu wazima na watoto walilazwa kwenye chumba kimoja, kliniki na ICU huku wodi ya kulaza wagonjwa ilikuwa na vitanda 11.

Pia alisema kutokana na eneo dogo la kutolea huduma za kliniki, wagonjwa waliopata huduma kwa siku walikuwa 25 hadi 30, huku uwezo wa kupokea wagonjwa wengi ukiwa mkubwa.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, Rais aliwapatia sehemu ya jengo la Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kwa ajili ya watoto na iliwachukua miezi tisa kilikarabati na kubadilisha miundombinu kukidhi mahitaji halisi ya watoto.

"Nina furaha kubwa kuona jengo letu limekamilika na lina vitanda 40, kwa ajili ya watoto na vingine vinane kwa ajili ya wagonjwa walio katika uangalizi maalumu (ICU). Hivi karibuni litafunguliwa kwa sasa tuko katika hatua za mwisho," alibainisha Prof. Janabi.

Mkurugenzi huyo alisema uwapo wa jengo hilo utawezesha madaktari kutoa huduma kikamilifu tofauti na kipindi cha nyuma walivyokuwa wanachanganywa watoto na watu wazima katika wodi moja.

"Katika kliniki tumepata vyumba bora vinne na hii itatuongezea idadi ya kutoa huduma kutoka watoto 30 hadi 60 kwa siku kwa sababu eneo limekuwa kubwa na mitambo inayotumika kuwahudumia watoto karibu yote imeshanunuliwa," alibainisha.

Mmoja wa madaktari bingwa wa magonjwa ya moyo, Dk. Naiz Majani, alisema tatizo la ugonjwa wa moyo kwa watoto nchini ni kubwa na kwamba mwaka 2018 walizaliwa watoto 10,000 katika Hospitali ya Taifa Muhimbili kati yake 100 walikutwa na ugonjwa huo.



Dereva wa bajaji, akipakia mzigo wa abiria wake juu ya chombo hicho, katika Barabara ya Morogoro, eneo la Manzese, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni ukiukwaji wa sheria za usalama barabarani. **PICHA: JOHN BADI**

# Hatima ya Kabendera kwa DPP

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam imeuagiza upande wa utetezi katika kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili mwandishi wa habari za uchunguzi, Erick Kabendera, kufuatilia majibu ya barua kwa Mkurugenzi wa Mashtàka (DPP) ili kujua hatima yake.

Kabendera aliandika barua kwa DPP ya kufanya makubaliano na kuomba msamaha na kukiri tuhuma zinazomkabili.

Jana kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Janeth Mtega.

Wakili wa Serikali, Esther Martin, alidai kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa, na kuwa upepelezi haujakamilika.

Hata hivyo, wakili wa utetezi, Jebra Kambole, alidai kuwa Oktoba 11, mwaka huu waliitaarifu mahakama kuhusu mshtakiwa kuandika barua ya kuomba msamaha na kukiri kosa kwenda kwa DPP, lakini hadi jana, ikiwa ni miezi miwili hawajapata mrejesho wowote kutoka kwa DPP.

"Bado tunasubiri kukamilisha mchakato wa majadiliano ya barua tuliyomwandikia DPP kwa kuwa mpaka sasa hakuna chochote ambacho kimefanyika, na mtuhumiwa bado yupo mahabusu na ni mgonjwa," alidai Kambole.

Wakili Martin alikiri maombi hayo yapo kwa DPP tangu Oktoba 11, hadi jana, lakini alidai suala la makubaliano si maamuzi yanayoweza kutolewa mara moja, na kwamba itapendeza kama watakwenda kwa mkurugenzi huyo.

Hakimu Mtega alisema upande wa utetezi waende wenyewe kufuatilia jalada la kesi kwa DPP ili wajue kinachoendelea.

Alisema kesi hiyo itatajwa tena Desemba 18, mwaka huu na mshtakiwa ataendelea kukaa mahabusu.

Katika kesi ya msingi, Kabendera anakabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi yenye mashtaka matatu, likiwamo la utakatishaji wa Sh. milioni 173.

Katika shtaka la kwanza ilidaiwa Kabendera alijihusisha na mtandao wa kihalifu kwa kutoa msaada kwa genge la uhalifu kwa nia ya kujipatia faida.

Inadaiwa kuwa bila ya sababu, alikwepa kodi ya Sh. 173,247,047.02 ambayo ilitakiwa ilipwe Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Pia, inadaiwa Kabendera alitakatisha Sh. 173,247047.02, huku akijua fedha hizo ni mazalia ya kosa la kujihusisha na genge la uhalifu na ukwepaji kodi.

CAPITAL RADIO

POPOTE ULIPO SIKILIZA CAPITAL RADIO KATIKA MASAFA YAFUATAYO




www.capitalradioco.tz @capitalradiotanzania @CapitalRadiotz capitalradiotz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tunahitaji kuanza kampeni ya maadili

**TUNAPOADHIMISHA** Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, kampeni ya kimataifa kuhamasisha jamii kuacha unyanyasaji wanawake na watoto, tuna mengi yakujikosoa. Ni kwa sababu wakati huo ndipo tunaposikia kuwa ukatili unaongezeka nchini.

Kampeni hiyo inayoanza Novemba 25 hadi Desemba 10, inakutana na taarifa kuwa taifa linakabiliwa na changamoto kubwa ya unyanyasaji. Taarifa ya Polisi jijini Dar es Salaam inasema ubakaji na ulawiti umeongezeka na kwamba kila siku watu wawili hubakwa. Polisi Kanda Maalumu inasema mwaka huu matukio ya ubakaji yaliyoripotiwa yamefikia 719 ikilinganishwa na 608 ya mwaka jana. Inasema ulawiti umeongezeka kutoka visa 259 mwaka jana hadi kufikia 319 mwaka huu, hizi si taarifa njema ni kama vile kusema unyanyasaji unatishia hatima ya Watanzania.

Ukatili huu ni kero kila upande, inaonyesha jinsi ambavyo tunakuwa taifa la watu wasio na maadili.

Watoto wanalawitiwa na kubakwa na jamaa wa karibu, wakiwamo baba walezi au wa 'kambo' ndugu wa kiume ambao pia ni wa 'kambo' wanadhulumiwa kingono na hata wazazi wao, licha ya walimu shuleni nao kufanya hivyo.

Kwenye vyuo wanafunzi wa kike wanalalamikia kuombwa rushwa ya ngono na wahadhiri, lakini pia kazini na popote wanawake wanapoomba huduma huishia kuombwa ngono.

Katika maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia,kama taifa inabidi tubadilike lazima kuwa na maadili.

Licha ya kufanya kampeni nyingi kwa miaka mingi inakuwaje rushwa ya ngono, unyanyasaji watoto, ulawiti na ukatili kuongozeka? Tunapaswa kufanya kazi zaidi. Ndiyo maana tunazipongeza na kuziunga mkono juhudi nyingi zinazofanywa na taasisi mbalimbali kutetea haki za watoto na wanawake na kupinga ukatili wa kijinsia.

Kwa mfano Chama cha Wanahabari Wanawake Tamwa, Shirika la ActionAid, TGNP Mtandao ni miongoni mwa wadau wakuu.

Tunazipongeza asasi hizi zimefanya mambo mengi kwa mfano ActionAid, imeanzisha masanduku ya maoni shuleni ili mabinti waeleze wanavyonyanyaswa kwenye jamii.

Aidha, wameunda mitandao ya kuwalinda mabinti inayohusisha madereva wa bodaboda ambao wanatuhumiwa kuwa wahusika wakuu kwenye kuwapa mabinti na wanafunzi mimba.

Madereva hawa sasa ni nguzo muhimu kulinda na kufuatilia watu wanaowanyanyasa wasichana. Yote hayo yakifanyika wilayani Mafia mkoani Pwani. Tamwa Zanzibar na Bara ni mfano wa kuigwa imekemea tabia ya kuficha siri za wadhalilishaji kwa kuhimiza jamii kutoa taarifa kwa wadau na walinzi wa watoto mitaani.


Aidha, mafunzo ya mara kwa mara na kutangaza kwenye vyombo vya habari taarifa za unyanyasaji, kumewezesha kuibua matukio ya ubakaji na wengi kufikishwa mahakamani. Yote haya yamefanikisha kuripoti na kufikishwa mahakamani wahusika.

Leo hii tunauona mkono wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), ikianza kujiingiza kupambana na rushwa na ngono na pia kuzishughulikia familia zinazoficha taarifa za watoto kunyanyaswa kingono kwa kisingizio kuwa wanayamaliza wenyewe nyumbani. Tunapongeza juhudi hizi ni njema ambazo sasa zitaamsha ari mpya ya kuripoti polisi, kwenye vyombo vingine vya dola na kuwezesha kunasa watuhumiwa kwa kuuogopa mkono wa Takukuru. Tunaona kuwa licha ya kujitahidi za kuwafikisha mahakamani watuhumiwa hao ni wakati taifa kuwa na mkakati wa kurejesha maadili kuanzia shuleni, kwenye ibada, sehemu za kazi, vyuoni na vyuo vikuu.

Ni vyema kufundisha heshima, maadili ulinzi wa watoto na pia kuhamasisha Watanzania wazee kwa vijana kubadilika na kuwa watu wenye maadili na kuheshimiana. Tunaona kuwa kampeni hii ni muhimu kwani unyanyasaji ni ukiukaji wa haki za binadamu, sheria na huzorotesha afya na maendeleo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Utozaji kodi uendane na elimu, uwajibikaji pamoja



Na Sabato Kasika

**KISIASA** na kiserikali ukitaka kujua moja ya ishara kuu za matendo ya Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Rais Dk. John Magufuli, ni kwamba ulipaji na ukusanyaji kodi ni muhimu na likichukua nafasi ya lazima kisheria.

Ni ajenda aliyoifanyia kazi kwa namna nyingi Rais Dk, Magufuli kufikia upeo wa mbali. Mwanzo wake ni katika hatua ya kampeni za uchaguzi. Alihimiza mno haja ya kukusanya kodi kwa manufaa ya taifa, sasa na baadaye.

Alitufunza namna kila mmoja wetu anakuwa muwajibikaji katika hilo. Dhana ya kudai risiti katika ununuzi ilikuwa sehemu ya mikakati. Kila muuzaji anaingia katika mfumo unaomuwajibisha kulipa kodi.

Matumizi ya mashine maalum za kutoza kodi na kutoa risiti zilisambaa kila mahali ambako kituo cha biashara kilikuwa na kiwango cha mauzo kinachotakiwa.

Ni hali ambayo wakati serikali katika upande mmoja wanaendeleza mikakati iliyoonyesha mafanikio, katika sura ya pili ni kwamba kuna wafanyabiashara wenye mashine za kukata kodi, lakini wazito wamakusudi kuzitumia

Wanachofanya ni kukata risiti za mauzo kwa kuvizia. Wanaokwepa sana kufanya mauzo yenye risiti kwa sababu itawaingiza katika mfumo wa kutozwa kodi kwa kila wanachokiuza.

Ndipo ninarudi katika kauli ambayo Rais Dk. Magufuli, daima hajaacha kuihimiza. Kuna wakwepaji kodi na wakati huohuo, wajibu wetu mkuu ni kuhakikisha hao wakwepa wanatimiza wajibu wao.

Nimesema hilo ni eneo moja tu, kwani kuna mustakabali wa michango ya kiserikali katika maeneo mengi ya kisheria, ikiwamo michango ya waajiri kuwasilishwa kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii.

> **Wale ambao ni watoaji wa sadaka hizo, mara nyingi wanakuwa zao la somo bora la imani waliopata kupitia hatu mbalimbali za kiimani katika maisha yao. Hiyo ni elimu ambayo katika hatua zao za maisha wanakutana na dhana ya utozaji ushuru au kodi.**

Kwa ujumla, kuna mengi yanayohitajika kwa wakati mmoja. Mgandamizo kwa kila anayetakiwa na anayepaswa kulipa kodi afanye hivyo, inayoendana na elimu husika.

Mabadiliko hayatokei ghafla hata mara moja, tena katika jambo la wajibu watu kufanya malipo hata kama ni ya kisheria ikianzia na mazingira ya imani.

Tujiulize, hata katika nyumba za ibada kuna wakati utoaji wa sadaka za hiari inakuwa mtihani.

Wale ambao ni watoaji wa sadaka hizo, mara nyingi wanakuwa zao la somo bora la imani waliopata kupitia hatu mbalimbali za kiimani katika maisha yao. Hiyo ni elimu ambayo katika hatua zao za maisha wanakutana na dhana ya utozaji ushuru au kodi.

Nini kifanyike? Kama unavyotumika katika bidii za uwakala wa vita vyakutafuta afya bora, usalama na hata uchumi, matumizi ya nguvu na hiari kuchukua nafasi kuanzia serikalini hadi mifumo binafsi, ndicho kinapaswa kuwapo katika kodi.

Kama nilivyosema awali, mengi yameanzishwa na kufanyika kiserikali, kuanzia awamu zilizopita hadi iliyopo. Tuendelee zaidi ya pale tulipofika.

Mwalimu Julius Nyerere katika zama zake alishatamka kwamba serikali yoyote haramu sifa yake halipi kodi, kwa maana inawakumbatia wakwepaji, huku mwenyewe katika msimamo wa serikali yake, hakuwea na masihara na wakwepa kodi.

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), hadi sasa inabeba wajibu mkubwa katika jukumu la kukusanya mapato ya serikali. Haishii katika mapato na ushuru pekee, bali inaenda mbali katika makusanyo ya tozo mbalimbali ya kiserikali, kama vile faini na ada za huduma nyingi.

HABARI KITAIFA

# Mama yake Bilionea Msuya akubali kuondoa kesi kortini

**Na Allan Isack, ARUSHA**

MAMA wa Marehemu Bilionea Erasto Msuya, Ndishu Msuya, amesema yuko tayari kuondoa kwa muda shauri la miradhi lililoko mahakamani dhidi yake na mke wa marehemu, Miriamu Mrita, ili kupisha mazungumzo nje ya mahakama.

Amesema endapo mazungumzo hayo yanayotarajiwa kuongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, hayatafanikiwa, atarejea mahakamani kuendelea na shauri hilo ili kupata haki ya msingi ya hatima ya mali za mwanawe.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Ndeshu alisema amefika mahakamani hapo kuiomba mahakama kuondoa kwa muda shauri hilo ili watafute mwafaka nje ya mahakama.

Kwa mujibu wa mama huyo, amefungua shauri hilo la mirathi kumpinga msimamizi wa mirathi, mke wa marehemu, kwa madai ya kushindwa kusimamia, kugawanya na kufunga mirathi kwa wanufaika kwa kipindi cha miaka saba kinyume cha sheria. "Tumekuja mahakamani kuiomba mahakama, kama itapendezwa, tuondoe shauri hili kwa muda na si kufuta kesi ili turejee kwenye mazungumzo nje ya mahakama na tukishindwa kuafikiana tutarudi tena mahakamani," alisema.

Bilionea Msuya aliuawa kwa kupigwa zaidi ya risasi 20 mwaka 2013 na kuacha mjane na watoto wanne pamoja na mali mbalimbali zikiwamo majumba, fedha, magari, mashamba na hoteli mali ambazo zinadaiwa kuwagombanisha wanandugu.

Ndeshu aliamua kukimbilia mahakamani kupinga msimamizi wa mirathi hiyo, akidai kwamba Miriam anashikiliwa gerezani kwa tuhuma za mauaji ya wifi yake, hivyo si mwaminifu na ameshindwa kugawanya mali za marehemu kwa wanufaika kwa muda wa miaka saba tangu kifo cha mumewe.

Alisema mali hizo zimekuwa zikiwanufaisha upande wa mke wa marehemu (wajomba) badala ya watoto wanne wa marehemu ambao kimsingi ndio wanaostahili kurithi mali hizo.

Awali, mtoto mkubwa wa marehemu, Kelvin, alimwomba bibi yake kuridhia kesi hiyo kuondolewa mahakamani na kukaa meza ya mazungumzo na upande wa wazazi wa baba yake.

Naye mjomba wa watoto wa marehemu, Mbazi Mrita, aliomba serikali kuingilia kati mgogoro huo kwa kuondoa kesi hiyo mahakamani kama walivyoshauriwa na Muro.

Kesi hiyo itasikilizwa na Jaji Johane Masara wa Mahakama Kuu na ilipelekwa mahakamani hapo Novemba 29, mwaka huu, lakini iliahirishwa na Msajili Msaidizi wa Mahakama hiyo, John Nkwabi, hadi Desemba 13, mwaka huu.



Mjumbe wa Bodi ya Wadhamini wa Chama cha Wananchi (CUF), Mussa Haji Kombo (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, akimlalamikia aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chama hicho, Maalim Seif Sharif Hamad (hayupo pichani), kwa kukihujumu chama hicho, katika maeneo ya Unguja na Pemba. Kulia ni Mwenyekiti wa Wazee CUF, Mohammed Chunga na Mkurugenzi wa Haki za Binadamu na Sheria, Harub Mohammed Shamis. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## UNHCR yahitaji bil. 290/- kuwahudumia wakimbizi

**Na Faustine Feliciane**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR), limesema linahitaji kiasi cha dola za marekani milioni 126 (zaidi ya Sh. bilioni 290) kwa ajili ya kuhudumia wakimbizi waliopo maeneo mbalimbali nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Kamishna Msaidizi wa Operesheni wa Shirika hilo, George Okoth-Obbo, alisema licha ya kuhitajika fedha hizo, kiasi walichonacho ni moja ya tatu tu ya fedha hizo, hivyo bado wanaziomba taasisi nyingine washirika kuendelea kuchangia. Aidha, alisema katika makubaliano ya pande tatu juu ya wakimbizi wa Burundi waliopo nchini kati ya Serikali ya Tanzania, Burundi na UNHCR, wamekubaliana kuwa wakimbizi walio tayari kwa hiari yao kuanza kurejea nchini kwao waende, lakini ambao bado hawapo tayari kurejea Burundi wataendelea kubaki Tanzania na kupata huduma zote kwa mujibu wa taratibu na sheria za kimataifa.

"Nitumie nafasi hii pia kuipongeza na kuishukuru sana Serikali ya Tanzania kwa kuendelea kuwasaidia wakimbizi wa Burundi, lakini pia kwa pamoja tumekubaliana na kutiliana saini mkataba wa kuwarudisha nyumbani wakimbizi walio tayari," alisema.

Alisema hadi sasa zaidi ya wakimbizi 79,000 wamesaidiwa kurejea Burundi katika kuanzia Mei 2015 mpaka sasa.

Kwa mujibu wa takwimu zilizopo, Tanzania imewapa hifadhi ya ukimbizi watu 278,275 ambapo kati yao wakimbizi 166,000 ni raia wa Burundi, ambao wengi wao walianza kuingia nchini tangu Aprili 2015.

Katika makumbaliano hayo ya pande tatu, wakimbizi walijioandikisha watasaidiwa kurejea kwao ambapo 2,000 watapokelewa Burundi katika makundi ya wakimbizi 1,000 kwa wiki.

# Malipo makandarasi yamshtua waziri

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ameagiza Katibu Mkuu wa Tamisemi na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijini (Tarura) kuwasiliana na Katibu Mkuu Hazina ili kubaini sababu za kuchelewesha malipo ya makandarasi.

Jafo alitoa agizo hilo jana wakati wa ziara ya kukagua ujenzi wa miradi ya maendeleo jijini Dodoma, ikiwamo ya barabara ya Swaswa kwa kiwango cha lami kilomita 1.8, eneo la kuegesha malori Nara na ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za sekondari Itega na Lukundo. Akiwa katika mradi wa eneo la kuegesha malori Nara, Jafo alielezwa na Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi, kuwa mradi huo umeshajengwa kwa zaidi ya asilimia 80, lakini malipo kwa mkandarasi bado yapo nyuma na wanahofu kuanza kutozwa riba.

"Mheshimiwa waziri, kama unavyoona hapa kazi kwa kiasi kikubwa imefanyika, lakini bado lipo tatizo la kuchelewa kwa malipo kwa makandarasi, kama tutaendelea hivi, hofu yangu ni kulipishwa riba na mkandarasi kwa kuchelewesha malipo yake kwani kazi kubwa amefanya kwa fedha zake mwenyewe," alitahadharisha.

Kutokana na hali hiyo, Jafo aliimwagiza Katibu Mkuu Tamisemi, Joseph Nyamuhanga, na Mtendaji Mkuu wa Tarura, Victor Seif, kuhakikisha wanafuatilia kwa Katibu Mkuu Hazina sababu za kuchelewa kwa malipo hayo ili kupata suluhu ya suala hilo.

"Kazi hii nimeona kwa macho yangu, ni kazi nzuri sana na hii 'packing' (maegesho) ya malori ni kubwa kuliko ile tuliyoijenga kule Makambako, hivyo nawaagiza Katibu Mkuu Tamisemi pamoja na Mtendaji Mkuu Tarura kufuatilia Hazina kuona nini kinakwamisha ili kupata fedha za hawa makandarasi na miradi hii sasa ikamilike kwa wakati," aliagiza.

Akiwa katika mradi wa ujenzi wa barabara ya Swaswa, Jafo alimpa siku 26 mkandarasi wa mradi huo ambaye ni Kampuni ya SKOL, kuukamilisha vinginevyo asipewe tena kazi nchini.

Jafo alisema mkandarasi huyo ameonyesha kushindwa kufanya kazi na kukamilisha kwa wakati kwa kuwa alitakiwa kumaliza kazi Agosti mwaka huu, akaongezwa hadi Oktoba mwaka huu, lakini hadi sasa hajamaliza.

"Mkandarasi huyu nikija hiyo Desemba 30, mwaka huu, baada ya hizo siku 26, kama atakuwa hajakamilisha mradi huu, asipewe tena mradi mwingine na nimefurahi kuwa mmeanza kumkata fedha kwa kuchelewesha mradi," alisema.

Meneja wa Tarura Dodoma, Geofrey Mkinga, alisema tayari wameshamkata mkandarasi huyo Sh. milioni 82 kutokana na kuchelewa kukabidhi mradi huo.

"Tumemlipa mpaka hivi sasa Sh. milioni 759 na kazi aliyoifanya mpaka sasa ni asilimia 83, bado asilimia 17 na gharama ya mradi mzima ni Sh. bilioni 1.375," alibainisha.

# Chungu, tamu za Sumaye Chadema

INATOKA UK. 2

hisia iliyojengeka katika jamii kuwa ndani ya Chadema hakuna demokrasia ya kweli," alisema Sumaye.

Aliendelea kueleza kuwa aliamua kuwania nafasi hiyo kuondoa dhana kuwa Chadema inamilikiwa na Mbowe peke yake na haipaswi kusogelewa na mwanachama yeyote.

"Mimi binafsi sikuamini kuwa hisia hizi ni za kweli ndiyo maana haya yasipofutika yatatuchafulia jina la chama chetu. Kumbe mimi ndiyo nilikuwa nimekosea kufikiri hivyo. Matokeo yake badala ya busara kutumika hata kama tungetaka kumlinda Mbowe wetu, zilizotumika njia za ovyo," alisema Sumaye.

Alisema kilichotokea ni baadhi ya wajumbe wa kamati kuu ambao ndio waliofanya mpango wa kupelekewa fomu za kuwania nafasi ya Mwenyekiti wa Kanda ya Pwani, walimgeuka na kuhakikisha hashindi nafasi hiyo.

Katika uchaguzi huo, uliofanyika Alhamisi iliyopita, Sumaye alimwagwa kwa kupigiwa kura za hapana 48 dhidi ya ndiyo 28 na moja iliharibika.

"Baadhi ya wajumbe wa kamati kuu ambao ndio walifanya mpango wa mimi kuletewa fomu ya kuwania kanda hiyo, wakageuka kuhakikisha mimi ambaye nilikuwa mgombea pekee wa nafasi hiyo nanyimwa kura na za hapana zilishinda," alisema Sumaye.

Sumaye alidai wajumbe walipiga kura wakawekwa hotelini, wakalipwa fedha kwa kazi hiyo na sababu kubwa ni kwa nini alichukua nafasi ya kuwania kiti cha mwenyekiti wa taifa.

"Basi wangenitahadharisha kuwa katika chama chetu nafasi hiyo ina utaratibu wa tofauti nje ya katiba, ningeelewa na labda ningetii na kama nisingetii basi wangenisubiri kwenye vikao vinavyohusu nafasi hiyo," alisema Sumaye na kusisitiza kuwa chama hicho hakina demokrasia ya kweli na kwamba nafasi aliyoishikilia Mbowe haiguswi.

"Kwa bahati mbaya sana ndivyo ilivyotokea na waliojaribu kuwania nafasi hiyo katika siku za nyuma yaliwakuta kama haya na labda mengine mabaya zaidi," alisema.

Sumaye alitangaza kutowania tena nafasi ya mwenyekiti taifa wa Chadema licha ya kuchukua fomu, kuilipia Sh. milioni moja, kuijaza na kuirudisha kwa wakati baada ya kufanya uchunguzi na kujiridhisha kuwa si busara kuendelea na safari hiyo.

"Inabidi leo (jana), nitangaze kuwa hiyo safari ya kugombea uenyekiti ngazi ya taifa naisitisha rasmi kwa usalama wangu, usalama wa wanachama na chama chenyewe. Kwa bahati nzuri tulipokuwa kwenye mkutano wa kanda, Mbowe alitutahadharisha kuwa sumu haionjwi kwa ulimi na mimi sitaki kuionja," alisema Sumaye.

Alisema uchaguzi wa mwaka huu ndani ya chama, umeacha majeraha ambayo si ya kushindwa kwenye uchaguzi bali mgawanyiko ndani ya chama kwa sababu watu walikuwa wanachaguana kwa kutegemea kundi la nani.

"Kwa wale waliokuwa wanaitwa timu Mbowe, kulikuwa na nguvu kubwa kutoka nje ya kanda zilizotumika na watu ambao si timu Mbowe waliumizwa sana," alisema Sumaye.

**MATAMU YA CHADEMA**

Sumaye alisema muda baada ya kujiunga Chadema, alipokewa vizuri na kufanya kazi kwa kushirikiana.

Alisema baada ya muda Mbowe alimteua kuingia katika kamati kuu ya chama hicho nje ya miezi sita baadaye baadhi ya viongozi na wanachama wa Chadema wa kanda ya Pwani, walimwomba awanie nafasi ya mwenyekiti wa kanda hiyo.

Nafasi hiyo, alisema alichaguliwa na kuwa mwenyekiti hadi juzi walipofanya uchaguzi na kushindwa licha ya kutokuwa na mpinzani.

Alisema licha ya kujiondoa katika chama hicho, yuko tayari kutoa ushirikiano kama atahitajika kwa ajili ya kuwashauri juu ya yale yote yaliyotokea.

"Mwisho kabisa nataka niwaambie ndugu zangu wa Chadema mimi bado nawapenda sana na nina imani na hiki chama katika safari yetu ndefu ya kuleta mabadiliko chanya katika ujenzi wa demokrasia yetu," alisema Sumaye.

Alisema hata kama hayupo ndani ya chama hicho lakini ataendelea na kazi na kujenga demokrasia.

Naye aliyekuwa Katibu wa Kanda ya Pwani Chadema, Casmir Mabina, alitangaza kujivua nafasi hiyo kwa madai ya 'figisu' zilizotokea kwenye uchaguzi wa kanda hiyo.

Alisema tayari jana alikabidhi barua yake katika ofisi za makao makuu ya Chadema na atabaki kuwa mwanachama mwadilifu kupitia tawi lake.

# Wazazi wadaiwa kukingia kifua watuhumiwa ubakaji

INATOKA UK. 3

Hata hivyo, alisema kuongezeka kwa vitendo hivyo kunachangiwa na mambo ya usasa ya mitandao ya kijamii na baadhi kujifunza na kutaka nguvu ielekezwe kwa kutoa elimu zaidi.

Juzi, Kamanda wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, alitaja takwimu za ubakaji na ulawiti na kueleza kuwa katika kipindi cha Januari hadi Oktoba, mwaka jana, matukio ya ubakaji yalikuwa 608 na kufikia 719 mwaka huu.

"Ulawiti umeongeza kutoka 259 mwaka jana na kufikia 319 mwaka huu, matukio ya wizi wa watoto yamepungua kutoka 12 hadi matukio saba," alisema.

Kamanda Mambosasa alisema matukio ya utupaji wa watoto nayo yamepungua kutoka 17 mwaka jana na kufikia 15, mwaka huu.

"Kesi 218 zimepelekwa mahakamani, za kubaka zikishinda kesi 27, kulawiti zilizoshinda 99, kutupa watoto kesi ni mbili," alisema.

Alisema kesi za ubakaji 19 zilishindwa kutokana na ushahidi hafifu, ulawiti 12 na za utupaji watoto ni mbili.

Kamanda Mambosasa alisema kwa mwaka huu jumla ya watuhumiwa 298 walikamatwa kwa makosa ya kubaka, 133 kulawiti, kutupa watoto matukio manne na wizi wa watoto tukio moja.

# Serikali yatangaza msimamo uzimaji wa laini

INATOKA UK. 2

hawajafanya hivyo wajitokeze.

"TCRA ipo katika kampeni ya Mnada kwa Mnada ya uhamasishaji wa usajili wa laini za simu kwa alama za vidole ambaye hatatimiza matakwa ya kisheria ya kusajili laini ya simu kwa alama za vidole laini hiyo itafungwa," alisema Salum.

Kampeni hiyo inashirikisha kampuni ya simu, Jeshi la Polisi kitengo cha uhalifu mitandaoni, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Idara ya Uhamiaji kwa ajili ya utoaji wa huduma za usajili wa laini za simu kwa kutumia vitambulisho vya kitaifa na kuhakikiwa na kampuni za simu kuweka alama za vidole kwa laini za simu.

Mhandisi Emelda alisema ni fursa kwa wananchi wa Babati na maeneo mbalimbali waliofika katika viwanja vya stendi ya zamani ya Magugu kupata namba ya kitambulisho cha Taifa na kusajili laini zao.

Alisema kampeni hiyo ilianzishwa ili kutoa fursa ya wananchi kuhudumiwa kwa pamoja na kuwataka wajitokeze kwenye maduka ya kampuni za simu kusajili laini zao kabla ya Desemba 31.

Ofisa Mawasiliano Mwandamizi wa TCRA, Mabel Masasi, alisema wananchi wameitikia wito kwa kujitokeza kuangalia namba ya vitambulisho kwa ajili ya kusajili laini zao.

**Imeandaliwa na Romana Mallya na Gwamaka Alipipi**



Mkuu wa Kitengo cha Wafanyabiashara wa Kati na Wadogo wa Benki ya NBC, Evance Luhimbo, akizungumza na wafanyabiashara wadogo na wa kati wa maeneo ya Kariakoo, katika semina ya siku moja iliyoandaliwa na benki hiyo, yenye lengo la kuwawezesha kimafunzo ambayo yatasaidia ukuaji wa biashara za wateja wake wa Jiji la Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Profesa Safari abwaga manyanga

INATOKA UK. 2

akawe Jaji, jambo lililosababisha baba yake kupata mshituko na kufariki dunia baada ya kuona mwanawe kapoteza kazi.

"Sifikirii sasa hivi kutoka Chadema, Nitabaki Chadema lakini sitajihusisha na siasa," alisema.

Aidha, alisema iko haja ya kuboresha demokrasia ili kuwa na uhalali wa kuisema CCM kuwa wanapokea demokrasia, huku akitolea mfano wa Sumaye na Cecil Mwambe alivyotaka kugombea nafasi ya mwenyekiti na yaliyowakuta.

**UCHAGUZI BAWACHA**

Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kimetangaza majina ya wagombea waliorejesha fomu kugombea nafasi ya Makamu Mwenyekiti na Baraza la Wanawake wa Chadema (Bawacha).

Uchukuaji fomu ulianza Novemba, mwaka huu na wagombea 171 walichukua, kujaza na kurudisha kugombea uteuzi wa wagombea wa nafasi 109 za uongozi ngazi ya taifa unaotarajia kufanyika Desemba 18, mwaka huu.

Wanaogombea nafasi ya Makamu Mwenyekiti Zanzibar ni Hawa Mwaifunga, Aisha Yusuph, Mary Nyagabona na Marceline Stanslaus wakati wanaogombea nafasi ya Makamu Mwenyekiti Bara ni Maryam Salum, Sharifa Suleiman na Zeudi Abdulahi.

Baraza la Wazee ndani ya chama hicho nalo limetangaza majina ya waliorudisha fomu kwa ajili ya uchaguzi wa wazee wa baraza utakaofanyika Desemba 9, mwaka huu.

Wagombea waliotajwa na Baraza la Wazee ni pamoja na Hashim Juma Issa na Hugho Kimaryo wakigombea nafasi ya Mwenyekiti Taifa, Idrisa Mkila na Mwanamrisho Abama.

Nafasi ya Mwenyekiti ni Suzana Lymo nafasi ya Makamu Mwenyekiti Bara, Andrew Kimbombo na Helen Kayanza nafasi ya Naibu Katibu Bara pamoja na Erasto Gwota akigombea nafasi ya mweka hazina.

# Ripoti ya WB yabainisha ongezeko masikini nchini

**Na Gwamaka Alipipi**

LICHA ya Tanzania kuendelea kufanya vizuri katika kuendeleza sekta ya kilimo, idadi ya watu masikini nayo imeendelea kuongezeka kutoka milioni 12.3 mwaka 2012 hadi milioni14 mwaka jana.

Hayo yalibainishwa katika ripoti ya 13 iliyotolewa na Benki ya Dunia (WB), inayohusu hali ya uchumi wa Tanzania, maendeleo katika sekta ya kilimo.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo iliyosomwa jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mkazi wa WB Tanzania, Bella Bird, Tanzania inaendelea kuimarisha hali ya maisha ya wananchi wake, lakini mwaka 2012 idadi ya watu masikini imeendelea kuongezeka.

"Kwa mujibu wa takwimu za makazi kwa sasa, umasikini kwa wakazi wa Tanzania bara umepungua kutoka asilimia 28.2 kwa mwaka 2012 hadi asilimia 26.4 mwaka 2018," alisema Bird na kuongeza:

"Katika kipindi hicho, ongezeko la watu limekuwa likiongezeka zaidi na kuwa kubwa kuliko kupungua kwa umasikini, kwa mwaka 2018 idadi ya Watanzania milioni 14 walikuwa wanaishi kwenye umasikini, ikilinganishwa na idadi ya watu milioni 12.3 kwa mwaka 2012 waliokuwa masikini, na watu milioni 13.2 mwaka 2007 waliokuwa masikini."

Ripoti hiyo ilieleza kuwa kilimo cha kati kwa mashamba kuanzia hekta tano hadi 20 kimeongezeka kutoka asilimia 23 kwa mwaka 2008 hadi asilimia 35 kwa mwaka 2014.

Pia ilieleza kuwa sekta ya kilimo Tanzania imeendelea kubadilika, na kwamba uzalishaji umeongezeka, masoko yameongezeka, pamoja na ongezeko la uzalishaji wa mtu nao umeongezeka.

Ripoti hiyo pia imeeleza kuwa wakulima wa kati wameongezeka nchini na wamekuwa na ushirikiano na wakulima wadogo.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya uzinduzi wa ripoti hiyo, Mchumi Mwandamizi kutoka WB, Emma Isinika Modamba, alisema ripoti hiyo imetoa mapendekezo matatu ambayo serikali ya Tanzania inapaswa kuyatekeleza ili kuboresha zaidi sekya ya kilimo.

Alisema pendekezo la kwanza ni kuhakikisha mazingira ya kufanya biashara yanaongezeka, pili fedha zaidi zielekezwe katika sekta ya kilimo kwa wakulima kupewa pembejeo bora pamoja na kuboreshewa masoko.

Alisema pendekezo lingine ni kuboreshwa kwa matumizi ya maji na ardhi, kwa sababu asilimia 60 ya ardhi Tanzania imeharibika kutokana na matumizi ya muda mrefu.

# Sababu wilaya kusitisha kilimo cha pamba

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

WAKULIMA wilayani Sikonge, mkoani Tabora ambao wanataka kulima zao la pamba, wametakiwa kuwa wavumilivu hadi hapo utafiti utakapokamika ili Serikali ijiridhishe kama tishio la mdudu aina ya funza mwekundu halipo katika maeneo jirani yaliyopigwa marufuku kulima zao hilo.

Ushauri huo ulitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, wakati wa kikao robo ya kwanza cha baraza la madiwani.

Alisema kwamba Wizara iliweka karantini kwa wilaya zinazopakana na mikoa ya Rukwa na Mbeya kutolima pamba kutokana na kuwapo funza wekundu wanaoshambulia zao hilo.

Mkuu wa Mkoa alisema hawezi kuruhusu watu walime hadi hapo wataalamu wa Wizara waje wajiridhishe na watoe tamko kuhusiana kutokuwepo kwa tishio la mdudu huyo.

Mkuu wa Mkoa aliwataka Madiwani wasiende kuwahamasisha wananchi kulima zao la pamba kabla hawajapata msimamo wa Serikali ili wasijekupata hasara.

Mwanri alisema kitendo cha kuruhusu kulimwa kwa zao hilo kabla ya matokeo ya wataalamu hayajatoka kunaweza kusababisha hasara kubwa katika maeneo ya ndani na nje ya Mkoa wa Tabora ambapo funza huyo mwekundu anaweza kusabambaa hata katika maeneo ambayo alikuwa hayupo.

Awali Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge, Peter Nzalalila, aliishauri Serikali iwaruhusu walime pamba kama zao mbadala ya tumbaku ambayo inapigwa vita kimataifa.

Aliomba Serikali iwaruhusu kulima pamba kwa kuwa maeneo ya jirani zao ambayo yalikuwa yamepigwa marufuku wameanza kulima na wana vyama vya Msingi vya zao hilo.

Nzalalila alisema wakazi wengi wamehamasika kulima pamba wanachosubiri kibali ili waweze kushiriki kilimo hicho kwa ajili ya kuondokana na umaskini.

Katika hatua nyingine madiwani na viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge wametakiwa kutumia mvua zinazoendelea kunyesha kuwahimiza wananchi kujielekeza katika kulima kwa kuzingatia kanuni za kilimo bora.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuzalisha chakula na mazao ya biashara ya kutosha ambayo yatawasaidia kujiongezea kipato na kuboresha maisha yao.

Aliongeza kuwa kwa kutambua umuhimu wa kipindi hiki ndio maana amesimamisha kwa muda likizo za Maofisa Ugani na Kilimo ili waweze kutoa ushauri utakaomsaidia mkulima kulima kisasa.



Mwendesha guta akiwa amesheheni mzigo wa madumu matupu ya plastiki, katika Barabara ya Morogoro, eneo la Jangwani, jijini Dar es Salaam jana, kitendo kinachomfanya ashindwe kuona magari yanayokuja nyuma jambo ambalo ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: JOHN BADI**

# Agizo Baraza NGO kukutana

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya uratibu wa mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini, imeliagiza Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kukutana ili kuhakikisha wanatatua changamoto za uendeshaji wa Baraza hilo kikamilifu na kutoa taarifa kwa Bodi ndani ya siku 14.

Taarifa hiyo itaeleza jinsi walivyoshughulikia changamoto hizo ikiwamo kuwasilisha taarifa ya utekelezaji ya Baraza hilo.

Agizo hilo lilitolewa jijini Dar es Salaam na Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Dk. Richard Faustine Sambaiga, wakati akizungumza na wajumbe wa Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika kikao kilicholenga kutoa maelekezo mahsusi kwa Baraza ili kukitaka chombo hicho kuzingatia matakwa ya kisheria katika uendeshaji wake.

Dk. Sambaiga aliliagiza Baraza hilo kufanya mapitio ya Kanuni ya Sheria ya marekebisho Na. 11/2005 na Sheria ya marekebisho Na.3/201 ili kukidhi mapendekezo ya mapitio ya kanuni hizo na kuwasilisha kwenye Bodi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ndani ya siku 30 ili kuondoa mkwamo wa kiutendaji wa majukumu ya Baraza la NGOs nchini.

Pia Dk. Sambaiga aliliagiza Baraza hilo kujielekeza kwenye matakwa ya muda wa kisheria wa kuwa kiongozi wa Baraza hilo ambao ni miaka mitatu toka kuteuliwa kwa Baraza mwaka 2016, na hivyo kuelekeza kuanza kwa mchakato wa uchaguzi wa Baraza jipya ndani ya siku 30.

"Nalielekeza Baraza kupitia upya uwakilishi wa wajumbe wa Mikoa na makundi maalum hasa ikizingatiwa ipo mikoa mipya na makundi ambayo hayana wawakilishi kwani kumekuwa na changamoto kubwa ya uwakilishi wa wajumbe kutoka mikoani," alisema.

Aidha, Dk. Sambaiga amewataka Viongozi wa Baraza la Taifa kuzingatia uwasilishaji wa taarifa yake ya utekelezaji wa kazi zake kwa Bodi ili kutosababisha Bodi kushindwa kutekeleza majukumu yake ya kisheria kama yalivyoainishwa kwenye kifungu 7(1) (j) cha Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali kinachoitaka Bodi kupokea kujadili na kupitisha taarifa za Baraza hilo.

Dk. Sambaiga alilitaka Baraza kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ikiwamo kutetea maslahi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kuwa jukwaa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kuhakikisha wanakuwa mwavuli wa hayo katika masuala yote yanayohusu uratibu na kutandaa kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

"Nawasihi viongozi wa Baraza Kutunga na kusimamia utekelezaji wa Kanuni za Maadili kwa lengo la kuwezesha Mashirika Yasiyo ya kiserikali kujiongoza kwa kufuata misingi ya kimaadili yenye uwazi na uwajibikaji."

# Mwenyekiti halmashauri kortini tuhuma rushwa

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Mkuranga mkoani Pwani, imemfikisha mahakamani Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga, Juma Abeid, akituhumiwa kujihusisha na vitendo vya kuomba na kupokea rushwa kiasi cha Sh. 220,000.

Akisoma mashtaka hayo, Mwendesha Mashtaka wa Takukuru wilayani humo, Euphrazia Kakiko, mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Mkuranga, Veronica Mawole, alidai kuwa mtuhumiwa huyo alitenda makosa hayo kwa nyakati tofauti kati ya Januari Mosi na Julai 22, mwaka huu.

Alidai kuwa mshtakiwa huyo aliomba kiasi hicho cha fedha kutoka kwa mlalamikaji, Bashiri Chande, ili amsaidie kufanikisha uhamisho wa mke wake ambaye ni mwalimu anayefanyakazi Wilaya ya Babati mkoani Manyara kwenda Mkuranga.

Alidai kuwa baada ya hatua hiyo mtuhumiwa alipokea kiasi hicho cha Sh. 220,000 kupitia kwenye simu yake ya mkononi, hivyo mlalamikaji alipeleka taarifa Takukuru na taratibu za hatua mbalimbali zikafanyika.

Hata hivyo, mshtakiwa hakutakiwa kujibu lolote kwa kuwa hakimu aliyekuwapo siku hiyo hakuwa na mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.Ilielezwa kuwa upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika.

Mtuhumiwa huyo yuko nje kwa dhamana, baada ya kutimiza masharti ya dhamana yaliyomtaka kuwa na wadhamini wawili kila mmoja akisaini bondi ya Sh. milioni moja.



Mwananchi akipita kwenye daraja jipya la Mto Mara, lililopo mpakani mwa wilaya za Serengeti na Tarime mkoani Mara juzi, ambalo limekamilika ujenzi wake, hatua ambayo imesaidia kuwaondolea madereva usumbufu kusubiri kupishana kwenye daraja la zamani ambalo lilikuwa ni dogo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# TMDA yatoa vibali 26,478 kimtandao

**Na Devota Mwachang'a**

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), imetoa vibali 26,478 katika mwaka 2018/19 sawa na ongezeko la asilimia 203 ukilinganisha na 13,018 mwaka 2015/16 kwa njia ya mfumo wa kieletroniki wa utoaji wa vibali.

Mfumo huo unamwezesha mteja kutuma maombi, kufanya malipo popote alipo kisha kupata kibali ndani ya saa 24.

Katika taarifa ya kiutendaji ya mamlaka hiyo iliyotolewa na kusainiwa na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Adam Fimbo, amesema wameongeza udhibiti wa uingizaji na usafirishaji wa bidhaa ndani na nje ya nchi kupitia mfumo wa kieletroniki wa utoaji vibali.

Fimbo alisema utoaji huduma za vibali kwa wateja umerahisishwa kwa kiasi kikubwa kupitia mfumo wa IMIS ambao umetumika kuweka taarifa na takwimu za TMDA zikiwamo za bidhaa, majengo yaliyosajiliwa na za wateja, na kuwa wanaweza kuleta maombi yao kwa mtandao bila kufika ofisi za TMDA.

"Kwa lengo la kutekeleza agizo la Rais John Magufuli, la Mei, 2017 linalolenga kuharakisha utoaji wa mizigo bandarini, Mamlaka imeweka wakaguzi wake ambao hufanya kazi saa 24 kwa siku zote za juma, na kufanikiwa kufikia na kuvuka malengo iliyojiwekea katika udhibiti wa ubora, usalama na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi ili kulinda afya ya jamii," alilezea Fimbo.

Aidha, alisema: "Kwa miaka minne ndani ya uongozi wa Rais Magufuli tumefanikiwa kutekeleza mpango wa ufuatiliaji wa ubora wa bidhaa katika soko, sampuli 1,136 za dawa za binadamu zilifuatiliwa na kuchunguzwa katika kipindi hiki ambapo asilimia 96 ziliendelea kukidhi vigezo vya ubora.

Kwa mujibu wa fimbo, TMDA imeanzisha mfumo wa kielektroniki wa ufuatiliaji utoaji wa taarifa za madhara yatokanayo na matumizi ya dawa na vifaa tiba kwa kutumia simu za mkononi au kompyuta na njia ya kutuma ujumbe wa simu.

Ameeleza kuwa Mamlaka imefanikisha uchunguzi katika mwaka 2017/18, jumla ya tani 140,705.25 za bidhaa dawa, na vifaa tiba zisizofaa kwa matumizi ya binadamu zenye thamani ya takribani Sh. 22,394,078,744 ziliteketezwa ikilinganishwa na tani 664.68 zilizoteketezwa mwaka 2018/19.

Pia amesema TMDA imeimarisha shughuli za maabara kwa kuongeza vifaa vya uchunguzi pamoja na ufungaji wa maabara ndogo 25 zinazohamishika katika vituo vya forodha kwaajili ya uchunguzi wa awali wa bidhaa. Matokeo ya uchunguzi wa sampuli yanaonesha kuwa bidhaa zilizochunguzwa zimekidhi viwango vya ubora na usalama kwa wastani wa asilimia 90.

Fimbo amesema kwa tathmini iliyofanywa usajili wa bidhaa za dawa, vifaa tiba na vitendanishi umeendelea kuimarika ambapo idadi ya bidhaa zilizosajiliwa imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka, katika kipindi cha miaka 2015/16 hadi 2018/19, jumla ya bidhaa 20,247 zimesajiliwa. Hii imetokana na kuongezeka kwa uelewa wa matakwa ya sheria miongoni mwa wafanyabiashara na kukua kwa biashara.

Fimbo alisema mamlaka imesimamia vyanzo vya makusanyo kwa ajili ya udhibiti ambapo bajeti imeongezeka kutoka Sh. bilioni 34.64 mwaka 2015/16 hadi Sh. bilioni 53.31 mwaka 2018/19 sawa na asilimia 53.8. Hii imewezesha utoaji huduma kwa ufanisi na kutoa gawio kwa Serikali kila mwaka hadi kufikia takribani Sh. bilioni 29.

## Ushahidi kichocheo cha mimba shuleni

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

TATIZO la mimba kwa wanafunzi mkoani Shinyanga limetajwa kuendelea kushika kasi, kutokana na kesi nyingi kushindwa kufikia hukumu, na watuhumiwa kufungwa jela kutokana na kesi hizo kukosa ushahidi.

Imeelezwa kuwa jamii inahusika kutokana na kufanya malidhiano kimya kimya na kuacha kuhudhuria mahakamani.

Hayo yalibainishwa na ofisa ustawi wa jamii Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Elizabeth Mweyo, wakati akiwasilisha taarifa ya mpango mkakati wa Serikali kitaifa wa kupunguza ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto (MTAKUWWA), kwenye kikao cha kujadili kutokomeza ukatili huo kilichoandaliwa na Shirika la Kivulini.

Alisema wanafunzi wa kike kwenye halmashauri hiyo wameendelea kukatishwa masomo yao kwa kupewa ujauzito, kutokana na watuhumiwa kuchochukuliwa hatua kali za kisheria ikiwamo kufungwa jela, na kusababisha jambo hilo kuzoeleka na wanaume kuendelea kuwatia mimba wakitambua hawatafungwa.

"Taarifa ya robo ya mwaka ya halmashauri ya wilaya ya Shinyanga kuanzia Julai hadi Septemba 2019, wanafunzi 18 wameshapewa ujauzito na kukatishwa masomo yao, 14 kutoka shule za sekondari, wanne za msingi," alisema Mweyo.

"Kesi hizi tunapokuwa tukizishughulikia na kuzifikisha mahakamani, nyingi zimekuwa zikiishia njiani kutokana na ushahidi kukosekana, ambapo wahusika wapande zote mbili wamekuwa wakifanya maliziano na kuacha kuhudhuria mahakamani au mhanga kumkana mtuhumiwa na hatimaye kesi kufutwa," aliongeza.

Naye mratibu wa MTAKUWWA, Mkoa wa Shinyanga, Tedson Ngwale, alisema kutokana na kuwapo kwa changamoto hiyo ya ushahidi, wanaandaa mkakati wa kuwabana wazazi, ambao wamekuwa na tabia ya kumaliza kesi kimya kimya, pamoja na kujenga nyumba salama za kuhifadhi waathirika ili wasirubuniwe kukana watuhumiwa.

Mzee wa kimila, Kapaya Sosoma mkazi wa Halmshauri ya Wilaya ya Shinyanga, alisema utamaduni wa kabila la Wasukuma huwa hawapendi kesi, na ndiyo maana wanamaliza kesi kimya kimya, pamoja na kuwaambia watuhumiwa wakimbie ili kesi ifutwa mahakamani.

Kwa upande wake Ofisa Tathmini na ufuatiliaji kutoka Shirika la Kivulini, Godfley Paschal, wanaotetea haki wa wanawake na watoto, alisema wameendesha kikao hicho ili kujadili changamoto za matukio ya ukatili wa kijinsia pamoja na kuzitafutia ufumbuzi likiwamo suala la mimba za wanafunzi.

# Dereva teksi auawa, afungwa mikono

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MWILI wa dereva wa teksi Lembris Mollel (23) mkazi wa Tengeru, wilayani Arumeru, umekutwa ndani ya gari baada ya kuuawa huku mikono yake ikiwa imefungwa na nyaya.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha Koka Moita, dereva huyo, alikutwa ameuawa ndani ya gari aina ya Toyota Corolla namba T183 BAZ.

Moita alisema tukio hilo, lilitokea mtaa wa Elikiroa Kata ya Lemara jijini hapa, baada ya mwili wake kukutwa ndani ya gari hilo.

Alisema mwili wa dereva huyo, ulikuwa nyuma ya viti vya gari hilo, ukiwa na majeraha kadhaa na mikono yake ikiwa imefungwa kwa nyuma na waya na gari hilo likiwa limetumbukizwa mtoni.

Aidha, alisema Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi wa kuwatafuta wahusika wa tukio hilo.

Mwili wa marehemu umehifadhiwa katika Hospitali ya Mkoa wa Arusha Mount Meru.

Halikadhalika, katika tukio jingine mtoto mdogo wa miaka mitatu Gift Michael, aliyekuwa akiishi katika Kijiji cha Ilkuishini Wilaya ya Arumeru amefariki dunia, baada ya kutumbukia kwenye shimo la kuhifadhia maji ya ujenzi.

Chanzo cha tukio hilo kilielezwa na Kaimu Kamanda kuwa ni mtoto kucheza karibu na shimo hilo, ambalo lilikuwa wazi na lilikuwa limejaa maji ya mvua.

Kaimu Kamanda alisema mwili huo, haukuonekana kwa haraka kutokana na maji yaliyokuwa shimoni kuwa na takataka nyingi hivyo yalimfunika marehemu. Mwili wa Gift umehifadhiwa katika Hospitali ya Selian kwa ajili ya uchunguzi zaidi.



Kiongozi wa Dawati la Kunusuru Kaya Maskini (TASAF), kutoka Benki ya Dunia, Michelle Zini (katikati), akimshukuru Mkuu wa Wilaya ya Karatu, Theresia Mahongo (kulia), kwa niaba ya wananchi wa kijiji cha Laja, wilayani humo, Mkoa wa Arusha jana, baada ya kukabidhiwa zawadi ya mbuzi, kama ishara ya kushukuru kwa kutolewa katika umaskini na mpango huo. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# Wabobezi wamtibu aliyeugua miaka 15

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

TIMU ya madaktari wabobezi wa macho kutoka chama cha Lions Club Arusha imemfanyia upasuaji wa jicho mgonjwa aliyeteseka na maradhi hayo kwa miaka 15.

Mgonjwa huyo Rashid Mkulenya (20), mkazi wa Kijiji cha Mdori mkoani Manyara, aliteseka na ugonjwa huo wa macho kwa zaidi ya miaka 15, bila kupata masaada wa matibabu ya upasuaji wa macho.

Hata hivyo, wataalamu hao hawakueleza maradhi yaliyokuwa yanamsumbua na kumsababishia upofu.

Akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki, Mkulenya, alisema tatizo la macho alikuwa nalo tangu akiwa mtoto na kuwashukuru madaktari hao kwa matibabu waliyompatia.

Alisema baada ya kufanyiwa upasuaji ameanza kuona na kwamba akilinganisha na mwanzo kabla ya kupewa huduma hiyo, alikuwa anakata tamaa.

Alisema pamoja na kumkwamisha kimaisha kwa kiasi kikubwa ugonjwa huo umemdumza na watu wakimwangalia wanaweza kumkadiria kuwa na umri wa miaka pengine 14 wakati ameshatimiza miaka 20 sasa.

Alisema baada ya kupata matibabu hayo, matarajio yake ni kuiona nuru aliyeikosa kwa kipindi cha miaka 15 tangu alipokuwa mdogo.

Fatma Samson dada wa Rashid Mkulenya, alisema alianza kuishi na mdogo wake baada ya wazazi wao kufariki wakati huo akiwa na umri wa miaka mitano.

Fatma alisema alipata tatizo hilo akiwa na miaka mitano, lakini hakutaja alikuwa na shida gani.

"Mdogo wangu hajawahi kusoma shule yoyote kutokana na kuwa mgonjwa wa macho. Leo tunamshukru Mungu madaktari hawa walioshirikiana na mbunge wa Babati wamemtibu na sasa ameanza kuona," alisema Fatma.

Mbunge wa Babati Vijijini, aliyeshughulikia tiba hiyo, Vrajil Jituson, alimtaka dada wa mgonjwa kumwangalia kwa umakini.

Alishauri mgonjwa kutokuangalia runinga kwa muda wa mwezi mzima kutokana na uwezekano wa mionzi yake kuumiza macho yake.

Hata hivyo, alisema wakati akisubiri kutengemaa kwa afya yake, alimshauri kutafuta vitabu vya kusoma, pia alimwahidi kumpeleka katika vituo vya mabingwa wa

## Wataka waziri kuingilia kati ili wapate umeme

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAKAZI takribani 40 wa Kata ya Terat katika Halmashauri ya Jiji la Arusha, wameiomba serikali kuingilia kati na kutatua kikwazo kinachowakwamisha kupata umeme.

Aidha, wamemwomba Waziri wa Nishati Dk. Merdadi Kalemani, kuingilia kati ili kutatua tatizo la umeme walioomba tangu Januari mwaka huu, lakini Tanesco mkoani Arusha, haijawapatia huduma hiyo.

Wananchi wa eneo hilo, waliandamana hadi kwenye Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Mkoa wa Arusha, wakiilalamikia Tanesco kuwa tangu mwezi Januari, haiwaunganishii umeme kwa madai ya kukosekana nguzo za umeme.

Wakizungumza na waandishi wa habari kwa niaba ya wananchi wengine, Ally Hamis, James Baraka na Felician Matthew walisema suala la kuunganishiwa umeme limechukua muda mrefu bila ya kupewa ufumbuzi na maelezo ya kutosheleza hivyo wanamwomba waziri kuingilia kati ili wapate kupata haki yao.

Walisema jambo hilo limekuwa kikwazo cha maendeleo na kwamba kila walipofanya jitihada za kupata msaada ofisi hizo za Tanesco zimekuwa zikitoa ahadi zisizotekelezwa.

Walisema wakati wa ziara yake mkoani hapa, Mei mwaka huu, Waziri Kalemani aliagiza Tanesco kufikisha huduma hiyo kwa wananchi haraka iwezekanavyo.

Walisema wamekuwa wakitumia gharama kubwa kila siku kwenda Tanesco kwa ajili ya kupata mrejesho wa lini wataunganishiwa huduma ya umeme lakini hawajapata maelezo ya kueleweka.

Walisema kero yao kubwa ni kuwa tatizo hilo halijatatuliwa licha ya kulifikisha kwa viongozi wa Mkoa na Wilaya wamekosa majibu kwa muda miezi kadhaa, licha ya kufanya jitihada zao za kutafuta maelezo kwa wahusika.

Katika hatua nyingine Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo na Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqarro, walisema juhudi za kutatua kero hiyo zinaendelea kufanyika.

Akijibu malalamiko hayo Meneja wa Tanesco Mkoa wa Arusha, Herini Mhina, alisema kwa sasa shirika hilo, linakabiliwa na tatizo la upungufu wa nguzo za umeme, jambo linalokwamisha usambazaji wa nishati hiyo.





# Wasikitika mradi wa umwagiliaji

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

WADAU wa uzalishaji wa mazao ya chakula katika skimu ya umwagiliaji ya soko Wilaya ya Moshi, wameeleza masikitiko yao kuhusu mradi wa uimarishaji wa skimu hiyo kutengewa Sh. milioni 150 ambazo hauwezi kukidhi mahitaji ya kuzalisha malighafi kwa ajili ya viwanda.

Skimu hiyo yenye wakulima zaidi ya 270, inahudumiwa na wananchi wa vijiji vitatu vya Kiterini, Soko na Kyomu.

Baadhi ya wakulima walitoa dukuduku lao juzi, ikiwa ni siku chache baada ya kamati ya siasa ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Kilimanjaro, kupita eneo hilo la Kata ya Kahe Mashariki na kutoa maelekezo kwa serikali kuongeza fedha zaidi kwa ajili ya kuboresha skimu hiyo ili kuondoa malalamiko ya wakulima.

Mmoja wa wakulima hao, Kabanga Alli, alisema kilimo cha umwagiliaji ili kiwe endelevu na chenye tija kuweza kufikia Tanzania ya viwanda, uwekezaji wa miundo mbinu ya kisasa, mitaji, maofisa ughani na uwezeshwaji kiuchumi wa wakulima wenye mambo muhimu yanayopaswa kuzingatiwa.

Rehema Mgonja alisema: "Ukitazama kiasi cha fedha ambacho serikali imewekeza nadhani bado ni kidogo, ikilinganishwa na mahitaji ya viwanda vyetu hasa vya kuongeza mnyororo wa thamani mazao ya mpunga, mbogamboga na mahindi. Tunashauri serikali kwa maana ya halmashauri yetu kuongeza fungu la kuimarisha miundombinu ya skimu ya soko."

Greyson Badueli alisema pamoja na uwekezaji huo, wakulima wanaomiliki vitalu katika skimu ya soko, hawajapewa elimu ya kutosha ya kujiunga katika vyama vya umwagiliaji.

Alisema jambo hilo kama litafanywa na watendaji wa serikali, litasaidia wakulima kusimamia na kuihudumia vyema miundo mbinu ya umwagiliaji ili iwe endelevu kwa kulipia ada za uendeshaji, matunzo na matumizi ya maji.

Juzi, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Kastori Msigala, akizungumza na wakulima hao, alisema mradi huo unaendeshwa na umoja wa wakulima wa umwagiliaji soko (Uwaso) na una jumla ya wakulima 270.

Sheria ya Umwagiliaji, Namba 5 ya Mwaka 2013, na Kanuni zake za Mwaka 2015, inahamasisha skimu za umwagiliaji kusimamiwa na kuendelezwa na vyama vya umwagiliaji ili ziweze kuwa na ufanisi zaidi.

Alisema chanzo cha maji ya skimu hiyo ni mto soko na kwamba zao kuu linalolimwa katika skimu hiyo ni zao la mpunga na mazao mengine ni mboga mboga, matunda na mahindi.

Alisema eneo linalofaa kwa umwagiliaji ni hekta 400 na kwamba hadi sasa, eneo lililoendelezwa ni hekta 270 sawa na asilimia 67.5.

# Wataka tiba kisaikolojia ujauzito shuleni

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

WASICHANA 40 wa shule za msingi za Himo na Korona zilizopo Mji Mdogo wa Himo, Wilaya ya Moshi, wameitaka serikali kuja na mpango maalum wa tiba ya kisaikolojia kwa watoto wa kike wanaokatisha masomo yao kutokana na kupata ujauzito katika umri mdogo.

Wazo la kutaka kuwapo kwa mpango huo maalum lilitolewa jana kupitia sanaa ya ngoma na maigizo, wakati klabu za kuwajengea uwezo wasichana shuleni zilipowasilisha ujumbe wao katika maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia.

Katika maadhimisho hayo yaliyofanyika katika uwanja wa Shule ya Msingi Himo, kwa nyakati tofauti shule zilizoshiriki maadhimisho hayo zilihimiza Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kufikiria kuja na mpango huo ili kupunguza maumivu yanayojitokeza kwa waathirika hao.

Moja ya igizo la Shule ya Msingi Himo, lilieleza namna mimba za utotoni na ubakaji zinavyoendelea kuathiri kisaikolojia idadi kubwa ya wanafunzi wanaopata matatizo hayo.

Wakati, wanafunzi wa Shule ya Msingi Korona wao walitaka mpango huo pamoja na mambo mengine kuweka mkazo wa tiba ya kisaikolojia kwa wanafunzi wanaobainika kukeketwa.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Himo, Martin Minja, akizungumza na wanafunzi wa shule hizo na wazazi walioijitokeza kushiriki maadhimisho hayo alisema mwanamke au msichana anapobakwa sio kosa lake, hivyo inashauriwa apewe ushauri wa kisheria wa jinsi ya kuchukua hatua kikamilifu.

Akizungumza katika maadhimisho hayo ya kupinga ukatili wa kijinsia, Mratibu wa mpango wa kuwawezesha wasichana (GEP) unaotekelezwa na Shirika la kiraia la Kwieco kwa ufadhili wa Taasisi ya Kimataifa ya Crossroads International, Immaculate Mworia, alisema ukatili wa kisaikolojia unatajwa kama ni kitendo cha kumuumiza mtu kiakili na kihisia.

"Matumizi ya maneno mabaya kwa mtu au kuwaita majina mabaya huumiza mtu kiakili, na hii inajumuisha masuala kama uonevu, umbea na kudanganya yanayosababisha kitu kinachoitwa ukatili wa kisaikolojia," alisema Mworia.

Aidha, alieleza kuwa pamoja na mambo mengine wanawasaidia wasichana kujitambua masuala ya hedhi salama.

Pia, mpango huo unawasaidia kuwajengea uwezo katika uwezeshaji wa kiuchumi, ukatili wa kijinsia na afya ya uzazi.

"Tumetengeneza miongozo mbalimbali na miongozo hii inawalenga watoto wa sekondari na msingi.

Ni miongozo ambayo watakuwa nayo watoto hawa na watakabidhiwa kupitia wawezeshaji wao ambao ni walimu; na kimsingi tumeanzisha klabu ambazo zitakuwa na wasichana 40 katika kila shule na watakuwa na hiyo miongozo.

"Inayo elimu kamilifu ambayo itawasaidia wasichana wawe na hamasa ya kujifahamu na kujitambua na kuweza kujijenga kwa maisha ya baadae. Lakini pia wataweza kuelimisha na wengine ambao hawajapata nafasi ya kufikiwa na Kwieco katika shughuli zake."

Mpango huo wa mwaka mmoja unatekelezwa na Shirika la Kwieco, kwa ufadhili wa Taasisi ya Kimataifa ya Crossroads International katika kata tano za Mabogini, Mwika Kaskazini, Uru Kusini, Himo na Kibosho Kati.

Kuhusu hedhi, Mworia ameeleza kuwa katika hedhi salama wamegundua kwamba wasichana wengi, bado wana ile hali ya kutojitambua kipindi gani anakuwa na hedhi, anajitunzaje akiwa katika hedhi na atumie nini kujitunza katika hedhi.

"Mabinti hawa tunaowazungumzia ni wale ambao bado hawawezi kununua vile visodo vya kuvaa (taulo za kike), hawana uwezo, kwa hiyo tunawafundisha namna ya kujitengenezea vitu vya kujihifadhi kama mabinti ili waweze kuendelea na shule, badala ya kukaa nyumbani," alieleza Mworia



Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Tanzania Women Research Foundation (Tawref), Dafrosa Itemba (wa pili kushoto), akimpongeza mwalimu Rose Chuwa wa Shule ya Msingi Pasua, Manispaa ya Moshi, baada ya kupokea cheti cha ushiriki mradi wa kudhibiti virusi vya Ukimwi kwenye shule za msingi, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkakati Same ya kijani waamsha wadau

**Na Mwandishi Wetu,** SAME

MKAKATI wa serikali katika Wilaya ya Same, wa kuifanya kuwa ya kijani umeanza kupata mwitikio, baada ya baadhi ya wadau wa mazingira kuanza kujitokeza kuunga mkono juhudi hizo kwa kupanda miti zaidi ya 46,000 maeneo mbalimbali yanayozunguka mji huo.

Jana, Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule alikuwa akitoa taarifa kuhusu maelekezo ya Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, ambayo yametekelezwa na wilaya hiyo hadi sasa. Akizungumzia utekelezaji wa maelekezo ya Makamu wa Rais, Senyamule alisema: "Tumesema tutapanda miti zaidi ya milioni mbili kwa mwaka huu na tutaanzia pale round about mpya. "Mkakati wetu wa sasa ni kuubadili mji wa Same na kuupa alama ya kipekee. Katika hilo tumeanzisha mji mpya wa kilometa moja (one kilometer city) ambao tutapanda miti kwenda kilometa moja kila upande, tumejipanga tunatamani kuiona Same mpya iliyopiga hatua kiuchumi."

Kwa mujibu wa Mkuu huyo wa Wilaya, Shirika la Floresta Tanzania limeendelea kupanda miti katika maeneo ya kimkakati Wilayani Same, ambapo katika Kata ya Suji wameshirikiana na serikali kupanda miti pembezoni mwa barabara iliyojengwa kwa kiwango cha lami.

Katika taarifa yake, alisema pamoja na mpango huo kuifanya Same kuwa ya kijani, pia utasaidia kupendezesha barabara, kukinga mmomonyoko, kukinga ajali pamoja na kusaidia mabadiliko ya tabia nchi.

Aliwataka maofisa watendaji wa kata na watendaji wa vijiji , kwa umoja wao kuweka mpango kazi wa kupanda miti ili kutekeleza mpango mkakati wa mazingira wa wilaya ili kufikia lengo la kitaifa.

ama
ALHAMISI DESEMBA 5, 2019
AFYA NA MAZINGIRA



**UTAFITI ISRAELI**
**Bakteria kulishwa hewa ukaa, ushindi au kuzidishwa shida?**
Ukurasa 20



**JICHO SIKU 16 KUPINGA UKATILI JINSIA**
Wanaharakati wapaza ‘ Tanzania bila ukatili jinsia inawezekana’
Ukurasa 14



Ukurasa 18
**Zilivyokuwa saa 48 Dunia ya Mafuriko**



MRATIBU MAGONJWA...
# Ndivyo kilivyo kichocho kitafunacho robo tatu jiji Mwanza na wilaya zake
Ukurasa 16

# Rekodi Tiger azurura na kurudi 'Dar- Nairobi'



Mnyama Tiger, katika nyendo zake. **PICHA: MTANDAO.**

**Maharashtra, India**

MNYAMA aina ya Tiger, ambaye ni aina fulani ya jamii ya chui, ameweka rekodi nchini kwa kutembea umbali mrefu wa kilomita 1300 ndani ya miezi mitano, ambao haujafikiwa na mnyama mwingine.

Hiyo ni sawa na umbali kutoka jijini Dar es Salaam hadi Nairobi na kurudi, kukiwa na ziada ya wastani wa kiliomita 40, kwa maana sawa na umbali kutoka Mwenge jijini Dar es Salaam hadi Bagamoyo.

Utafiti uliofanyika kwa kumfuatilia mnyama huyo dume kupitia mifumo ya satelaiti - GPS, alivuka maeneo mbalimbali akipita mtoni, milimani na msituni, katika mfumo wake wa maisha kama walivyo wanyama wengine wanaohamahama.

"Kuna uwezekano Tiger anatafuta himaya, chakula na wenzake (nchini India). Wapo wengi wa kuwachunguza," anasema Dk. Bilal Habib, Mwanabailojia Mwandamizi kutoka Taasisi ya Wanyamapori ya India. Inaelezwa, tabia ya mnyama huyo huwa anasafiri usiku, huku akiwakuta nguruwe pori na jamii ya ngombe akiwaua kupata mlo.

Hata hivyo, katika vurugu zake hizo ni nadra kumdhuru binadamu na katika historia ya safari ya tiger huyo aliyefuatiliwa, alimdhuru binadamu mara moja tu ikitajwa ilikuwa 'bahati mbaya.'

Kwa mujibu wa shirika la habari AFP, nchini India kunakadiriwa kuhifadhi asilimia 70 ya wanyama hao duniani, jumla yao ikiongezeka kwa kadirio wako 500.

AFYA

JICHO SIKU 16 KUPINGA UKATILI JINSIA

# Wanaharakati wapaza ' Tanzania bila ukatili jinsia inawezekana'

## •Waziri Ummy, wadau 50 washikamana




Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Wazee na watoto, Ummy Mwalimu, akizungumza na waliohudhuria uzinduzi wa Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia mkoani Dodoma. Kushoto kwake ni, Katibu Mkuu wa Wizara, Dk. John Jingu, akifuatiwa na Mkurugenzi wa Wildaf, Wakili Anna Kulaya mwisho kulia, ni Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini, Patrobas Katambi. **PICHA: BLOGU YA CCM.**

**Na Mwandishi Wetu, aliyekuwa Dodoma**

SHAMRASHAMRA za siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia zilizinduliwa hivi karibuni jijini Dodoma na mamia ya wanaharakati wa mikoa yote walishiriki katika siku hiyo muhimu kwa ajili ya vita vya haki za kupinga ukatili.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, ndiye aliyezindua siku hizo 16, ambazo kwa kawaida kila mwaka huishia mpaka Desemba 10, wadau mbalimbali wakiadhimisha kwa shughuli mbalimbali za kutoa msaada wa kisheria.

Baadhi ni hughuli zinazofanywa na mashirika yasiyo ya kiserikali katika siku hizo 16 zinaangukia kaulimbiu ya mwaka 'Kizazi Chenye Usawa: Simama Dhidi ya Ubakaji.

Mtazamo uliopo ni kuhakikisha asasi zinatoa msaada wa kisheria na elimu kwa wananchi wa kawaida, ili wanapopata matatizo ya ukatili wa kijinsia waweze kujua mahali pa kuripoti matukio hayo.

Wadau hao wanasema, mwamko na watu kwenda kuripoti matukio ya ukatili wa kijinsia kwenye madawati mbalimbali yaliyoanzishwa polisi na kwenye maeneo mbalimbali umeongezeka na ndiyo sababu idadi ya matukio ambayo imekuwa ikitangazwa na kuongezeka kila kukicha.

Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Africa (Wildaf), kwa kushirikiana na Mtandao wa Kupinga Ukatili wa Kijinsia (Mkuki) ambayo ni mashirika zaidi ya 50 ndio waliratibu uzinduzi wa kampeni hizo 16 ambazo kwa mwaka huu zilifana kwa kiwango kikubwa, kulinganisha na miaka mingine.

Idadi kubwa ya watu walijitokeza kwenye uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma, kukiwapo mashirika mengi yasiyo ya kiserikali yaliyokuwa yakiendesha shughuli za kutoa msaada wa kisheria na elimu ya sheria kwa wageni waliofika uwanjani hapo.

Baadhi ya asasi zilizoshirikiana na Wildaf, kufanikisha uzinduzi huo, ni pamoja na: UN Women, Legal Services Facility (LSF), Foundation for Civil Society, Irish Aid, Pact Tanzania, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Women Trust Fund, Restless Development na Freedom House.

BOSI WILDAF

> **"Hii itasaidia sana kuharakisha kesi za ubakaji na nyinginezo za ukatili na hivyo kuongeza imani na moyo kwa wananchi kutoa ushirikiano endapo watatakiwa kutoa ushahidi.**

Mkurugenzi wa Wildaf, Wakili Anna Kulaya, anasema kumekuwapo mitazamo tofauti kwenye jamii, hasa inapofika katika utoaji ushahidi wa matukio ya ubakaji, kwani kwa bahati mbaya wanaofanya hivyo ni ndugu na jamaa wa karibu.

Mkurugenzi huyo anasema, ni hali inayosababisha ama kuharibika au kutokamilika kesi nyingi, sababu kuu ni kukosekana ushahidi kamili na ushirikiano wa kutosha kutoka kwenye familia husika, majirani na waliosh uhudia vitendo hivyo.

Anabainisha, mara nyingi kesi za ubakaji zimekuwa tatizo kwa sababu ya ama hofu, aibu au kuogopa kunyanyapaliwa, pale mtu anapoamua kusimama kuhakikisha haki inatendeka kwa aliyeathiriwa na ubakaji.

Kwa mujibu wa Anna, kesi nyingi zina historia ya kuchukua muda mrefu kumalizika, hali inayoifanya kutoa mwanya kwa ndugu na jamaa kumalizana nyumbani, kwani hasira inakuwa imeshapoa.

"Ni kutokana na changamoto hizo, wadau wa Mkuki tunaamini muda umefika sasa wa kuwa na sheria maalum inayoshughulikia masuala ya ukatili pamoja na mahakama za familia.

"Hii itasaidia sana kuharakisha kesi za ubakaji na nyinginezo za ukatili na hivyo kuongeza imani na moyo kwa wananchi kutoa ushirikiano endapo watatakiwa kutoa ushahidi.

"Kaulimbiu inasisitiza kila mmoja wetu kusimama katika nafasi yake kukemea, kuchukua hatua dhidi ya vitendo vya ubakaji,

**Inaendelea Uk. 15**

AFYA

Inatoka Uk. 14

kwani tukiunganisha nguvu zetu kwa pamoja, tunaweza kupunguza au kumaliza kabisa vitendo hivi viovu.

'Waswahili wanasema 'kidole kimoja hakivunji chawa.' Hivyo ni jukumu letu sote kusimama dhidi ya vitendo hivi vya ubakaji," anasimulia Anna

WAZIRI UMMY

Waziri Ummy, aliyekuwa mgeni rasmi kwenye uzinduzi huo, anasema serikali inadhamira kupambana na ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto, kwa mujibu wa maelekezo rasmi ya yaliyopo kiserikali.

Anasema, serikali inadhamiria kuona wanawake na watoto wanapata haki ya kulindwa dhidi ya ubaguzi, udhalilishaji, dhuluma, unyanyasaji, ukatili wa kijinsia na mila potofu, katika kuzingatia azma hiyo, serikali iliandaa na inaratibu utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTTAKUWA 2018-2022).

Waziri anautaja kuwa ni mpango unaolenga kupunguza nusu ya ukatili kwa wanawake na watoto, ifikapo mwaka 2022, ikwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya mwaka 2000.

Ummy anataja hatua ambazo serikali imezichukua, ni pamoja na kuanzishwa madawati ya jinsia na watoto katika vituo vya polisi, jumla yake sasa yako 420 yanayofanyakazi kwa lengo la kuwezesha huduma stahiki kwa wote wanaofanyiwa ukatili wa huo wa kijinsia.

"Madawati ya jinsia yamewezesha jumla ya watu 96,424 waliofanyiwa ukatili wa kijinsia kupata huduma stahiki. Mwaka 2015, watu 23,012; mwaka 2016 watu 31,996; na mwaka 2017 watu 41,416 walipatiwa huduma hizo," anasema.

Ummy anaongeza: Pia, tumeongeza vituo vya huduma za 'mkono kwa mkono' vya kutoa huduma kwa waathiriwa wa vitendo hivi, kutoka vituo vine mwaka 2015/2016 hadi vituo 13 mwaka huu."

Waziri huyo anasema, vituo hivyo vimeanzishwa kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Mwanza, Mbeya, Iringa na Shinyanga, lengo ni kutoa huduma rafiki na za haraka kwa waathiriwa wa matukio ya ukatili kijinsia.

Anasema kwamba, wameendelea kutoa huduma ya simu bila malipo kwa watoto wanaofanyiwa ukatili, ili taarifa zifikie haraka kwa mamlaka zinazohusika.

Kwa mujibu wa Waziri Ummy, watoto hao wamekuwa wakiunganishwa na huduma mbalimbali za kijamii kama polisi, hospitali, ustawi wa jamii na mahakama na tayari kuna jumla ya watoto 493 waliohudumiwa; mwaka 2016 na hadi sasa kuna jumla ya watoto 3,833 wamefiki-

## JICHO SIKU 16 KUPINGA UKATILI JINSIA

# Wanaharakati wapaza ' Tanzania bila ukatili jinsia inawezekana'




Katibu Mkuu Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Dk. John Jingu, akizungumzia chimbuko wa siku 16 za Kampeni ya kupinga ukatili wa kijinsia katika uzinduzi uliyofanyika kitaifa jijini Dodoma.

> **"Madawati ya jinsia yamewezesha jumla ya watu 96,424 waliofanyiwa ukatili wa kijinsia kupata huduma stahiki. Mwaka 2015, watu 23,012; mwaka 2016 watu 31,996; na mwaka 2017 watu 41,416 walipatiwa huduma hizo," anasema.**

wa na huduma hiyo.

Waziri Ummy anatumia nafsi hiyo kuwaagiza maofisa maendeleo ya jamii wa mikoa na halmashauri zote kuhakikisha wanasimamia uanzishwaji na uendeshwaji wa Kamati za Ulinzi wa Wanawake na watoto ngazi za mikoa, wilaya, kata na vijiji.

Anasema, uanzishwaji kamati hizo ni maelekezo ya mwongozo wa mpango wa taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Ummy anaagiza, maofisa maendeleo ya jamii na ustawi wa jamii wa halmashauri zote kuanzisha programu za kijamii za kutokomeza ukatili wa kijinsia na kutoa msaada kwa wathiriwa wa vitendo vya ukatili, kwenye halmashauri husika.

Waziri Ummy anasema, kampeni ya kupiga vita ukatili wa kijinsia, inahusu wanaume na wanawake hivyo hakuna sababu ya wanaume kuona haya kwenda kutoa taarifa wanapofanyiwa vitendo vya aina hiyo.

Anasema, wanaume wanaofanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia na wake zao kuacha kuona aibu kuomba msaada na badala yake watoe taarifa kwenye madawati ya kijinsia, wasaidiwe kupata haki zao.



Baadhi ya wanafunzi kutoka Shule za Sekondari za Mkoa wa Dodoma wakiwa katika uzinduzi wa siku 16 za Kampeni ya kupinga ukatili wa kijinsia iliyofanyika kitaifa jijini Dodoma.
**PICHA ZOTE: BLOGU YA CCM.**

AFYA

## MRATIBU MAGONJWA...

# Ndivyo kilivyo kichocho kitafunacho robo tatu jiji Mwanza na wilaya zake

- Namba moja wavuvi, Pili, wako Mwaloni
- Kinachojiri Ukerewe shida ya 'kimataifa'

**Na Anthony Gervas, MWANZA**

ALHAMISI wiki iliyopita, ilikuwa sehemu ya tatu ya mfululizo wa simulizi za matatizo ya kiafya na hatua zinazochukuliwa mkoani hapa, kuanzia na mzizi mkuu wa katika Hospitali ya Rufani ya Sekou Toure hadi mkoa mzima wa Mwanza. Endelea na sehemu ya nne kuhusu namna maradhi ya kichocho na minyoo tumbo ilivyo donda sugu kimkoa. Mratibu wa Magonjwa Yasiyopatiwa Kipaumbele Mkoa, Dk. Mabai Thobias ana simulizi inayojitosheleza. Fuatilia.

--"HAKUNA wilaya ya Mwanza iliyo salama katika ugonjwa wa kichocho na minyoo ya tumbo. Hizo ni takwimu zilizokusanywa kutoka kwenye vituo vya afya mwaka jana, zilizokuwa zikionyesha kuwa watu wengi katika mkoa huo, walikuwa wameathirika na kichocho," anaeleza Dk. Mabai Thobias.

Mkoa wa Mwanza una wilaya za Ukerewe ambayo ni kisiwa cha Ziwa Victoria na zinyime zilizopakana na Victoria ni Sengerema Nyamagana, Ilemela, Magu, Misungwi na Buchosa. Kwimba ndiyo pekee haijapakana na maji.

Dk.Thobias, Mratibu wa Magonjwa yasiyopewa kipaumbele wa mkoa katika mazungumzo maalum na Nipashe ofisini kwake hivi karibuni, anaieleza kichocho ni minyoo inayosababishwa na vimelea anavyoviita kitaalamu 'schistosoma' vinavyoenezwa na konokono, ikiwa na dalili za mtu kuumwa tumbo na kukojoa damu.

Pia, anaieleza minyoo ya tumbo intawaliwa na sifa za kukohoa, kutokwa vipelele na kuwashwa, kupata kichefuchefu, utumbo kujisokota, kuharisha na kutapika damu.

Mratibu huyo anafafanua takwimu kutoka katika vituo vya kukusanyia taarifa za afya mkoani mwaka jana, akisema:"Watu waliokuwa wameathirika na ugonjwa wa kichocho pekee Wilaya ya Ukerewe zaidi ya watu 1765; Buchosa watu 1000; Nyamagana watu 600 na Ilemela zaidi ya watu 572."

"Katika takwimu za minyoo ya tumbo mwaka 2018, waathirika wa ugonjwa huo mkoa wa Mwanza walikuwa 17, 000, Ilemela zaidi ya watu 9, 000, Ukerewe zaidi ya watu 7, 000, Sengerema zaidi ya watu 5,000 na Buchosa zaidi ya watu 5,000."

Dk.Thobias, anaeleza dalili za kichocho huchelewa kuonekana, hali inayomfanya mgonjwa kuchelewa kupata matibabu mapema na hata baadaye yanapoonekana, mgonjwa anakuwa na madhara makubwa.



Maeneo ya pwani ya Ziwa Victoria na milima ya mawe jijini Mwanza, mandhari rafiki kwa kusambaa kichocho.

> **"Katika takwimu za minyoo ya tumbo mwaka 2018, waathirika wa ugonjwa huo mkoa wa Mwanza walikuwa 17, 000, Ilemela zaidi ya watu 9, 000, Ukerewe zaidi ya watu 7, 000, Sengerema zaidi ya watu 5,000 na Buchosa zaidi ya watu 5,000."**

Mratibu anafafanua:"Yapo magonjwa mengi, lakini kwa mpango wa taifa unaodhibiti magonjwa hayo. Mpango huo umeanza na magonjwa matano yanayodhibitiwa kwa pamoja, ambayo ni kichocho cha tumbo na kichocho cha kibofu cha mkojo na minyoo ya tumbo.

"Minyoo ya tumbo iko aina tatu. Kuna minyoo ya safura, mijeredi na mviringo. Pia, magonjwa mengine ni ugonjwa wa kope, (trakoma) ugonjwa wa usubi, ambao hupatikana katika sehemu za mito inayotiririka kwa kasi, lakini yapo mengine ya matende na mabusha ambayo hupatikana pande za Pwani."

Anaendelea kwamba usubi hupatikana katiKa ukanda wa Pwani na Nyanda za Juu, kwenye mito, milima, maporomoko ya maji akitaja baadhi ya maeneo hayo ni kama Wilaya ya Mahenge, mkoani Morogoro na ukope unapatikana zaidi katika maeneo kame, akitaja mifano ya mikoa Dodoma, Singida na Arusha.

KICHOCHO MWALONI

"Kwa Kanda ya Ziwa tumeathirika zaidi na ugonjwa wa kichocho pamoja na minyooo ya tumbo, ambayo uwepo wake hupatikana kwenye maji ya mabwawa, mito na maziwa," anasema.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, maambukizi ya kichocho huenezwa na konokono wanaopevua mayai yanayotoa viluwiluwi vya maambukizi ya ugonjwa huo na kumuingia anayekojoa au kuingia majini.

Anafafanua, vivyo hivyo maambukizi huendelea kwa binadamu anayeisaidia katika vyanzo vya maji na ana kichocho, mwingine akitumia maji hayo anapata maambukizi hayo, kwa mfano anapoogelea, kuchota maji au kufua nguo.

"Dalili za kichocho ni mtu kuumwa tumbo, kukojoa damu akichelewa kwenda kupata matibabu na hata kupata kansa ya kibofu cha mkojo wakiwa tumboni vimelea hao, kuathirika mfumo mzima wa chakula ndani ya tumbo, kuathiri ini, bandama na kongosho,' anaeleza.

Aidha, Dk.Thobias anaeleza dalili zingine za ugonjwa huo, mbali na vimelea kukaa muda mrefu bila aliyeambukizwa kujitambua, hukaa katika kuta za damu na kuathiri kuta za utumbo.

Zingine kwa mujibu wa daktari huyo, ni kusababisha kuvimba tumbo na kujaa maji mithili mwenye kitambi, kupasuka mishipa ya damu, kutapika damu na akichelewa kupata matibabu, kuna hatari ya kupoteza maisha.

Mratibu huyo wa Magonjwa Yasiyopewa Kipaumbele, anasema utafiti uliofanywa na Mradi wa Udhibiti Endelevu wa Kichocho, katika miaka miwili kwenye Wilaya za Ilemela na Nyamagana mwaka jana jijini Mwanza, jamii zinazoishi kando ya Ziwa Victoria kwenye mialo, iligundulika kati ya watu 10, wakazi saba hadi wanane (asilimia 70 hadi 80) wana kichocho.

Anasema ni utafiti huo uliofanyika kwa lengo la kuelimisha jamii na utoaji wa matibabu na kinga katika jamii zilizoko kando ya Ziwa na mialo.

Dk. Thobias anataja mkakati kuelekea mwakani 2020, ni ajenda ya kila mmoja kuhakikisha anatoa ushirikiano katika utoaji elimu kwa jamii, ikiwamo vyombo vya habari kuhusu tiba na kujikinga na ugonjwa huo.

Anasema mwaka jana, sekta ya afya kwa kushirikiana na sekta ya elimu, waliwafikia watoto zaidi ya 700,000 katika jumla ya shule zote 967 za mkoa Mwanza na kuwapa kinga tiba.

"Ugonjwa wa kichocho upo, hakuna wilaya iliyo salama katika Mkoa wa Mwanza Ilemela na Nyamagana, zaidi ya asilimia 80," anaeleza Dk,Thobias, anayefafanua kwamba ugonjwa huo uko katika aina mbili anazozotaja kuwa 'kichocho cha tumbo' na 'kichocho cha kibofu cha mkojo.'

Anaorodhesha dalili zake ni kuumwa tumbo, kukojoa damu, kuathirika kwa mfumo mzima wa chakula ndani ya tumbo, kupata kansa ya kibofu cha mkojo, pia anaweza kupoteza maisha.

Aidha kundi la wavuvi ziwa vichoria linadaiwa ndilo liko kwenye hatari zaidi ya kuathirika na kichocho, kutokana na shughuli zao za kukaa kwenye maji saa nyingi kuvua samaki na kutumia maji hayo yasiyo salama.



Makazi ya aina yake wilayani Sengerema: **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU.**

MINYOO TUMBO

Dk. Thobias, anataja aina tatu za minyoo ya tumbo' ambayo ni ya safura, mijeredi na mviringo, anayoitaja kuwa ya hatari kwa mgonjwa na dalili zake ni kukohoa, kutokwa vipelele, kuwashwa, kupata kichefuchefu, utumbo kujisokota, kuharisha na kutapika damu anapochelewa kwenda kupata matibabu mapema katika vituo vya afya au hospitali.

"Kundi linaloathirika zaidi na ugonjwa wa minyoo ya tumbo ni watoto wenye umri wa kwenda shule kuanzia miaka mitano hadi watu wazima miaka 60," Dk. Thobias anasema na kufafanua sababu kwamba:

"Kutokana na kutumia vyakula visivyokuwa salama, vikiwemo kachumbali, karoti, kabichi, kutonawa mikono akitoka kujisaidia chooni, kutembea peku na kutokuwa na vyoo."

Anawaasa wakazi wote wa Mwanza kujenga utamaduni wa kuzingatia kanuni za huduma za afya, kwenda katika vituo kupima afya zao, badala ya kubuni matibabu wakiwa nyumbani na kutumia dawa za miti shamba, akihitimisha kwamba 'kinga ni bora kuliko tiba.'

Mwandishi anapatikana Kanda ya Ziwa kwa amwani ya baruapepe: anthonygervas@yahoo.com na simu (+255) 0682 86 92 44.



Mazingira ya 'magonjwa' ya kutumia simu. **PICHA: MTANDAO.**

# Ulevi utumiaji simu janja wageuka maradhi ya akili

**Na Mwandishi Wetu**

WATAFITI wa masuala ya akili ya binadamu wamegundua kupenda kupita kiasi mbwembwe zizomo katika simu janja sasa inachukua sura ya ugonjwa wa akili kwao vijana.

Utafiti uliofanyika kutoka Chuo cha King's cha jijini London, unasema ni haki iliyofika mbali hata kijana huyo anaponyang'anywa au kuwekwa mbali na simu hizo, anachanganyikiwa.

Tatizo la vijana wanaelezwa hawana uwezo wa kusimamia muda wao katika matumizi ya simu hizo na wenyewe wataalamu wanaitafsiri ni sehemu ya maradhi ya akili.

Ni utafiti uliowagusa vijana 42,000 na simu zao. Asilimia 23 ya kundi hilo kwa maana ya vijana 9,660 simu wameshaharibiwa kiasi cha kukosa muda wa kushughulikika mengine au matumizi ya kawaida ya simu. Ni tabia iliyowaathiri kwa mengine ya kimaisha.

Athari za moja kwa moja tajwa zinajumuisha uchovu, hisia za msongo wa mawazo, kuzubaa, hawalali na masomoni wanafanya vibaya.

"Simu janja zinaendelea kuwapo, kuna haja ya kuelewa kuongezeka tatizo la simu janja," anatamka mmoja wa waandaji ripoti hiyo ya kitafiti, Nicola Kalk anayeongeza: "Hatuelewi kama ni simu janja zenyewe ndizo zinalewetea au 'apps' zake zinazotumiwa na watu."

"Pia, kuna haja ya kuwapo muamsho wa umma kuhusu simu janja zinazotumiwa na watoto na vijana. Wazazi wanapaswa kujua kiasi cha muda watoto wao wanatumia simu zao."

Msomi mwingine, Samantha Sohn, ambaye pia ni mtafiti na mwandishi mkuu wa ripoti hiyo kuhusu ulevi wa simu janja, ana ufafanuzi: "Inaweza kuwa na athari kubwa katika akili za maisha ya kila siku. Kunahitajika uchunguzi zaidi katika matumizi ya simu janja."

Mtafiti, Dk. Amy Orben, kutoka Chuo Kikuu cha Cambridge, Uingereza ambaye hakusjuriki kutafiti, anasoma ripoti na anakumbusha si vyema kuoanisha moja kwa moja matumizi ya simu janja na kuwapo msongo wa mawazo uliopitiliza. Kuna mengi ya ziada.

"Ilitafitiwa huko nyuma kwamba matumizi ya simu janja katika mtazamo mmoja pekee, ila hisia hiyo nayo ina athari pia katika matumizi ya simu janja," anasema Dk. Orben.

Kuna utafiti uliofanywa na shirika la habari kuangalia tabia za mtoto wa miaka 12 na kijana wa kiume mwenye umri wa kati, juu ya namna anavyotekwa na simu hizo.

Hapo iligundulika binti alizama kwa asilimia zote, huku kijanawa kiume walau kuna wakati alijirudisha katika matumizi ya kawaida, ingawa anakiri alishakuwa mlevi.

Tangu mwezi Septemba iliyopita, kampuni ya Apple, imezindua programu iitwayo 'ScreenTime' ambayo mtumiaji anaweza kujitathmini matumizi yake. Kampuni ya Android, tayari inayo, ikisaidia mtu kujitathmini.

Watu hao waliofanyiwa uangalizi wa kitafiti, waliweka programu za kompyuta na wakakutana kukaguana, nani ametumia muda mrefu katika 'ulevi' wa simu hizo.

- **Makala hii ni kwa mujibu wa taarifa za kimataifa.**

MAZINGIRA

# Zilivyokuwa saa 48 Dunia ya Mafuriko

- Ngumu kuamini lori lasombwa darajani
- Basi letu? Tulitokea dirishani, maji kiuno
- Saa 5 nashuhudia vijana wavushaji 'buku'
- Kurudi kupitia mbadala, mji 'umesombwa'



Abiria wakisubiri maji yapungue kwenye daraja la Tirina. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA.**

**Na Sabato Kasika, aliyekuwa Serengeti**

SIKU ya Jumatano wiki iliyopita nilikuwa abiria katika safari ya kati ya Dar es Salaam na Mwanza, mwelekeo wangu ukiwa Mugumu Serengeti, mkoani Mara.Tulifika jijini Mwanza majira ya saa 6.30 usiku na kulala hadi asubuhi, nikitafuta usafiri mwingine kwenda Mugumu.

Alfajiri ya Alhamisi, niliwahi kwenye stendi ya mabasi ya Buzuruga na kupata usafiri wa basi kati ya jijini Mwanza na Mugumu.

Kondakta alinitaarifu basi litaanza safari saa 3.00 asubuhi, hivyo nisiwe mbali. Nikiwa nimepunzimka ndani ya gari kusubiria safari, nilimuuliza kondakta muda wa kufika Mugumu, naye akajibu ni kati ya saa 8.30 hadi saa tisa kamili. Muda ulipotimu safari ya kuelekea Mugumu ilianza.

Njiani basi lilisimama na kuchukua abiria, kwa kuwa lilikuwa lina nafasi na kufika Bunda majira ya saa tano na nusu likuwa na abiria wa kutosha.

Baadaye safari ilianza tukiwa tumeacha barabara ya lami inayokwenda mjini Musoma na kuelekea kulia, ambako kuna barabara ya vumbi kwenda Mugumu.

Hapo si haba kutaja maeneo ya kupita kama vile, Nyamuswa na Salama, hadi kufika mpaka wa wilaya za Bunda na Serengeti, ambako kuna daraja la Tirina linalotenganisha wilaya hizo mbili.

**GARI LASOMBWA**

Ilikuwa majira yasa 6.00 mchana.Pasipo kutarajia, nilishuhudia maji mengi yaliyojaa kwenye barabara hiyo yakitokea Kaskazini kwenda Kusini na kusababisha magari kusimama.

Madereva walilazimika kusimamisha magari kusubiri kwanza maji hayo yapungue kwanza, ili kuepusha madhara, ambayo yangeweza kutokea iwapo wangelazimisha kuvuka upande wa pili.

Hata hivyo, dereva wa lori aina ya Scania lenye trela, ambaye alikuwa akitokea Mugumu, alilazimisha kupitia kwenye maji hayo. Hapo ni ghafla mithili ya tamthilia, gari lake ilizolewa na maji likalala upande.

> **Ni hali iliyosababisha maji kuingia ndani, huku abiria tukilazimika kupitia madirishani kujinusuru na wengine wanasita kutoka ndani ya basi wakihofia kuzolewa na maji.**

Naam! Ilikuwa taharuki na mshangao zenye ujumbe wa salamu, kwanini madereva wanaambiwa 'wasubiri.'Ni hali iliyomfanya dereva wa llori na timu yake kufungua milango kwenda juu ya gari, kisha wakavushwa ng'ambo ya pili na vijana waliokuwapo eneo hilo.

Ni maisha mapya yaliyoendana na biashara ya kumvusha mtu mmoja anayetaka kwenda ng'ambo ya pili, kati ya Sh. 500 hadi Sh.1,000. Vijana walichangamkia 'hapa kazi tu' biashara iliyodumu kuanzia ushuhuda wangu wa kwanza saa sita hadi tulipoondoka eneo hilo majira ya saa 11 jioni.

**BASI LETU LASOMBWA**

Majira ya saa 11 jioni, madereva wa mabasi mawili yaliyokuwa yakielekea Mugumu, waliamua kuwasha na kuwaambia abiria wao kwamba wapande, ili safari ya kuelekea Mugumu iendelee.

Baadhi walipanda na wengine walibaki kuhofia shaka ya kusombwa na maji hayo. Ni bahati nzuri, yalipita na kufanikiwa kufika ng'ambo ya pili, kwa mazingira ya 'vuta nikuvite' kati ya dereva na gari lake, dhidi maji ya mafuRiko.

Dereva wa basi letu ambaye muda wote alionekana kuyahofia maji hayo, huku baadhi ya abiria wakimshauri asubiri kwanza yapungue, aliliwasha na kuwaambia abiria wake 'ingieni tuondoke.;

Mimi nilikuwa wa kwanza kupanda basi na kukaa kwenye siti yangu ya mbele na begi langu dogo la kuweka mgongoni, lakini nikiwa makini kupita kiasi kufuatilia kinachoendelea mbele barabarani.' Hapo nilishachukua hatua, vitu vyangu muhimu kama simu nilishaweka kwenye mfuko wa jaketi, ambalo nilikuwa nimejifunga shingoni.

Safari ya kuvuka mto ikaanza. Nilipokaribia katikati, basi lilivutwa na maji na kumshinda dereva na kujikuta limelala upande. Mambo yakawa mambo!

Ni hali iliyosababisha maji kuingia ndani, huku abiria tukilazimika kupitia madirishani kuijinusuru na wengine wanasita kutoka ndani ya basi wakihofia kuzolewa na maji.

Binafsi nilifanikiwa kupitia dirishani na kuingia ndani ya maji hayo yaliyokuwa yamefikia kiunoni na kuanza kutembea taratibu tena kwa umakini hadi ng'ambo.

Nilipofanikiwa tu kuvukai, huku wengine wakitozwa fedha za kuvushwa maji hayo, sikutaka kupoteza muda. Nilipanda moja ya mabsi yaliyofanikiwa kuvuka maji hayo.

**BAADA MTO MAFURIKO**

Haraka iliyosababishwa na kukaa kwa muda mrefu eneo la hatari, ilinifanya hata nisijue jina la basi, bali nakumbuka nauli ya Sh.5,000 safari ikaanza na hatimaye kufika Mugumu, saa moja usiku.

Huko nako nikakuta mvua ambayo wenyeji wangu walisema, ilianza kunyesha tangu mchana wa siku hiyo na kuliwapo baridi kali, hata nikalazimika kujikunyata kwenye jaketi langu.

Asubuhi ya siku iliyofuata Ijumaa, hakukuwapo mvua asubuhi, lakini majira ya saa saba mchana, ilianza kunyesha hadi saa 11 jioni.

Jumamosi ilikuwa tofauti, hali ilikiwa shwari na bada ya kutimiza kilichonipeleka huko, nilianza safari ya kurudi Dar es Salaam, lakini hapo nikishituka, Sikuwa tayari kupitia tena njia niliyokumbana na chupuchupu ya kifo cha maji, badala yake nikapitia barabara ya Kyagata hadi Musoma Mjini.

**MAFURIKO MUSOMA**

Nilifika stendi kuu ya mabasi iliyopo eneo la Bweri, mjini Musoma majira ya saa 11 jioni. Hapo kinashangaa kusikia watu wakizungumza kuwa mvua kubwa zilizonyessha siku hiyo, zilisababisha mafuriko.

Sumulizi zenye simanzi na hofu. Maji yayojaa kwenye nyumba na kupita juu ya barabara kuu ya Musoma na kuelekea Ziwa Victoria, huku ikidaiwa kuwa yalizoa baadhi ya vitu kutoka katika nyumba hizo.

Maeneo yaliyokumbwa na mafuriko ya mvua ni Kariakoo na Machinjioni, ambako watu walijazana kuangalia namna nyumba zilizingirwa na maji, kukiwa na taarifa ya kifo cha mtu mmoja.

Si hadithi tu, bali Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Vincent Anney, alithibitisha, huku baadhi ya watu wakidai kwamba ni mara ya kwanza mji huo kukumbwa na mafuriko ya kiwago hicho.

"Mwananchi wangu mmoja amefariki dunia kutokana na mafuriko haya yaliyosababishwa na mvua kubwa ambayo kwa kweli hatukuitarajia," anasema Dk. Anney.

Kauli yale ikanena: "Huwa tunasikia na kuona kwenye vyombo vya habari mafuriko yakitokea Dar es Salaam na kwingine, lakini leo imekuwa ni zamu yetu."

Ni mafuriko yaliyopendana na mji wa Musoma kukosa umeme karibu usiku wote wa kuamkia Jumapili na mjadala ukawa kuhusu mvua hiyo iliyonyesha muda mfupi na kuleta kizaazaa kizito. Mwenyezi atuepushe na janga hilo niloshuhuda mkoani Mara. Amina.

***Soma zaidi kilichompeleka mwandishi safarini uk 19.***

AFYA

NGARIBA AFUNGUKA:

# Hiki hapa kilichojificha nyuma ya ukeketaji uliokubuhu Serengeti

## •Kwanini hawaachi? Aanika 'A' hadi' Z'



Mkuu wa Wilaya ya Serengeti, Nurdin Babu akizungumza kwenye mahafali ya wasichana walihitimu mafunzo ya ujasiriamali, waliokimbia ukeketaji. Kushoto ni Mkurugenzi wa Hope for Girls and Women Tanzania, Rhobi Samwelly. P**ICHA ZOTE: SABATO KASIKA.**

**Na Sabato Kasika, aliyekuwa Serengeti**

UKEKETAJI una madhara makubwa kwa mwanadamu, ikiwamo mhusika kutokwa damu nyingi, kuambukizwa maradhi iwapo vifaa vilivyotumiwa havikuwa safi, pia kuambukizwa na kuenea hadi katika viungo vya ndani vya uzazi, kumsababisha ugumba hata vifo.

Hatari nyingine ni kuambukizwa virusi vya Ukimwi wakati wa ukeketaji, kuziba mkojo na damu ya hedhi kwa kwa mwanamke, maumivu makali wakati wa kujamiiana na matatizo wakati wa kujifungua.

Ni hali inayoelezwa kumpunguzia mwanamke hamu ya kujamiiana, kuharibu umbile na kazi za viungo vya uzazi vya nje vya na madhara kimwili na kisaikolojia.

Kauli hiyo inatoka kwa Dk. Majaliwa Marwa, Mratibu wa Mradi wa Ukimwi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu na Maendeleo (UNFPA) nchini Tanzania.

Ingawa ukeketaji bado upo kwenye baadhi ya mikoa nchini, jitihada hizo zimechangia kuwafanya baadhi ya ngariba kuachana na kazi hiyo na kuwa waelimishaji wa jamii kuachana na mila hizo potofu.

Miongoni mwao ni Muhabe Marwa, wa mazi wa Mugumu, Serengeti mkoani Mara, anayeamua kuachana na kazi hiyo, sasa anaelimisha jamii kuacha kazi hiyo akiwa nyumba salama ya Hope for Girls and Women Tanzania.

Ngariba huyo anaweka wazi kile ambacho kimejificha nyuma ya ukeketaji na kusababisha ukatili huo kuendelea ndani ya jamii ingawa umepigwa marufuku nchini, huku wahusika wakichukuliwa hatua za kisheria.

**KILICHOJIFICHA**

Mama huyo anaiambia Nipashe, kabla ya mahafali ya wasichana waliokimbia ukeketaji na kulelewa katika nyumba salama, ngariba huyo anasema kuna biashara inafanywa na makundi matatu.

Anataja kundi la ngariba, wazee wa mila na wazazi wa watoto ambao wote wanafaidika na vitendo vya ukeketaji vinavyopingwa kila anayepiga vita ukatili.

Ngariba anafafanua kuna mgawo wa fedha zinazotokana na ukeketaji na kwamba ndicho chanzo kikuu ya kuendelea kuwapo kwa vitendo hivyo kwenye baadhi ya maeneo ikiwamo Serengeti.

"Yaani ni kwamba, kukeketa msichana mmoja ni Sh. 30,000, na katika hizo fedha, Sh, 10,000 ni ya wazee wa kimila zinazobaki ni za ngariba, lakini wazazi wanafaidika kwa kuwaoza watoto wao waliokeketwa," anasema.

"Nilianza kazi hii mwaka mwaka 2016 na kukeketa wasichana 60, ukipiga hesabu ya kila msichana Sh.30, 000, utagundua kuna kiasi kikubwa cha fedha nilipata na kuwapa wazee wa mila sehemu yao," anasema Muhabe.

Anasema, kuna wakati gharama ya ukeketaji inaongezeka kufikia Sh. 35, 000 au 40,000 kwa kila msichana iwapo atakutwa ameshaanza tendo la ndoa.

> **"Yaani ni kwamba, kukeketa msichana mmoja ni Sh. 30,000, na katika hizo fedha, Sh, 10,000 ni ya wazee wa kimila zinazobaki ni za ngariba, lakini wazazi wanafaidika kwa kuwaoza watoto wao waliokeketwa," anasema.**

"Kabla ya kukeketa huwa kuna dawa ya asili ambayo msichana anawekewa sehemu za siri, ili kubaini kama ameshaanza mambo ya kikubwa au bado. Kama atakuwa ameanza, gharama ya kukeketwa itaongezeka," anasema.

Muhabe anasema, hilo linafanyika kwa vile anayetakiwa kukeketwa ni ambaye hajajamiiana, lakini kwa kuwa anaunganishwa na wenzake, inabidi akakeketwe kwa gharama kubwa.

"Unaweza kudhani wazazi wa watoto hawafaidiki, lakini ukweli ni kwamba wanawatoa wakeketwe wakiamini kwamba baada ya hapo wataolewa na hivyo na hivyo kupata mahari," anasema.

Anasema, fedha wahusika wanazopata kwenye ukatili huo, ndizo zinasababisha baadhi ya ngariba na wazee wa mila kukumbatia mila ambazo jamii inazikataa sasa, hivyo elimu inahitajika kuepusha madhara kwa mabinti.

**ALIVYOJISALIMISHA**

Ngariba huyo anasema alianza kazi hiyo mwaka 2016, lakini mwaka uliofuata aliacha, baada ya kuelimishwa na Mkurugenzi wa taasisi ya HoPe for Girls and Women Tanzania, Rhobi Samwelly.

"Mwaka 2016 ulikuwa unagawanyika kwa mbili, hivyo nilianza kwa kukeketa wasichana 60, ila akaja Rhobi na kuniambia niache kazi hiyo nitafungwa, nimaamua kuiacha," anasema.

Anasema, baada ya hapo alichukuliwa kwenda nyumba salama iliopo Mugumu na sasa anatoa elimu kuhusu mambo ya mila na desturi kwa wasichana waliopo katika nyumba hiyo.



Ngariba mstaafu, Muhabe Mwita

**DC AWAPASHA**

Mkuu wa Wilaya ya Serengeti, Nurdin Babu, alikuwa mgeni rasmi kwenye mahafali ya wasichana waliohitimu mafunzo ya ujasiriamali, wanolelewa na Nyumba Salama ya Mjini Mugumu.

Babu anawataka ngariba, wazee wa mila na wazazi kuwaacha mabinti wasome, wasiwatese na mila zao zilizopitwa na wakati.

Anaweka bayana, serikali itaendelea kupambana na wote wanaojihusisha kwa na ukeketaji wilayani mwake, akisisitiza: "Ngariba, wazee wa mila na wazazi acheni vitendo hivyo, acheni watoto wasome kwa ajili ya maisha yao ya baadaye."

"Kama mila zenu za ukeketaji zina maana, kwanini vijana wenu wanakwenda kuoa kwingine? Hebu badilikeni na msipobadilika, jueni serikali haijalala, inaendelea kupambana na mila potofu," anasema.

Hoja yake kwa Mkurugenzi wa taasisi ya Hope for Girls and Women Tanzania, Rhobi Samwelly, asikate tamaa katika vita dhidi ya ukeketaji, kwa vile serikali iko nyuma yake.

"Ninajua kuna vitisho ambavyo umekuwa ukikutana navyo, katika vita hii. Wewe endelea usikate tamaa, serikali inaunga mkono juhudi zako na inataka vitendo vya ukeketaji vikomeshwe kwenye jamii," anasema.

*• **Kesho usikose simulizi ya ajira mapya ajira ya ngariba mstaafu.***

MAZINGIRA

## UTAFITI ISRAELI

# Bakteria kulishwa hewa ukaa, ushindi au kuzidishwa shida?

**Na Nimi Mweta**



Sehemu ya msitu ulioko nchini Israeli. Picha ndogo, wanyama wakineemeka na mlo, pia hewa safi ya oksijeni. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

WANASAYANSI nchini Israel hivi karibuni walitoa tangazo la kufanya ugunduzi wenye kila sababu za kuchangamsha hisia za watu. Ni hatua nyingine ya sayansi, ambayo ingeweza kuleta mabadiliko chanya duniani.

Suala hilo bado liko mezani. Ugunduzi huo ulivyosimama, bado hauna mchango bayana katika upunguzaji hewa chafu (carbon dioxide) kwa viumbe wanaotembea, wakati miti ni habari njema, kwa maana ni chakula chao

Ni pale watafiti waliporekebisha moja ya bakteria za kawaida hasa kwa wanaougua magonjwa ya tumbo, yaani 'e-coli' kuwa tofauti.Waliunda upya, ili ihitaji hewa ya ukaa kuishi. Muhimu, iwe nishati kuendesha miundombinu ya kimaumbile ya bakteria, ambayo ni wazo zuri tu.

Ni ugunduzi ulioleta matumaini ya haraka, kuwa mpangilio huo wa kuunda bakteria, unaweza kusaidia kupambana na mabadiliko ya tabianchi, endapo kutakuwapo nyenzo za kuzalisha kwa wingi bakteria hizo bila ya madhara kwa mazingira au gharama kubwa kupita kiasi.

Bado maswali yanaendelea kuulizwa kwa upande huo, kwani jitihada za wanasayansi kupunguza uzalishaji hewa chafu kwa nishati mbadala, haijapata mafanikio? Kwani, ubadilishaji nishati ni maeneo kadhaa tu?

Wakati huohuo, viwanda vinavyotumia nishati za jadi, vyombo vya usafiri, ni wazi vitaendelea kuongezeka, kwani nchi nyingi zenye watu wengi zinaelekea uchumi wa viwanda.

Kilichofanyika ni mwendelezo wa juhudi za wanasayansi kutafuta kitu hai kinachohitaji hewa ya ukaa, kama nishati. Hivyo, kinapokuwapo kingi katika uso wa nchi wingi wa hewa hiyo uanze kupungua.

**KIKWAZO**

Ni katika eneo la kuunda viumbehai (synthetic biology) ambako mbinu za kunyonya hewa ya ukaa kutoka angani, kwa kuitumia kama chakula cha viumbe hai vya chini kabisa vyenye uwezo huo.

Wamefikia malengo yao, lakini ushindi huo katika medani ya sayansi au utafiti, hautakuwa rahisi kuhamishia viwandani au mipango ya mazingira.

Taarifa zinasema kuna upana zaidi wa jitihada hizo, kwani suala halisi ni jinsi ya kutumia hewa hiyo ya ukaa inayoharibu mazingira, kwa kuongeza joto katika anga na hivyo kuathiri mpangilio mzima wa uwiano wa joto, mvua, barafu na vimbunga katika ardhi na bahari.

Nia, ni kutumia hewa hiyo ambayo sasa inaielemea anga kuwa chakula, nishati na dawa ya aina tofauti, ambazo zinaweza kutumika viwandani na kwingineko. Juhudi hizo zimelenga viungo vya bakteria vinavyokutanisha hewa hizo na ulimwengu wa kemikali.

**KINGO YA UTAFITI**

Utafiti uliojadiliwa kiasi ni wa mwaka 2016, wanasayansi walijaribu kuunda sukari kutoka hewa chafu ikipitishwa katika bakteria, lakini haikufaulu ipasavyo.

Ni utafiti uliochapishwa katika jarida la Cell, ulisema watafiti katika Taasisi ya kisanyansi ya Weizmann ya nchini Israel, walitengeneza mchepuo wa walioita 'Escherichia Coli' (|E-coli) kula hewa ukaa, badala ya kutumia nishati mzito zaidi ya sukari na mafuta.

Walakini wa utafiti huo ni kwamba, licha ya kufaulu kuunda bakteria wanaotumia chakula hewa ukaa, badala ya nishati hizo za kawaida, waliishia kuzalisha hewa nyingi ya ukaa kuliko iliyotumiwa na bakteria kama nishati kujikimu. Ni pengo kubwa, katika kufanya tathmini ya utafiti huo na matumizi yake kisayansi, kabla hata ya kutafakari kama kuna uwezekano wa kutumia ugunduzi kuunda kitu, kibiashara.

Hata hivyo, watafiti hao na wengine wanatazamia kuwa utafiti umefungua njia ya kupatikana mifumo ya nishati katika siku za usoni, ambayo haitaongeza hewa chafu (carbon dioxide) angani, yaani hewa chafu inatumika zaidi kuliko inavyozalishwa.

> Ni ugunduzi ulioleta matumaini ya haraka, kuwa mpangilio huo wa kuunda bakteria, unaweza kusaidia kupambana na mabadiliko ya tabianchi, endapo kutakuwapo nyenzo za kuzalisha kwa wingi bakteria hizo bila ya madhara kwa mazingira au gharama kubwa kupita kiasi.

Itawezesha kuipunguza badala ya kuongezea katika uzalishaji kwa jumla, lakini ina maana kwamba vikwazo vilivyoainishwa katika utafiti tangulizi, vinapaswa vipatiwe ufumbuzi na mpangilio wa fikra ambao baadhi ya wachunguzi wa utafiti wanautilia shaka.

Ndipo inakuja hoja, itabidi ipatikane aina nyingine ya kiumbe ya kutumia hewa ukaa zaidi, kuliko inavyoizalisha.

Siyo rahisi kuona kiumbe kama hicho kiwe mnyambuliko wa aina mojawapo ya vilivyopo, kwani kimsingi vinahitaji nishati nzito na siyo gesi hiyo ya ukaa.

Wanasayansi tayari wanafahamu aina ya vitu vyenye uhai vinavyohitaji au vinatumia chakula cha hewa ukaa na vikiwepo au kuzalishwa kwa wingi, vitapunguza uharibifu wake katika mfumo wa maji au baharini.

Ni kundi la mimea, kwani dunia ina makundi mawili ya vitu hai. Wanaotengeneza chakula chao wenyewe kwa kutumia mahitaji ya msingi yanayopatikana katika hewa au udongo na wanaotumia viumbe au vitu vingine vinavyotokana na mada za msingi, mathalan maji, udongo na hewa.

Makundi ya viumbe hai yanayotumia maada za msingi, yaani mimea yanajitengenezea chakula, lakini yanahitaji nishati nzito zaidi hutumia viumbe wengine au nishati nzito halisi.

Mtu anapotumia dhana kinzani badala ya kutoa taarifa ya maendeleo ya sayansi, atajiuliza kwanini wanasayansi wanahangaika kutafuta 'vijidudu' au 'vijiluwiluwi' vya kutafuta hewa chafu - ukaa, wakati mimea inapandwa kirahisi?.

Popote penye athari bayana, si kivuli tu bali kurahisisha kupumua na kuwa nzuri zaidi, hasa kwa wanaokaa mijini au miji mikubwa.

Inazaa maana ya kuondoa sehemu kubwa ya hewa chafu iliyozagaa hewani na baharini. Jambo la msingi ni kuondoa majanga makubwa duniani, kwa mkakati wa kimataifa wa kusafisha maji ya bahari kwa mitambo maalum, kujenga mabwawa na kusambaza maji kwa mtawanyiko, kutumia chumvi iliyotolewa baharini kwa mbolea, kueneza mbegu za miti.

Jicho la kasoro katika utafiti huo, ni wanasayansi wote duniani wameelekeza hisia zao katika uzalishaji mwingi wa hewa ukaa.

Siyo rahisi kusema, kwanini hakuna mkutano wowote wa kimataifa wa masuala ya mazingira uliowahi kujadili suala la kuondoa majangwa kwa kusafisha maji na kuyasambaza, kwa mtawanyiko pamoja na mbegu za miti. Ingeundwa misitu badala ya majangwa.



# Magari yagongana na kuua watatu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATU watatu wamefariki dunia mkoani Mbeya kwenye ajali ya barabarani iliyohusisha magari mawili ya mizigo yaliyogongana uso kwa uso katika Kijiji cha Ibula, wilayani Rungwe.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Ulrich Matei, alisema jana kuwa ajali hiyo ilitokea juzi saa 4:00 asubuhi katika eneo lijulikanalo kwa jina la Kanyengele au Airport.

Kamanda Matei aliyataja magari yaliyohusika kwenye ajali hiyo kuwa ni gari lenye namba za usajili T.257 CZA aina ya Howo lenye tela namba T. 597 CRR mali ya Kampuni ya Camel Oil ya jijini Dar es Salaam na Canter yenye namba za usajili T.840 CLY mali ya kiwanda cha Maji cha Rungwe Spring Water.

Aliwataja waliofariki dunia kwenye ajali hiyo kuwa ni dereva wa gari la mafuta, Frank Sangumo, maarufu kama 'Chota' mkazi wa Morogoro na utingo wake aliyetambuliwa kwa jina la Silas pamoja na dereva wa Canter, Nelson Samson (35).

Matei alisema chanzo cha ajali hiyo ni gari la mafuta ambalo lilikuwa limepata hitilafu kwenye mfumo wa breki na tairi moja la nyuma likashika moto, hivyo kupoteza mwelekeo na kukutana uso kwa uso na gari la maji lililokuwa upande wake.

Alisema gari hilo la mafuta lilikuwa limebeba mafuta aina ya dizeli ikitokea Dar es Salaam kwenda nchi jirani ya Malawi na gari la maji ilikuwa inatokea Rungwe kwenda jijini Mbeya.

"Pamoja na vifo vya watu hao, pia umetokea uharibifu mkubwa wa magari yote mawili. Kilichotokea ni uzembe wa dereva wa gari la mafuta ambaye hakuchukua tahadhari ya kukagua mfumo wa breki za gari lake kabla ya kuanza kuteremka mlima," alisema Kamanda Matei.

Alisema miili ya marehemu imehifadhiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Rungwe Makandana kwa ajili ya kusubiri taratibu zingine ikiwamo kusafirisha na kuzika.

Aliwataka madereva wa magari makubwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa mifumo ya breki kabla ya kuanza kuteremka kwenye milima mirefu ili kuepuka madhara ya ajali hasa wanapoingia katika mkoa wa Mbeya ambao alisema una milima mingi.

Alisema kwa sasa Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wadau wengine wa usalama barabarani, wameandaa maeneo maalumu ya madereva kukagua magari yao kabla ya kuanza kuteremka milima hiyo mirefu.

Alisisitiza kuwa hata kama dereva ana uhakika na mifumo ya breki za gari lake, ni vyema akasimama kwenye maeneo hayo kwa ajili ya kuruhusu gari lipowe kwa kuwa magari makubwa yakitembea kwa muda mrefu breki huwa yanapata moto na kuwa katika hatari ya kufeli.



Diwani wa Kata ya Mwakibete, jijini Mbeya, Lucas Mwampiki (kushoto), akishirikiana na baadhi ya wajumbe wa Kamati za Shule za Mwakibete na Uhuru, kuhesabu fedha mbazo wananchi walichangishana juzi, kwa ajili ya kuajiri mlinzi wa kulinda mali za shule hizo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wachangishana kuimarisha ulinzi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wa Kata ya Mwakibete jijini Mbeya, wamekubaliana kuchangishana fedha kwa ajili ya kuwalipa walinzi waliowaajiri kulinda shule za msingi za Mwakibete na Uhuru ambazo zinakabiliana na tishio la wizi wa mali.

Walifikia makubaliano hayo juzi wakati wa kikao cha dharura cha wazazi baada ya kutokea wizi wa mali ikiwamo mashine ya kurudufu maandishi, zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 10.7 kwenye ofisi ya Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Uhuru.

Wananchi hao walisema waliamua kuajiri walinzi wawili kwa dharura na kuwalipa fedha walizochangishana wakati wanaendelea kusubiri kibali rasmi cha kuchangishana fedha kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa.

Diwani wa Kata hiyo, Lucas Mwampiki, alisema waliamua kufanya hivyo ili kunusuru mali zilizobaki na kwamba kinachowasikitisha ni kibali kuchelewa kutolewa. "Tumesubiri kibali kwa muda mrefu, lakini bado hakijapatikana na hatuwezi kuendelea kusubiri wakati mali zinaibwa ndio maana tumekubaliana kuchangishana na kuajiri walinzi maana shule hizi zipo eneo moja," alisema Mwampiki.

Alisema wananchi wake wako tayari kuchangia fedha lakini hawawezi kuanza kuchangisha kabla kibali hakijatolewa, hivyo akaiomba Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kuwahisha kibali hicho. Mwenyekiti wa Kamati ya Shule hiyo, Tito Nyondo, alisema kwa sasa walikubaliana watumie utaratibu wa kuchangishana kwa njia ya harambee ili watakapopata kibali waanze kuwachangisha wananchi kama ilivyokuwa zamani.

Alisema walituma barua ya kuomba kibali cha kuwachangisha wananchi fedha za kumlipa mlinzi tangu Juni, mwaka huu, lakini mpaka sasa bado hakijapatikana.

Nyondo alisema endapo kibali kingetolewa mapema pengine wizi uliotokea hivi karibuni kwenye shule hiyo usingetokea kwa kuwa wazazi wako tayari kuchangia lakini kilichokuwa kinachelewesha ni kibali hicho.

"Tumekubaliana tuajiri walinzi wawili ambao watakuwa wanalinda shule zote mbili na kwa sasa kwa kuwa hatuna kibali tunatumia harambee kukusanya fedha za kuwalipa lakini tutakapokipata kibali tutaanza kuwachangisha wananchi moja kwa moja," alisema Nyondo.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mwakibete, Lugano Mwamsojo, alisema kwa mujibu wa taratibu ni kosa kuwachangisha wazazi mchango wa aina yoyote bila kuwa na kibali cha serikali.

Alisema kutokana na utaratibu huo ndio maana walikuwa hawajaanza kuwachangisha wananchi mchango kwa ajili ya kuajili walinzi katika shule hiyo.

## Wadaiwa maji wapata ahueni

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA), imekuja na mkakati mpya wa ukusanyaji wa mapato kwa kuwaondolea faini wateja wote waliositishiwa huduma kwa sababu za kutokulipa ankara kwa muda mrefu na kutakiwa kulipa madeni kwa awamu.

Tangazo lililotolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka hiyo, Mhandisi Ndele Mengo, linawataka wananchi wote waliositishiwa huduma kulipa nusu ya madeni yao ili warejeshewe huduma bila kutozwa faini na kiasi kitakachobaki watakuwa wanalipa kwa awamu.

Tangazo hilo linaeleza kuwa ili kuhakikisha wateja wanalipa deni litakalobakia, watatakiwa kuingia mkataba maalumu na Mbeya-WSSA utakaokuwa na masharti nafuu kwa ajili ya kuwarahisishia kulipa bila usumbufu.

Kwa mujibu wa tangazo hilo, utaratibu huo ulianza kutumika Desemba Mosi, mwaka huu na mwisho wa kuutumia itakuwa Desemba 30.

"Ofa hii inalenga kuwafanya wateja wetu wasivuke mwaka wakiwa na madeni ndiyo maana tuna kauli mbiu yetu inayosema 'Mwaka Mpya Bila Madeni ya Maji Inawezekana'. Hii ni ofa ambayo wateja wanatakiwa waitumie ipasavyo," alisema Mengo.

Mamlaka hiyo inadai madeni yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni nne na wadaiwa wakubwa ni taasisi za serikali, vikiwamo vyombo vya dola, zinazodaiwa zaidi ya Sh. bilioni 1.5.

Hivi karibuni, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alizitaka taasisi hizo kulipa madeni hayo kabla ya Desemba 15 na zisipotekeleza zisitishiwe huduma.



# Waapa kuwachongea viongozi wabovu

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

WAKAZI wa kijiji cha Haneti, Chamwino mkoani Dodoma wamesema hawatakuwa tayari kufanya kazi na viongozi wazembe na wanaokiuka maadili ya utumishi wa umma.

Kauli hiyo ilitolewa mbele ya Sekretarieti ya Maadili kwa Viongozi wa Umma kutoka Ofisi ya Rais baada ya kufika kijijini hapo na kutoa elimu kuhusiana na misingi ya viongozi wanavyotakiwa kufanya kazi na wananchi.

Ronald Sigila, akizungumza kwa niaba ya wanakijiji hao, alisema mafunzo yaliyotolewa wamepata uelewa jinsi ya kutofanya kazi na viongozi wasio na maadili ya utumishi wa umma.

Pia alisema wamepata elimu ambayo itasaidia katika kuzuia hata yale maovu ambayo yamekuwa yakifanywa kwa wananchi walikuwa hawatambui wakifikiri ni haki yao kufanywa na viongozi hao kwa upande wao.

"Tumekuwa tunaonewa na tunaona kama ni halali kwa viongozi wanapokiuka ni haki yao, lakini kwa elimu hii tunaihakikishia serikali yetu tukufu hatutakubali kuwa na viongozi wa jinsi hiyo," alisema.

Naye Arafa Digidigi alisema mafunzo hayo yamewaongezea na kuwaamsha ufahamu namna ya kuwasilisha malalamiko ya viongozi ambao si waadilifu tofauti na awali ambapo walikuwa hawafahamu sehemu husika ya kupeleka malalamiko yao.

"Tumefurahi sana kamati hii ya maadili kuja kijijini kwetu kutupa elimu juu ya maaadili ya viongozi wa umma. Tumeelewa sasa hatua za kuchukua dhidi ya viongozi wasio waadilifu na viongozi hawa mwisho wao umefika. Tunaahidi kupeleka malalamiko yetu kamati ya maadili ili watusaidie," alisema wananchi.

Wananchi hao walisema wamejisikia furaha kupata elimu hiyo kwa kuwa wamekuwa wakionewa na baadhi ya viongozi wa kijiji kwa kutotambua maadili ya utumishi wa umma wanavyotakiwa kuwahudumia wananchi.

Kupitia elimu hiyo, walisema watakuwa na uwezo wa kufahamu haki zao za kimsingi na majukumu ya viongozi wa umma kwa wananchi wake.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Damas Paskal, alisema elimu hiyo iliyotolewa kwa wananchi itawanufaisha na watakuwa mabalozi kwa wengine juu ya maadili ya watumishi wa umma.

Alisema wakiwa viongozi, wamejifunza mambo mengi ikiwamo kufanya kazi kwa uadilifu na kwa kufuata maadili ya viongozi wa umma hasa kwa kutokujali maslahi yao binafsi.

Awali, akizungumza na wakazi wa Haneti, Ofisa wa Sekretarieti ya Maadili ya Watumishi wa Umma, Mariam Nguzo, alisema kuelekea kilele cha maadhimisho ya Siku ya Maadili, wameamua kutoa elimu hiyo kwa jamii ili kuhakikisha maadili ya viongozi yanafuatwa.

Pia alisema mafunzo haya yatawasaidia wananchi na jamii kwa ujumla kufahamu kiongozi bora ambaye ataweza kuwasaidia kutatua changamoto walizo nazo na kuwaletea maendeleo katika maeneo yao.



Mkuu wa Wilaya ya Kondoa, Sezeria Makota (kushoto), akikabidhi pedi kwa ajili ya wanafunzi wa kike wa Shule ya Msingi Iboni, zilizotolewa na Mratibu wa Mradi wa Umati, Rechel Stephen, katika Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Watu wenye Ulemavu yaliyofanyika kimkoa wilayani Kondoa, mkoani Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Umeme Tanesco kunufaisha nchi jirani

**Na Renatha,** DODOMA

SHIRIKA la Umeme Tanzania (Tanesco) limesema maboresho yanayofanywa kwenye gridi ya taifa ya kuunganisha mtandao wa umeme nchi jirani za Kenya, Burundi na Zambia, yataliwezesha kuwa kiungo muhimu cha biashara ya kimataifa ya kuuza na kununua umeme kwa nchi za kaskazini na kusini mwa Bara la Afrika.

Mwenyekiti wa Bodi ya Tanesco, Mhandisi Alexander Kyaruzi, alisema hayo, juzi, wakati akikagua ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme cha Zuzu kilichoko Dodoma katika mradi wa njia ya umeme ya msongo yenye kilovolti 4,000.

Kyaruzi alisema kituo hicho kinatarajia kukamilika mapema mwakani na kimeongezewa uwezo wa uzalishaji megawati 748 na maboresho hayo yamefanywa pia kwenye vituo vilivyoko katika mradi huo ili kusaidia kukidhi mahitaji ya umeme ndani na nje ya nchi.

Alisema biashara hiyo itakuwa imara kwa sababu kuna vyanzo vingi vya umeme nchini kwa mfano kutoka kwenye gesi na kwingineko ambako umeme unaozalishwa wanaamini utasaidia kwa kiasi kikubwa utoaji umeme ambao utakuwa na mchango mkubwa katika ujenzi wa viwanda.

"Nchi yetu itakuwa na viwanda vingi ambavyo vitajengwa ndio maana tumeviongezea uwezo vituo vya kuzalisha umeme ili uweze kujitosheleza katika viwanda vilivyopo na vile ambavyo vinatarajiwa kujengwa," alisema Kyaruzi.

Aidha, alisema kuwa umeme ni muhimu kukamilika katika muda uliopangwa kutokana na kwamba taifa hivi sasa linaelekea katika uchumi wa kati wa viwanda, hivyo ni lazima viwanda viwe na umeme wa kutosha ili vifanye kazi ipasavyo na kwa uhakika.

Mratibu wa mradi huo, Mhandisi Peter Kigadye, alisema lengo la kujiunga na nchi jirani katika gridi hiyo ni kutokana na kutaka kuendeleza biashara ya umeme toka hapa nchini na nchi jirani ambayo italeta manufaa makubwa kwa taifa.

Mhandisi Kigadye alisema moja ya faida ambazo zitapatikana kupitia muunganiko huo pamoja na Tanzania ikikosa umeme itanunua kwa jirani lakini wakikosa Tanzania itawauzia umeme kutoka nchini na kuliingizia taifa kipato.

"Huu mpango ni mzuri sana utaliwezesha Shirika kupanua wigo wa kufanya kazi zake hapa nchini na nje ya nchi," alisema Kigadye.

Aidha, alisema wataendelea na mfumo wa upanuzi wa vituo hivyo lengo ikiwa ni kutaka kuvipa uwezo wa kufanya kazi kwa kiasi kikubwa na kuongeza kuwa mfumo huo utaenda katika mikoa mbalimbali nchini ambayo iko ndani ya mradi huo.

Akitolea ufafanuzi juu ya ujenzi wa vituo hivyo, alisema katika awamu hii wanatarajia kutumia Sh. milioni 120 katika mikoa Dodoma, Singida, Iringa na Shinyanga ambazo zitatumika katika kufanya maboresho ya vituo hivyo ambayo yamebainisha awali.

# Takukuru yambana mbavu mkandarasi

**Na Renatha Msungu,** CHEMBA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana Rushwa (Takukuru) mkoani Dodoma imetoa siku 10 kwa kampuni ya Juan inayotekeleza mradi wa maji wa Kelema Kuu ulioanza toka 2014 kuhakikisha unakamilika ili kusaidia wakazi wa eneo hilo kupata huduma ya majisafi na salama.

Hivi sasa wakazi wa eneo hilo wanatumia maji ya bwawa ambayo si salama huku wengine wakifuata kijiji cha pili ambacho ni Kelema Balai umbali wa maili mbili.

Awali mradi huo ulikamilika 2014, lakini ulifanya kazi kwa wiki moja na mabomba yake kupasuka kutokana na kuzidiwa uwezo kutokana na msukumo mkubwa wa maji kutoka katika kisima.

Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Dodoma, Sostheness Kibwengo, alisema juzi kuwa kampuni hiyo imelazimika kununua mabomba yenye thamani ya Sh. milioni 51 ili kufidia gharama ya mradi huo ambazo ni Sh. milioni 223.

Kibwengo alisema wametoa siku hizo kwa mkandarasi huyo ili kuhakikishha wakazi wa eneo hilo wanapata majisafi na salama.

"Tumetoa siku hizo kwa kampuni hiyo ili wakamilishe kwa sababu mvua zikianza watapata visingizio," alisema Kibwengo.

Alisema baada ya kufanya uchunguzi wao, walibaini kwamba mabomba yaliyonunuliwa na kutumika katika mradi huo ni ya ukubwa wa PN 6 badala ya 12.5 kama zilivyoizinishwa katika mkataba wa kutekeleza mradi huo. Alisema baada ya siku hizo walizotoa hakutakuwa na msamaha wowote kwa kampuni hiyo kwa sababu ni uzembe na udanganyifu uliofanywa na mkandarasi huyo.

Alisema kinachotakiwa ni wao kufanya kazi haraka iwezekanavyo hasa ukizingatia mitaro tayari imechimbwa.

Naye Mhandisi wa Wakala wa Maji Vijijini (Ruwasa) wilayani Chemba, Robert Mganga, alisema kazi iliobakia ni nyepesi sana hivyo wiki moja inatosha kukamilisha kufanya utandikaji huo wa mabomba.

"Hakuna kazi ngumu hapa sema hii kampuni inaleta uzembe, tuko nao pamoja hivi sasa kuhakikisha wanakamilisha," alisema Mganga.





# Mil. 300/- zatengwa kukabili tabianchi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIKA juhudi za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, serikali imetenga zaidi ya Sh. milioni 300 kwa ajili ya kulinusuru eneo la Micheweni Pemba ambalo limeharibiwa na mmomonyoko wa ardhi unaotokana na mawimbi ya bahari.

Sehemu hiyo imeathirika na mabadiliko ya tabianchi na kusababishia mmomonyoko mkubwa wa ardhi na sehemu ya ardhi kuzama baharini.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mohamed Aboud, wakati akijibu swali la mwakilishi wa Jimbo la Chakechake Suleiman Sarhani, aliyetaka kujua hatua zinazochukuliwa kuyanusuru baadhi ya maeneo Pemba ambayo yamekumbwa na mmomonyoko wa ardhi unaotokana na mabadiliko ya tabianchi.

Aboud alisema yapo maeneo mengi katika kisiwa cha Pemba na Unguja yameathirika na mabadiliko ya tabianchi ikiwamo maji ya bahari kuvamia maeneo ya makazi ya wananchi.

Alisema tatizo hilo limewafanya baadhi ya wananchi wanaoishi pembezoni mwa bahari kuyakimbia makazi hayo ili kuepuka kufunikwa na maji ya chumvi.

Hata hivyo alisema juhudi zimeanza kuchukuliwa kukabiliana na athari hizo ambapo katika wilaya ya Micheweni Pemba, fedha zimetengwa kwa ajili ya kudhibiti tishio hilo.

"Eneo la Micheweni tayari tumelitengea Sh. milioni 300 kwa ajili ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na mmomonyoko wa ardhi, unaotokana na mawimbi ya bahari,"aliliambia baraza.

Aidha, alisema tayari yapo mashirika ya kimataifa yameonyesha nia ya kusaidia tatizo la mabadiliko ya tabianchi na mmomonyoko wa ardhi kwa ajili ya kunusuru wananchi na mazingira.

Alilitaja Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (UNEP) ambalo mkurugenzi wake alipata nafasi ya kutembelea Zanzibar na kukagua baadhi ya maeneo yaliyoathirika na mabadilikio ya tabianchi.

Baadhi ya sehemu hizo ni kisiwa kidogo Panza pamoja na Mtambwe Mkuu ambavyo baadhi ya maeneo yake wananchi wameanza kuyahama.

Aidha, sehemu za vijiji vya Jambiani, Paje pamoja na Bwejuu vipo katika tishio la kuathirika na mabadiliko ya tabianchi kiasi ya wananchi kuhama maeneo yaliopo karibu na fukwe na kukimbilia kwenye miinuko.

# Mwakilishi ataka ukumbi ufungiwe

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWAKILISHI wa Jimbo la Paje, Jaku Hashim Aboub, ameiomba serikali kuufungia ukumbi wa starehe uliopo Dunga (jina tunalo).

Jaku aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akiuliza swali la nyongeza na kueleza kuwa ukumbi huo ni kichocheo cha kuongezeka kwa vitendo vya udhalilishaji watoto.

Ukumbi wa starehe huo unapiga muziki nyakati za usiku Ijumaa hadi Jumapili upo katika kambi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania huko Dunga nje ya Mji wa Zanzibar Mkoa wa Kusini Unguja.

"Kwanini usifungwe kwa sababu baada ya vitendo vya udhalilishaji Zanzibar kupungua vimekua vikiongezeka, kwa mtazamo wangu ukumbi huo unasababisha kuongezeka kwa vitendo hivyo kutokana na mambo yanayofanyika huko kuendeleza udhalilishaji," alisema Jaku.

Akijibu suali hilo, Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Moudline Castico, alisema kuwa hajawahi kufika katika ukumbi huo na wala hajui mambo yanayotendeka. "Ni vyema Jaku tukaongozana kwenda huko kuangalia hali ilivyo ili kuweza kutafuta njia bora za kuweza kutatua tatizo la udhalilishaji," alisema Castico.

Alieleza kuwa Wizara itashirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ambayo ndiyo yenye mamlaka ya maeneo hayo kuangalia uwezekano wa kulifungia eneo hilo kisheria.

Awali, akijibu swali la msingi la mwakilishi huyo, Waziri Castico, alisema kuwa matukio ya udhalilishaji yaliyoripotiwa kwa mwaka 2017/2018 ni 9 1,147 ukiliganishwa na matukio 2,447 yaliyoripotiwa mwaka 2016/2017.

Alieleza kuwa jumla ya matukio 178 pekee yameripotiwa kutoka Mkoa wa Kusini Unguja kwa mwaka 2017/2018 ukilinganisha na matukio 490 yaliyoripotiwa Mkoa wa Mjini Magharib Unguja kwa mwaka huo.

Alisema kuwa hali inaonyesha kupungua kwa matukio hayo kutokana na kuongezeka kwa elimu ya kujikinga na hatua nyingine zinazochukuliwa na serikali.

"Mheshimiwa Spika, wizara haiwezi kusema kwamba matendo haya yanaongezeka katika maeneo ya Dunga, Tunguu, Kiboje, Ungujaukuu kutokana na ukweli kuwa hakuna utafiti uliofanywa kuthibitisha haya," alisema waziri huyo.

Aidha, alisema kuwa kutokana na takwimu alizozitaja mkoa unaongoza kwa matukio hayo ni wa Mjini Magharib Unguja na si maeneo hayo yaliopo Mkoa wa Kusini Unguja.

Hata hivyo, alisema serikali inaendelea na juhudi zake za kuelimisha jamii kujikinga na matendo hayo yasitokee na kuripoti haraka yanapotekea matukio hayo.



Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma (kulia), akijadiliana jambo na Waziri wa Ardhi, Maji na Nishati, Salama Aboud Talib, nje ya ukumbi wa baraza hilo, Mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Zanzibar kuanza uvuvi bahari kuu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar, imeahidi kujikita katika uwekezaji wa uvuvi wa bahari kuu pamoja na kujenga viwanda vya kuchakata mazao (kusarifu), ya baharini ili yalete tija katika mabadiliko ya uchumi wa bahari. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda, Hassan Khamis Hafidh, wakati akijibu swali la mwakilishi wa Jimbo la Tumbe Omar Seif Abeid, aliyetaka kujua serikali imejipanga vipi katika kuwawezesha wavuvi kuvua bahari kuu.

Hafidh alizitaja juhudi zilizoanza kuchukuliwa na serikali ikiwamo kununua boti ya uvuvi ya Sehewa 2 ambayo itakuwa inavua kwenye maji ya bahari kuu.

Alisema uvuvi wa bahari kuu umechelewa kuanza kufanyiwa kazi na kutoa huduma kufuatia kukosekana kwa vyombo vya uvuvi vyenye uwezo wa kuyafikia maeneo hayo.

"Mikakati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuhakikisha wavuvi wanavua katika maeneo ya bahari kuu kwa ajili ya kupata mavuno mazuri ya samaki,"alisema.

Alieleza kuwa wapo aina ya samaki kama jodari ndiyo wanaopatikana kwa wingi katika bahari kuu ambao bado hawajavuliwa kwa ajili ya kupata tija kiuchumi na maendeleo. "Jodari wanapatikana katika maeneo ya bahari kuu ingawa bado hawajavuliwa kwa sababu wavuvi wetu hawayafikii maeneo hayo," alisema.

Aidha, alieleza kuwa juhudi zimeanza za kuwahamasisha wawekezaji wa ndani na nje kujenga viwanda vya kusarifu mazao ya baharini ikiwamo mwani. Alisema wananchi wengi wamehamasika kulima kilimo cha mazao bahari, lakini hadi sasa bei ya mwani ni changamoto kwani ni ndogo kiasi cha ya kuwavunja moyo wakulima wa kilimo hicho.

"Yapo matumaini makubwa ya kujengwa kwa viwanda vya kusarifu mazao ya baharini ikiwamo mwani hatua ambayo italeta mabadiliko makubwa ya maendeleo ya kilimo hicho na mavuna ya maliasili zinazotokana na bahari," alisema.

# Watakiwa mchakato ujenzi kiwanda asali

**Na Tiganya Vincent**

MADIWANI na viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge mkoani Tabora, wametakiwa kuachana na mpango waliokusudia wa kutenga kituo cha ukusanyaji wa asali bali wafikirie wazo la ujenzi wa kiwanda cha kusindika asali ili kuongeza thamani ya asali.

Ushauri huo ulitolewa wilayani Sikonge na Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani.

Alisema utaratibu wa ujenzi wa kiwanda utawasaidia wafugaji wa nyuki kupata faida kubwa na kuwa na bidhaa ambazo zinajulikana asili yake zinazalishwa na kiwanda cha Sikonge (Made in Sikonge).

Mwanri alisema kitendo cha kuruhusu Sikonge kugeuka kuwa sehemu ya kukusanya asali ambayo haijasindikwa kutasababisha watu kutoka nje kuingia katika eneo la kukusanya asali yote na kuwaacha wafugaji wakiwa na faida kidogo huko ikienda kunufaisha maeneo mengine.

"Naona Sikonge hatuelewani mimi nazungumzia uanzishaji mwa kiwanda cha kusindika asali na kuiweka kwenye vifungashio kama vile chupa ambazo zina nembo ya Sikonge, nyie mnafikiria kuwa na 'collection centre' ambapo asali itauzwa kabla ya kuongezewa thamani na kwenda kunufaisha watu wa sehemu nyingine na kuwacha watu wakiwa maskini," alisema.

Alisema uanzishwaji wa kiwanda utasaidia kuwapa wafugaji na wakazi wa eneo hilo kupata mtaji na teknolojia ya kisasa ya usindikaji asali na ajira na kuboresha maisha ya familia katika eneo la Sikonge na halmashauri itapata mapato.



Ofisa Tathmini na Ufuatiliaji kutoka Shirika la Kivulini, Godfley Paschal (kushoto), akitoa mada kwenye kikao cha wadau wa elimu Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga jana, ili kujadili chanzo cha mimba za wanafunzi na kuzitafutia ufumbuzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# SMZ yafagilia Tehama huduma za umma

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imeanza kuvuna matunda ya matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) katika shughuli za umma, kwa sababu idara za serikali zinatumia mkonga wa taifa katika kutoa huduma kwa wananchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mkonga wa Mawasiliano Zanzibar, Mhandisi Shukuru Awadhi Suleiman, ndiye aliyebainisha hayo jana katika ufafanuzi wa ziada kwamba Tehama imeleta mapinduzi katika utoaji wa huduma za umma kwa kupunguza gharama za utoaji huduma, kuokoa muda, kuboresha udhibiti na kwa ujumla kuingiza ubora wa kileo katika utoaji huduma kwa wananchi.

Mhandisi Suleiman alisema wananchi wanafurahia huduma kwa vile si tu kwamba zinatolewa kwa daraja la juu, bali kwamba matumizi ya

Tehama imewapunguzia wananchi mahangaiko, safari za kufuata huduma mbali na makwao au kusubiri muda mrefu mahali huduma zinakotolewa.

Kuhusu kupunguza gharama za utoaji huduma kwa upande wa serikali na wananchi wakati ule ule, Mhandisi Suleiman ametumia mfano wa huduma za hospitali kwa kueleza kwamba vipimo vya kileo vikifanyika katika hospitali ya wilaya, vinatumwa kwa mtandao kwa Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja, Mjini Zanzibar na majibu yanarudishwa wilayani pasipo mgonjwa au mtumishi wa serikali au wote wawili kulazimika kusafiri kutoka wilayani mwao kwenda mjini Zanzibar.

Ameeleza kuwa vituo vya afya 24 vya Unguja na Pemba vimeunganishwa kwenye serikali mtandao, na kuwapunguzia wananchi adha na gharama za kusafiri.

Alisema wananchi wenyewe wanashuhudia urahisi, wepesi na ufanisi katika utoaji wa huduma za afya, kodi, elimu na huduma za


vyeti vya kuzaliwa.

"Wananchi sasa hawalazimiki tena kutoka wilayani mwao kwenda makao makuu Mjini

Zanzibar kufuata huduma. Mfumo huu wa 'Serikali Mtandao' umepunguza sana gharama, umeboresha udhibiti, unaokoa muda na umekuza mapato ya serikali."

# Umuonapo mtoto huyu toa taarifa

**Na Mwandishi Wetu**



MTOTO Zainabu Said (13), anatafutwa na ndugu zake baada ya kutoweka nyumbani kwao Sinza Palestina jijini Dar es Salaam na kwenda kusikojulikana.

Dada yake, Upendo Mapunda, amesema, mtoto huyo alitoweka tangu Desemba mosi mwaka huu, majira ya saa kumi na mbili jioni na kuelekea sehemu ambayo huwa anakwenda kuchota maji.

"Tangu wakati huo hakuonekana tena na tumetoa taarifa kituo cha polisi na kufungua jalada namba KYN/RB/6573/2019, tunaomba pia wasamaria wema watakaomwona watusaidie kutoa taarifa," amesema Upendo.

Upendo amesema, wasamaria wema watakaomuona watoe taarifa kituo chochote cha polisi na pia wawasiliane naye kwa simu namba **0716-261548** au **0658-532525.**

# Kasi matukio udhalilishaji

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

JUMLA ya kesi 93 za udhalilishaji kwa Wilaya ya Wete zimeripotiwa katika kituo cha Polisi Wete kuanzia Januari hadi Septemba mwaka huu.

Kesi hizo ni pamoja na kubaka 34, kutorosha 37, kunajisi (kulawiti)11, shambulio la aibu tisa na kuingilia kinyume na maumbile mbili .

Akizungumza katika mkutano wa kuwasilisha ripoti ya miezi mitatu, ulioandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Mratibu wa Dawati la kijinsia Mkoa wa Kaskazini Pemba, Fakih Mohamed Yussuf, alisema kesi hizo ni kwa Wilaya ya Wete pekee.

Alisema kesi 21 kati ya hizo zimepelekwa mahakamani, kesi mbili zimepata hatia, kesi moja na kesi 22 zimefungwa polisi kutokana na jamii kukataa kutoa ushahidi.

Alieleza katika jitihada yao ya kupambana na vitendo vya udhalilishaji, wanaendelea kutoa elimu katika jamii, na kuwa wameshazifikia madrasa 38 za Wilaya ya Wete na kuwafikia wanafunzi 5700.

"Tumezifikia shehia 27 na tunaendelea kutoa elimu hii, ili wananchi waelewe nini udhalilishaji na athari zake, kwa sababu kila uchao vitendo hivi vinaongezeka," alisema mwananchi huyo.

Msaidizi Mkurugenzi wa Baraza la Mji Wete kwa upande wa elimu, Ramla Omar Saleh, alisema vitendo vya udhalilishaji kwa watoto vinaongezeka siku hadi siku kutokana na wazazi kuficha taarifa za matukio hayo.

Ofisa Wanawake na Watoto Wilaya ya Wete, Siti Suleiman Juma, alisema ipo haja ya kurekebishwa sheria, ili watoto wa kike wenye kumri kuanzia miaka 15 nao wapewe adhabu, jambo ambalo litawatia hofu ya kufanya vitendo vichafu.

Ofisa Ufuatiliaji na Tathmini kutoka TAMWA, Mohamed Khatib Mohamed, alisema lengo la mkutano huo ni mwendelezo wa kupambana na udhalilishaji kwa wanawake na watoto, hivyo kila mmoja kwa nafasi yake awajibike katika kuhakikisha matendo hayo yanatokomezwa katika jamii.

Mratibu wa TAMWA Pemba, Fat-hiya Mussa Said, alisema ushirikiano unahitajika katika kuhakikisha wanapambana na vitendo hivyo kwa hali moja ama nyengine, ili watoto waishi kwa amani katika jamii.

"Kila mzazi ana hofu saa zote kwa watoto wetu, watoto hawaishi tena kwa amani, hakuna tena kuaminiana, hujui shuleni wala madrasa, kwa kweli ni mtihani mzito watoto wanateketea," alisema.

## Marekani yasaini muswada kupinga vikwazo

**WASHINGTON, Marekani**

BUNGE la Marekani limepitisha muswada ili kupambana na vile wanavyovisema kuwa ni vikwazo visivyo na mantiki, mateso na unyanyasaji kwa waislamu wa jamii ya Uighur nchini China.

Imelenga vile vikwazo vinavyowalenga wanachama wa serikali ya China na kumtaja kiongozi wa chama cha kikomunisti katika Mkoa wa Xinjiang, Chen Quanguo.

Lakini muswada huo bado unahitaji idhini kutoka kwa seneta na Rais Donald Trump.

Kwa upande wa China, Waziri wa Mambo ya Nje wa nchi hiyo ameoneshwa kutofurahishwa na kusema hatua hiyo ni ya uovu.

Muswada wa haki za kibinadamu za Uighur wa mwaka 2019 ulipitishwa bungeni na wabunge 407.

Kupitishwa kwake kunakuja baada ya Rais Trump kutia saini sheria inayounga mkono maandamano ya demokrasia mjini Hong Kong pia kusababisha ukandamizaji kutoka kwa China.

Thomas Massie kutoka chama cha Republican kutoka Kentucky, alipiga kura kupinga muswada huo wa Uighur, vilevile hakuupigia kura muswada wa Hong Kong.

Lengo kuu la muswada huo ni kuweka wazi unyanyasaji wa haki za binadamu zijulikazo duniani kote, ikiwamo kufungwa kwa waislamu milioni moja wa Uighur.

Na pia unaushutumu China kwa kuwabagua waislamu wa jamii ya Uighur katika mifumo yao kwa kuwanyima haki mbali mbali za kiraia na kisiasa, ikiwamo haki za kujieleza, dini, uhuru wa kuandamana na mashtaka ya haki.

Uangalizi wa wote kutumia teknolojiia za kisasa, ikiwamo ukusanyaji wa sampuli za vinasaba kutoka kwa watoto.

Muswada wa Uighur unalenga maofisa kutoka China ambao wanadhaniwa kuhusika na ukiukwaji wa haki za kibinaadamu katika mkoa wa Xinjiang.

Vievile unamtaja kiongozi wa chama cha kikomunisti cha Xinjiang, Chen Quanguo, ambaye inasemekana kuwa mbunifu wa kambi hizo.

Muswada huo unamtaka Rais Trump kupinga unyanyasaji wa waislam wa Uighur, China kufunga kambi zote haraka na kuhakikisha haki inatendeka.

BBC

# Sita wafariki kwa kusombwa maporomoko ya matope

**KAMPALA, Uganda**

WATU sita wamefariki na watu wengine zaidi ya 30 wanahofiwa kufa baada ya makazi yao kusombwa na maporomoko ya matope katika Wilaya ya Bududa, Mashariki mwa Uganda.

Karibu kila mwaka, watu wengi hupoteza maisha baada ya makazi yao kusombwa na maporomoko ya matope katika wilaya ya Bududa, Mashariki mwa Uganda.

Watu wapatao 50 bado hawajulikani walipo baada ya mafuriko hayo kutokea.

Kiongozi wa juu wa eneo hilo ameviambia vyombo vya habari kuwa watu kadhaa bado wamefukiwa na mwili mmoja pekee umepatikana mpaka sasa.

Hata hivyo, Kamishna kutoka idara ya kukabiliana na majanga, Martin Owur, amenukuliwa akisema miili mitatu imepatikana Bududa na mingie mitatu katika wilaya ya jirani Sironko, huku watu 47 wakiwa hawajulikani walipo na nyumba 38 zikiwa zimeharibiwa.

Barabara nyingi za Bududa zimefurika maji, hali inayofanya kazi ya uokoaji kuwa gumu. Maporomoko ya matope yalifuatiwa na mvua kubwa iliyonyesha mfululizo kwa saa tano.

Serikali ya Uganda bado inafanya juhudi ya kuwahamisha watu 140 katika vijiji vipya.

Mwaka jana, watu 51 walipoteza maisha na zaidi ya watu 850 walikosa makazi baada ya maporomoko hayo kukumba eneo hilohilo.

Mvua kubwa isiyo ya kawaida katika eneo la Afrika Mashariki iliwaua watu zaidi ya 200 na zaidi ya watu milioni moja kukosa mahali pa kuishi.

Nchini Kenya, zaidi ya watu 130 wamepoteza maisha kutokana na mafuriko yaliyotokea tangu Oktoba.Watabiri wa hali ya hewa wameonya kuwapo kwa mvua kubwa mpaka mwishoni mwa mwezi Disemba.

***BBC***



Mvua zinazoendelea kunyesha nchini Kenya zimeleta usumbufu kwa wakazi hususani wanaotumia vyombo vya usafiri. **PICHA AFP**

## WHO: Ugonjwa wa malaria bado tishio Afrika

**DW, Afrika**

SHIRIKA la Afya la Umoja wa Mataifa (WHO) limesema homa ya Malaria imeendelea kuathiri maisha ya mamilioni ya watu kila mwaka na kuwauwa zaidi ya watu 400,000 wengi wao ni watoto barani Afrika.

Fedha za kugharamia mapambano dhidi ya malaria, maradhi yanayouwa mtoto mmoja kila dakika mbili, zimekwisha, linaonya WHO.

Limesema kwa kuwa mbu ndio chanzo cha kuenea maradhi hayo kuna uwezekano nusu ya idadi ya wakazi duniani wakikabiliwa na hatari ya kushikwa na maradhi hayo.

WHO limeyatolea wito mataifa fadhili na serikali za nchi zinazoathirika na maradhi hayo wazifufue juhudi za kupambana na Malaria.

Daktari wa ugonjwa wa Malaria, Pedro Alonso alieleza kuwa ulimwengu umedhihirisha maendeleo yanawezekana.

Alonso alitoa mifano ya nchi ambako kadhia za Malaria zimepungua sawa na ilivyopungua idadi ya vifo tangu mwaka 2010.

Alisema matukio ya watu wanaoshikwa na malaria yamepungua kutoka watu milioni 239 na kufikia watu milioni 214 mwaka 2015 na vifo pia vimepungua kutoka watu 607 000 hadi watu laki tano mwaka 2013.

Aliema matukio ya walioshikwa na Malaria nayo yamepungua kidogo tu mwaka 2018 kutoka watu milioni 231 mwaka 2017 na kufikia watu 228, na watu 416 000 waliokufa mwaka 2017 wakilinganishwa na watu 405.000 waliokufa mwaka jana.

Ripoti ya shirika la Afya la Umoja wa mataifa WHO inasema wanawake wajawazito na watoto barani Afrika wanaendelea kuvumilia kishindo cha maradhi ya malaria.

Imeeleza kuwa Wanawake wajawazito wanaokadiriwa kufikia milioni 11 wanaoishi katika eneo la Afrika Kusini mwa jangwa la Sahara-kiwango ambacho ni sawa na asilimia 29 ya wanawake wote wajawazito wa kanda hiyo wameshikwa na malaria mwaka 2018, na kusababisha watoto 900,000 kuzaliwa na uzito mdogo.

Ripoti hiyo pia imeeleza kuwa zaidi ya theluthi ya vijana wanaoishi katika kanda ya Afrika Kusini mwa jangwa la Sahara hawakuwa wakilala kwenye kitanda cha chandaruwa mwaka 2018.

Ushirika katika juhudi za kupiga vita malaria umesema ripoti ya WHO inaonyesha juhudi jumla na uwekezaji ni muhimu sana katika kuendeleza maendeleo yaliyofikiwa hadi wakati huu . Ushirika huo umezitolea wito serikali zisichzoke.

***DW***

# Bashiru aanika mbinu ushindi CCM Pemba

**Na Waandishi Wetu, PEMBA**

KATIBU Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Bashiru Ali, amewataka wanachama wa chama hicho Mkoa wa Kaskazini Pemba kushirikiana kukijenga, ili kipate ushindi katika uchaguzi mkuu wa mwakani.

Dk. Bashiru alitoa rai hiyo juzi kwenye Ukumbi wa Baraza la Wawakilishi Wete alipozungumza na viongozi na wanachama wa CCM mkoa huo.

Alisema kazi kubwa inayowakabili viongozi na wanachama CCM ni kuhakikisha wanakuwa kitu kimoja katika kutekeleza majukumu yao kwa kuingiza wanachama wapya, akiamini ni mbinu muhimu ya kukifanya chama hicho kuendelea kukaa madarakani.

Alisema endapo wana CCM wataanza kupotezeana muda na kusema 'vijimanenomaneno' vya kugawana vyeo, madhara makubwa yatatokea ndani ya chama.

"Sisi wana CCM hatuwezi kupoteza muda na kubishana na watu ambao hawana heshima na muda, kwa sasa wana CCM tumeamua kuwaunganisha Watanzania wote bila ya kubagua wanakotoka," alisema.

"Misingi ya umoja katika chama ni vikao, hivyo ninawaomba viongozi na wanachama wenzangu kukaa pamoja katika vikao vyenu kila baada ya muda na tuwe na siri katika kupitisha uamuzi wetu.

"Sitokuwa tayari kutumbuliwa mimi, kabla ya kufanyiwa mimi hivyo, kwanza nitawajibisha wale wote ambao hawako tayari kufuata maelekezo ya kamati kuu."

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kaskazini Pemba, Mberwa Hamad Mberwa, alimhakikishia Dk. Bashiru kuwa CCM itashinda kwa kishindo katika uchaguzi ujao kutokana na ushirikiano mkubwa wa wanachama wao.

Katika ziara yake hiyo kisiwani Pemba, Dk. Bashiru pia aliwaomba wananchi kuthamini mabadiliko ya kimaendeleo ya kiuchumi na miundombinu ambayo yameletwa na serikali zinazoongozwa na chama hicho.

Alisema ziara yake kisiwani Pemba imelenga kufikisha salamu za ushindi wa chama chao katika uchaguzi wa serikali za mitaa Tanzania Bara.

Alisema CCM kwa upande wa Zanzibar imeimarika na mabadiliko makubwa yamejitokeza katika uongozi wa Rais Ali Mohamed Shein, akieleza kuwa kuna haja wanachama kuomba chama kipate mrithi wa kiwango cha Dk. Shein.

Alisema Pemba ya miaka ya 1990 nui tofauti kwa kiwango kikubwa na Pemba ya sasa, akibainisha kuwa miundombinu ya barabara na elimu imeimarishwa vya kutosha.



Meneja wa Benki ya Exim tawi la Tabora, Emmanuel Nkelebe (kulia), akikabidhi msaada wa taulo za kike kwa mmoja wa wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Tabora, Emmaculata Olola, ikiwa ni sehemu ya mpango wa uwajibikaji kwa jamii wa benki hiyo, unaofahamika kama Exim Cares. Wanaoshuhudia ni Ofisa Mauzo wa benki hiyo, Hawa Dachi (wa pili kulia) na walimu wa shule hiyo. **MPIGAPICHA WETU**

# Mawakala wa EFD kufikishwa kortini

**Na Innocent Ng'oko, MBEYA**

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amesema mawakala watatu wa mashine za kukusanyia mapato za kielektroniki (EFD) ambao walitiwa nguvuni na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kuhujumu mapato ya serikali, watafikishwa mahakamani kujibu mashtaka dhidi yao.

Chalamila, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, alisema jana kuwa uamuzi wa kuamuru mawakala hao kukamatwa, ulitokana na kukaidi kuhudhuria kikao cha kusikiliza kero za wafanyabiashara ambacho kilifanyika katika soko la Sido.

Kikao hicho kiliitishwa kutokana na baadhi ya wafanyabiashara hao kulalamikia kutopewa mashine za EFD kwa wakati licha ya kulipia fedha zao.

"Nikiwa mwenyekiti wa kamati ya ulinzi na usalama, niliagiza mawakala hao kufika katika kikao ambacho kilishirikisha vyombo mbalimbali wakiwamo TRA (Mamlaka ya Mapato Tanzania) kufika katika eneo la Sido kusikiliza kero za wafanyabiashara, ikiwamo kucheleweshewa mashine za EFD licha ya kulipia," alisema.

Mkuu wa mkoa alisema wafanyabiashara hao wamekuwa wakilalamikia kudhulumiwa fedha na mawakala hao kwa nyakati tofauti, hivyo kuathiri maagizo ya TRA ya kuwataka wafanyabiashara wenye vigezo kuwa na mashine hizo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Ulrich Matei, amekiri kuwakamata mawakala hao baada ya agizo la mkuu wa mkoa.

"Mimi nilitekeleza wajibu wa kuwatia nguvuni mawakala hao watatu, baada ya maagizo ya mkuu wa mkoa kutokana na kukaidi amri ya kuhudhuria kikao alichoitisha ili kusikiliza kero na kumaliza uhasama kati ya mawakala hao na wafanyabiashara," alisema.

Katika kikao hicho, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), ilitangaza kufanya uchunguzi kutokana na malalamiko ya wafanyabiashara hao kuwatuhumu baadhi ya maofisa wa TRA kuwaomba rushwa wakati wa operesheni za kukusanya mapato ya serikali na wafanyabiashara hao kuwashawishi maofisa hao wa TRA kupokea rushwa.

# Vigogo wasiotoa matamko mali kukiona

**Na Happy Severine, SIMIYU**

KAMISHNA wa Maadili, Jaji mstaafu Harold Nsekela, amewatahadharisha viongozi wa umma kutofanya mzaha katika kujaza na kuwasilisha fomu za matamko ya mali na madeni kwa wakati uliopangwa.

Jaji Nsekela amesema kuwa kitendo cha viongozi kushindwa kutekeleza jambo hilo kwa muda ambao umewekwa kishera kuna madhara makubwa ambayo wanaweza kuyapata.

Alisema hayo jana wakati wa semina ya siku moja ya maadili kwa viongozi wa umma Mkoa wa Simiyu, mjini Bariadi.

Aliwataka viongozi hao kujaza fomu hizo kabla ya hatua kali dhidi yao kuchukuliwa.

Katika kusisitiza umuhimu kwa viongozi hao jaza fomu hizo, alitolea mfano wa aliyekuwa Mbunge wa Singida Mashariki, Tundu Lissu, aliyepoteza nafasi hiyo kutokana na kushindwa kujaza fomu hizo.

"Mengi yaliongelewa baada ya kuvuliwa ubunge, lakini ukweli ni kwamba kwa miaka miwili alishindwa kujaza fomu hizo na kuwasilisha kwa Spika," alieleza Jaji Nsekela.

"Na kwa sheria za Bunge ni tofauti kidogo, wao wanatakiwa kuwasilisha kwa Spika na baadaye kuletwa kwangu, sasa yeye hakufanya hivyo kwa miaka miwili, huo ndiyo mfano mzuri, lazima na nyie muwe makini," alisema Jaji Nsekela.

Kamishna Nsekelo alisema baadhi ya viongozi hawalielewi vizuri tamko hilo, hivyo wanashindwa kujaza kama inavyotakiwa kwa awamu tatu baada ya kuingia kwenye nafasi hizo, kila mwisho wa mwaka na baada ya kustaafu.

Alisema tatizo kubwa lipo kwa viongozi ambao wanastaafu, kwani alieleza wengi wamekuwa hawazijazi, na pale wanapopata mafao yao basi wamekuwa wakidharau na hawajazi tena.

"Kwenye kustaafu ndiko tunatapa shida, na ofisi yangu tupo kwenye majadiliano, tunalifikiria kama ofisi, kwa kiongozi ambaye amestaafu ili apate mafao yake, sharti lazima awe amejaza fomu ya tamko," alisema Jaji Nsekelo.

Akifungua semina hiyo Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Antony Mtaka, alisema ana uhakika mafunzo hayo ya viongozi wa umma yatawasaidia sana katika kubadilika tabia na kutekeleza majukumu yao ya kuwasaidia wananchi ipasavyo.

Mtaka alisema kila kiongozi wa umma atakayezingatia maadili katika kutekeleza majukumu yake, yataepusha migogoro inayojitokeza kati ya viongozi.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KAZI /AJIRA

**Nafasi za kazi** ualimu masomo ya sst/diploma 0656490706/0784142792


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0782253676



## KUPOTEA KWA PASSPORT



**THOMAS VENDELIN MKWE** anatangaza kupotelewa na Hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba **AB744153.** Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa katika kituo chochote cha polisi: Taarifa ya polisi; **MOR/MOR/RB/531637/2019.**

115545302

## KUPOTEA KWA CHETI



**ISAYA SHEDRACK SONGO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0785-0065 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia DAR ES SALAAM CHRISTIAN SEMINARY mwaka 2012.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi:

**DAR/MBU/RB/527267/2019.**

115544902

## KUPOTEA KWA HATI

**TRAVELLERS LODGE CO. LTD** wanatangaza kupotelewa na hati ya TIC (Certificate of Approval No. 031002).

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:

DAR/OST/RB/511651/2019.

115544802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**FORM II**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO DODOMA MJINI**

**USIMAMIZI WA MIRATHI NA. 91/2019**

**OMBI LA HASSAN JUMA KUTEULIWA KUWA MSIMAMIZI WA MIRATHI MAREHEMU JUMA PETRO BILYETEGA**

WATU WOTE WANAODAI KUWA NA MAHUSIANO WOWOTE NA MIRATHI YA MAREHEMU HUYO WANAALIKWA KUJA NA KUHUDHURIA KESI WAKITAKA MNAMO TAREHE 18-12-2019 KABLA YA MUOMBAJI KUTEULIWA KUWA MSIMAMIZI WA MIRATHI HIYO.

WOSIA WA MAREHEMU HUYO UPO MAHAKAMANI WAWEZA KUKAGULIWA. TRH 03/12/2019

115545201

**FORM II**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA SHERIA**
**IDARA YA MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya KINONDONI**

**Usimamizi wa Mirathi No. 181/2019**

**Ombi la FELISTER PETER NZIGULA kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya Marehemu MUGANYIZI MEDARD MUTTA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 13/12/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

115541502

## KUPOTEA KWA VYETI



**ALFRED ANTHONY JILUMBA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index **namba S0127-0002** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MAKOKO SEMINARY mwaka 2011. Cheti cha kidato cha sita chenye **index namba S0144-0507** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia NSUMBA SEKONDARI mwaka 2014.

**Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.**

**Taarifa ya polisi:**
**DAR/KIJ/RB/437036/2019.**

115544602

## KUPOTEA KWA CHETI



**DIONISIA EPAPHRAS KIMINJO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0245/0007 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2004 katika shule ya Sekondari Palloti Girls.

Yeyote atakaekiona atoetaarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**DAR/GOG/RB/525942/2019**

115544502


***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa***

***Kutangaza Nasi***

***Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

**usikose Gazeti lako la**

**Nipashe kila siku**

**NJOO UTANGAZE**

**BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# WENGER:
## NITAFURAHI KUMSHAURI LJUNGBERG




**LONDON, England**

ARSENE Wenger amesema atakuwa na "furaha" kuzungumza na Freddie Ljungberg wakati wake huu akiwa kocha wa muda wa Arsenal.

Mchezo wa kwanza wa Ljungberg kuiongoza Arsenal ulikuwa ni ule wa sare ya 2-2 dhidi ya Norwich Jumamosi, wakati walipotoka nyuma mara mbili pale kwenye dimba la Carrow Road.

Ljungberg amesisitiza kuzungumza na Wenger - ambaye alikuwa kocha wake wakati akicheza pale London Kaskazini na kwamba ni moja ya mipango anayopanga kuifanya, na Wenger amesema atajisikia furaha kumpa ushauri.

"Mara zote nina furaha na wachezaji wangu wa zamani na klabu yangu ya zamani," alisema Mfaransa huyo akiiambia Sky Sports News. "Kama anahitaji hilo, bila shaka nitakuwa tayari.

"Moyo wangu upo na klabu na nataka wao wafanye vizuri. Freddie amekamata majukumu vizuri. Alitaka kazi hii kwa muda mrefu. Amepata nafasi. Tumwache afanye kazi kwa mawazo yake na tumpe sapoti yetu."

Wenger alitumia miaka 22 kama kocha wa Arsenal - akishinda mataji matatu ya Ligi Kuu na saba ya FA - kabla ya kuondoka kipindi cha majira ya joto mwaka 2018.

Ljungberg alicheza chini ya Wenger kwa miaka nane, akishinda mataji mawili ya ligi, na amesema anamkaribisha Wenger kupata uzoefu wake wakati akizungumza na waandishi wa habari.

"Kwa uhakika ningependa kuzungumza na (Wenger). Sijazungumza naye, yupo kwenye orodha yangu."

Raia huyo wa Sweden amesema pia anapanga kupata ushauri kutoka kwa raia mwenzake, Sven-Goran Eriksson.

## AGUERO ANANIPA HAMASA KUFUNGA MAN CITY - JESUS

**MANCHESTER, England**

GABRIEL Jesus anahisi kwamba presha kubwa ni kufunga katika kila mchezo wa Manchester City.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil, Jesus alimaliza ukame wa kutofunga mechi 10 kwa klabu yake na nchi kwa kufunga mabao mawili wakati City wakiibuka na ushindi wa 4-1 dhidi ya Burnley Jumanne.

Majeruhi ya nyama za paja yanayomkabili mfungaji wa wakati wote wa Man City, Sergio Aguero yamempa nafasi Jesus kuwa kwenye kikosi cha kwanza cha Pep Guardiola, nafasi ambayo aliitumia vizuri mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22.

"Najua naweza kufunga kila mchezo, lakini ni vigumu, soka si mchezo rahisi," alisema akiiambia Amazon Prime.

"Nipo na Sergio. Natakiwa kujifunza kutoka kwake kwa sababu yeye ni gwiji wa soka na klabu.

"Natakiwa kufunga kila ninapocheza kwa sababu Sergio anafunga kila wakati. Hayo ndiyo malengo yangu, kucheza na kufunga kila wakati."

Kiwango alichokionyesha Jesus pale kwenye Uwanja wa Turf Moor kitampa nafasi zaidi kuwapo kwenye kikosi cha Jumamosi kitakachocheza na majirani zao Manchester United pale kwenye dimba la Etihad.

City sasa imepunguza pengo hadi pointi nane dhidi ya vinara wa ligi hiyo, Liverpool, ambao jana Jumatano walikuwa wanacheza dhidi ya Everton pale kwenye dimba la Anfield.




## KLOPP AJIPANGA KUSAJILI JANUARI

**LIVERPOOL, England**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amesema yupo wazi kufanya usajili kipindi cha majira ya baridi Januari, huku akiongeza "klabu mara zote imekuwa tayari" kwenye soko la uhamisho.

Hii imekuja baada ya kocha wa Manchester City, Pep Guardiola kuondoa uwezekano wa kusajili wachezaji wapya wakati wa dirisha hilo dogo licha ya uhitaji wa beki wa kati.

Alipoulizwa kama alishangazwa na kauli hiyo ya Guardiola, huku City wakiwa nyuma kwa pointi nane dhidi ya vinara Liverpool, Klopp alisema: "Sipo hapa kuzungumza kuhusu dirisha la usajili la Man City.

"Ndio kwanza nasikia hilo kwa mara ya kwanza. Nimeshangazwa? Hapana. Si muhimu.

"Hatuwezi kuzungumza kuhusu hilo. Sisi mara zote tupo tayari - kama tunaweza kufanya kitu ambacho kitatusaidia sisi, tutajaribu kufanya. Kama sivyo, hatufanyi."

Makocha wengi huwa hawapendi kujihusisha na biashara ya usajili wa kipindi cha dirisha la Januari, lakini Klopp hana uhakika kama kutakuwa na tofauti yoyote ukilinganisha na dirisha la kipindi cha majira ya joto.

"Nafikiri kipindi cha dirisha la majira ya joto kwa uhakika ni kigumu kwa sababu ya tofauti ya nyakati wakati wa kufungwa barani Ulaya," aliongeza.

"Hilo inafanya mambo kuwa magumu. Tutaona namna itakavyokuwa kwa siku za usoni, lakini dirisha la kipindi cha majira ya joto kinaziumiza zaidi klabu za Uingereza na haiwasaidii."

Klopp haitakuwa mara yake ya kwanza kufanya usajili wakati wa dirisha la Januari, kwani mwaka 2018 wakati wa kipindi hicho alimsajili Virgil van Dijk kutoka Southampton kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 75, ambayo iliweka rekodi ya ada kubwa zaidi kununuliwa beki.

Usajili huo ulimlipa Klopp na Liverpool, huku Van Dijk akishika nafasi ya pili kwenye tuzo za Ballon d'Or 2019 - nyuma ya mshambuliaji wa Barcelona, Lionel Messi.



# GUARDIOLA

## AKATA TAMAA MBIO ZA UBINGWA EPL

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola anafikiri ni "uchizi" kwa Manchester City kufikiri kuhusu kuikamata Liverpool - ingawa kauli yake kwamba mbio za ubingwa wa Ligi Kuu ya England zilikuwa zimemalizika, ilionekana kama imefutwa baada ya kushuhudia timu yake ikiibuka na ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Burnley juzi, Jumanne.

City walikwenda pale kwenye dimba la Turf Moor wakiwa wameshinda mechi moja kati ya tano kwenye mashindano yote, wakati Gabriel Jesus akifunga mabao mawili kwenye ushindi huo.

Rodri alifunga la tatu kabla ya Riyad Mahrez aliyetokea benchi naye kufunga kwenye ushindi huo, huku bao la kufutia machozi kwa wenyeji likifungwa na Robbie Brady.

Matokeo hayo yameifanya City sasa kupunguza pengo la pointi na sasa imepitwa pointi nane na vinara wa ligi hiyo, Liverpool kabla ya vijana hao wa Jurgen Klopp kuwavaa Everton mchezo uliopigwa jana usiku.

Alipoulizwa kuhusu kiwango cha City na kama wamekata tamaa kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu, Guardiola alijibu: "Mbio za ubingwa zimeishaisha. Kwa kile ninachokisoma, hakuna mtu anayetupa sisi nafasi. Imeshamalizika."

Kocha huyo wa zamani wa Barcelona na Bayern Munich aliongeza: "Kwa mfano tuna mchezo dhidi ya Liverpool, itakuwa ni uchizi kufikiria kuhusu ubingwa, kwa uhakika kabisa.

"Tunatakiwa kufikiria kuhusu mchezo wetu wa 'dabi', nenda mchezo kwa mchezo kwa sababu si tu kwenye Ligi Kuu. Kuna mashindano mengine, kama FA na Carabao na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Kitu muhimu ni kuendelea kuwa na ari ile ile kwenye kila mchezo uliopo mbele yetu."

# Mwakinyo amuangukia rasmi Matumla

**Na Mwandishi Wetu**

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Hassan Mwakinyo, amejitokeza kumuomba radhi, Rashid Matumla "Snake Boy", kutokana na kumtolea lugha chafu baada ya mkongwe huyo kutoa uchambuzi wa pambano lililofanyika Ijumaa iliyopita dhidi ya Mfilipino, Arnek Tinampay.

Upepo ulionekana kuchafuka baada ya Mwakinyo kumkashifu Matumla, lakini wadau mbalimbali walijitokeza kumtaka Mwakinyo, ambaye ameanza kung'ara katika mchezo huo, kuomba radhi na kumweleza kuwa bado safari yake ni ndefu katika masumbwi.

Matumla amekubali kumsamehe Mwakinyo baada ya kuombwa radhi na kumtakia kila la kheri katika mapambano yake yajayo huku akieleza kuwa tayari kumsaidia pale atakapohitaji ushauri wake.

"Nimepigiwa wimbo wa taifa mara nyingi sana, wakati napigana, nashukuru baada ya kujua mwanangu kaja kuomba radhi, mimi namwambia nimepokea radhi yake, nimepokea vizuri, sina kinyongo, nashukuru kwa kuja mbele za watu kuniomba radhi baba yako, sina kinyongo, ukiwa na shida yoyote katika kujiendeleza, njoo," alisema Matumla.




Wadau mbalimbali wa mchezo wa ngumi walimtaka Mwakinyo, kumuomba radhi Matumla kutokana na kitendo chake cha kumponda kutokana na uchambuzi aliokuwa akiufanya wakati wa pambano lake dhidi ya Mfilipino Tinampay likiendelea.

Mwakinyo alijirekodi na kusikika katika mitandao mbalimbali akimkashifu Matumla, baada ya mkongwe huyo kutoa maoni yake wakati pambano likiendelea Ijumaa iliyopita na muda mfupi baada ya kutangazwa kuibuka na ushindi, bado alisikika kupitia redio moja jijini Dar es Salaam akiendelea kumponda mkongwe huyo.

Kupitia redio hiyo, Mwakinyo alisema Matumla alipewa nafasi hiyo ya uchambuzi ili apate hela ya kula, lakini ameitumia vibaya na kuwafanya watu wakiwamo mashabiki wake wengi kutoka kwao mkoani Tanga kuamini kwamba alibebwa dhidi ya Mfilipino huyo na kutaka yeye aombwe radhi.

Hata hivyo kwa uungwana wa Matumla, alipopigiwa simu, alisema: "Kama anataka nimuombe radhi basi namuoba, yeye ni mfalme anataka kuwa mfalme muache awe mfalme."

Katika sehemu ya uchambuzi wa Matumla wakati pambano hilo likiendelea, alisema Mwakinyo anapaswa kutomruhusu Tinampay kumpeleka hadi kwenye kamba lakini pia asikubali kushambuliwa sana tumboni na kwenye mbavu maana itamsababishia kupoteza nguvu huku akieleza hadhani kama kocha wake alimsoma vema mpinzani wake kabla ya pambano hilo, jambo ambalo bondia huyo kutoka Tanga hakulipokea vizuri.

# Argentina kufungua na Chile Copa Amerika

**BUENOS AIRES, Argentina**

ARGENTINA itafungua michuano ya Copa America 2020 kwa kucheza na Chile mjini Buenos Aires.

Hiyo ni kama mechi ya marudio ya kufafuta nafasi ya tatu ya michuano hiyo iliyofanyika mwaka huu, mchezo ambao Argentina walishinda na Lionel Messi na Gary Medel walitolewa nje kwa kadi nyekundu kwa kutaka kuzichapa, na sasa timu hizo zitakutana tena El Monumental Juni 12, mwakani.

Wakati droo iliyochezeshwa Jumanne wiki hii, timu hizo tayari zilishajua wapinzani wao kwa kuwekwa kwenye kanda kwa ajili ya michuano hiyo itakayofanyika kwa ushirikiano wa nchi mbili za Argentina na Colombia.

Hata hivyo, Australia akiwa mgeni mwalika kwenye Copa America kwa mara ya kwanza, imepangwa Kundi A pamoja na Argentina, Bolivia, Uruguay, Chile na Paraguay.

Qatar, timu nyingine mwalikwa kwenye michuano hiyo, ipo kundi moja na Colombia, Brazil, Venezuela, Ecuador na Peru.

Brazil itakwenda kwenye michuano hiyo kama bingwa mtetezi baada ya kulitwaa mwaka huu.

Timu nne za kwanza kwenye kila kundi zitafuzu kucheza robo fainali.

Kundi A linaundwa na Argentina, Australia, Bolivia, Uruguay, Chile na Paraguay.

Kundi B: Colombia, Brazil, Qatar, Venezuela, Ecuador, Peru.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# KLOPP: MESSI NI BORA ILA BALLON D'OR YA VAN DIJK

Labda ni mchezaji bora niliyewahi kumuona katika maisha yangu, ila msimu uliopita kamwe siwezi...

**LIVERPOOL, England**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amemsifu Lionel Messi akisema "pengine ni mchezaji bora zaidi niliyewahi kumuona maishani mwangu," lakini anadhani Virgil van Dijk alipaswa kutunukiwa tuzo ya Mchezaji Bora wa Mwaka ['Ballon d'Or'].

Nyota wa Barcelona, Messi Jumatatu aliweka rekodi ya kutwaa tuzo hiyo kwa mara ya sita, na waandaaji wa tuzo hiyo Jarida la Soka la Ufaransa ['France Football'] wakikiri kuwa kiwango chake cha alama saba zaidi ya Van Dijk kuwa ni kidogo zaidi katika historia ya kinyang'anyiro hicho kwa kipindi cha miaka 63.

Nahodha huyo wa Barcelona alimaliza kileleni mwa kura zilizopigwa akiwa na pointi 686 saba mbele ya Van Dijk aliyejikusanyia alama 679.

Licha ya kumkubali Messi kama mchezaji mkubwa zaidi wa kizazi hiki, Klopp anahisi Van Dijk alipaswa kutunukiwa tuzo hiyo kutokana na mchango mkubwa alioutoa Liverpool wakati ikitwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita.

Aliuambia mkutano wa wanahabari: "Uamuzi umefanywa na waandishi wa habari, sahihi? Ninaona ni tofauti kidogo. Lionel Messi labda ni mchezaji bora niliyewahi kumuona katika maisha yangu, ila msimu uliopita kamwe siwezi kukumbuka zaidi msimu wa kuvutia kwa beki.

"Ingekuwa sahihi kama Virgil angeshinda pia. Tulishinda Ligi ya Mabingwa na alikuwa na msimu mzuri."

Jana usiku Van Dijk alitarajiwa kuiongoza safu ya ulinzi ya Liverpool kwenye mechi ya 'Merseyside dabi' dhidi ya Everton katika Uwanja wa Anfield.

Na katika droo ya Kombe la FA raundi ya tatu, timu hizo zimepangwa kukutana tena wiki ya kwanza ya Januari, na Klopp akifunguka kuwa angependelea kuanza kirahisi kampeni yao ya kuwania kombe.

"Siwezi kukimbia ndani ya chumba changu ninachoishi na kusherehekea," alisema. "Sicho kabisa ambacho tulitaka, lakini hatuna tatizo la kucheza na Everton. Ni mechi kubwa dhidi ya wapinzani wakubwa. Ni wazi, tunaanza njia ngumu. Hatuwezi kulibadili hilo na tuna muda wa kujiandaa kwa mechi hiyo ya Everton baada ya hii moja [ya jana]."

Klopp alithibitisha kuwa Liverpool haina majeruhi wapya kabla ya mchezo huo wa jana, lakini akieleza kuwa Joel Matip bado hajawa fiti kutokana na majeraha ya goti, ambayo aliyapata tangu walipotoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Manchester United Oktoba 20.

"Joel anahitaji muda kidogo," alifafanua. "Ni uponyaji lakini si sahihi kabisa kwa kile tunachokitaka."

## KWA UFUPI

**ERIKSEN BEI CHEE SPURS**
Tottenham ipo tayari kusikiliza ofa ya chini ya pauni milioni 40 kwa kiungo Mdenmark Christian Eriksen, 27. ***(Evening Standard)***

**POCHETTINO KUMNG'OA SOLSKJAER**
KOCHA wa zamani wa Tottenham, Mauricio Pochettino anataka kutwaa mikoba ya Ole Gunnar Solskjaer kama kocha wa Manchester United. ***(Manchester Evening News)***

**SPURS HANA SHIDA NA MATIC**
Spurs haina lengo la kwenda kumsajili kiungo wa Manchester United na Serbia, Nemanja Matic, 31. ***(Manchester Evening News)***

**GUARDIOLA HASAJILI JANUARI**
KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola ameweka kando uwezekano wa kufanya usajili wowote katika dirisha la Januari licha ya kuwapo kwa matatizo katika safu yake ya ulinzi kutokana na kusheheni majeruhi. ***(Independent)***

**MOURINHO AMPOTEZEA FERNANDES**
KOCHA wa Tottenham, Jose Mourinho amehitimisha kuhusishwa na kiungo wa Sporting Lisbon, Bruno Fernandes, 25, kutokana na dau la pauni milioni 85 linalohitajika ili kuvunja mkataba wake. ***(Mail)***

**ARSENAL, MARCELINO WATETA**
Arsenal imefanya mawasiliano na kocha wa zamani wa Valencia, Marcelino wakati huu ikiendelea kutafuta kocha mpya. ***(Goal - in Spanish)***

**CITY, BARCA KWA MARTINEZ**
Manchester City imejiunga katika mbio za kuisaka saini ya mshambuliaji wa Inter Milan na Argentina, Lautaro Martinez. Barcelona pia inavutiwa na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22. ***(Sky Sports Italia, via Calciomercato - in Italian)***

**GIROUD, CHELSEA KUJADILIANA**
MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Ufaransa, Olivier Giroud atafanya mazungumzo na Chelsea kuhusu uwezekano wa kuondoka Januari. ***(Evening Standard)***

**BENITEZ KUZIGHARIMU KLABU EPL**
KLABU za Ligi Kuu England zinamtaka kocha wa zamani wa Liverpool na Newcastle, Rafael Benitez, lakini zitapaswa kulipa fidia ya pauni milioni 20 kwa klabu yake ya sasa ya Dalian Yifang. ***(Mail)***

**LIVER YAMFUNGUKIA BREWSTER**
Liverpool itamruhusu tu mshambuliaji wao na England U-21, Rhian Brewster, 19, kujiunga na klabu nyingine kama tu itahakikishiwa kupata muda wa kutosha kucheza. ***(Football Insider)***

**SILVA SIKU ZAHESABIKA EVERTON**
Everton inajiandaa kuendelea kumpa nafasi Marco Silva kama kocha wao kabla ya mechi ya 'dabi' dhidi ya Liverpool leo. ***(Express)***



## HABARI MICHEZO

# TANZANIA KUIVAA ZIMBABWE FAINALI COPA COCA-COLA KESHO

**Na Mwandishi Wetu, KENYA**

TIMU ya soka ya Tanzania ya vijana chini ya umri wa miaka 16, COPA Coca-Cola imeendelea kufanya vizuri katika michuano ya COPA Afrika baada ya kuwatoa wenyeji Kenya kwa penalti na kutinga fainali ambapo sasa itawavaa Zimbabwe kesho.

Katika mechi hiyo ya nusu fainali iliyopigwa katika Uwanja wa M-PESA Foundation Academy, Thika nchini Kenya, Tanzania ilishinda kwa penalti 5-4 baada ya mchezo huo kumalizika kwa sare tasa.

Haukuwa ushindi mwepesi kwa timu ya Tanzania inayonolewa na Kocha Abel Mtweve, kwani timu ya Kenya ilipigana mpaka mwisho na kulazimisha sare mpaka kipenga cha mwisho.

Hata hivyo, vijana wa Tanzania walicheza soka safi na la kuvutia licha ya timu zote mbili kushindwa kuliona lango la mwezie mpaka dakika ya mwisho.

Kipa wa Tanzania, Chuma Ramadhani, aliibuka shujaa wa mchezo huo baada ya kufanikiwa kuchomoa penalti moja kati ya tano na kuiweka Tanzania kutinga fainali.

Penalti za Tanzania zilizamishwa nyavuni na Mohameed Rai, Edward Bernard, Nyerere Paul, Frank Stephen na Innocent Mtoi, ambapo kwa ushindi huo itakutana na Zimbabwe fainali kesho, iliyoitoa Zambia kwa kuichapa mabao 4-2 katika mchezo mwingine wa nusu fainali uliopigwa jana.

Timu ya Tanzania ilipata baraka ya kutembelewa na Balozi wa Tanzania nchini Kenya, Dk. Pindi Chana ambaye aliwaongezea ari wachezaji kwa kuwasihi kuhakikisha wanashinda mechi hiyo.

Aidha, Chana aliishukuru Kampuni ya Coca-Cola kwa kuja na michuano ya namna hii yenye lengo la kuibua vipaji vya vijana kutoka katika viwango vya chini.

"Nimefurahi sana kuambiwa kuwa michuano hii inahusisha nchi kumi za barani Afrika, hivyo haya ni mashindano makubwa na yatawawezesha vijana wetu kufika mbali."

Akizungumza mara baada ya mechi hiyo kumalizika, Kocha wa Tanzania, Abel Mtweve alisema: "Mkakati wetu tangu mwanzoni umekuwa ni kushambulia kwa kushtukiza, lakini pia tunatumia muda mwingi kujilinda."

Naye Mkuu wa Msafara, Mwalimu Vitalis Shija, ambaye ni Makamu wa UMISSETA Taifa, alitoa pongezi kwa vijana kwa kupigana hadi mwisho na kuwataka kurudi na kombe Tanzania.



Balozi wa Tanzania nchini Kenya, Dk. Pindi Chana (katikati), aliyeonyesha dole gumba) akifurahia na kocha wa timu ya vijana wa Tanzania, Abel Mtweve (aliyevaa kofia) pamoja na wachezaji wa timu hiyo baada ya kuitoa Kenya kwa penalti 5-4 kwenye mechi ya nusu fainali ya michuano ya Copa Coca-Cola Afrika iliyopigwa Uwanja wa M-PESA Foundation Academy nchini Kenya jana. **MPIGAPICHA WETU**

# Kili Stars kuanza na Kenya, Z'bar na Sudan

**Na Somoe Ng'itu**

TIMU za soka za Tanzania, Kilimanjaro Stars ya Bara na Zanzibar Heroes ya Zanzibar, ambazo zinaondoka nchini leo, kuelekea Uganda kwa ajili ya kushiriki mashindano ya Kombe la Chalenji yanayotarajiwa kufanyika kuanzia Jumamosi wiki hii jijini Kampala, zitaanza kutupa karata zao za kwanza Jumapili kwa kuzivaa Kenya na Sudan.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Kocha Mkuu wa Kilimanjaro Stars, Juma Mgunda, alisema kikosi hicho kimejiandaa vizuri kwenda kushindana katika mashindano hayo yanayoshirikisha nchi kutoka Afrika Mashariki na Kati.

Mgunda alisema kuwa anafahamu timu zote zinazoshiriki michuano hiyo ni nzuri na wao ndio maana wanakwenda huko kupambana ili kupata matokeo mazuri.

"Niwahakikishie tu, kuwa mimi na benchi langu la ufundi tunakwenda huko kupambana, tumejiandaa kwenda kushindana, yoyote tutakayekutana naye sisi ni changamoto," alisema Mgunda.

Naye golikipa wa timu hiyo, Aishi Manula, alisema wamefanya maandalizi mazuri na malengo yao ni kwenda kupambana ili kupata matokeo chanya katika mashindano hayo.

"Tunakwenda kupambana, kupigania nchi yetu, na timu yetu, malengo yetu kama wachezaji ni kwenda kurejesha heshima yetu, heshima ile ambayo Tanzania Bara tuliipata mwaka 2010, ni muda mrefu umepita," alisema Manula.

Wakati huo huo, Waziri wa Vijana , Sanaa, Utamaduni na Michezo wa Zanzibar, Balozi Ali Karume, amewataka wachezaji wa Zanzibar Heroes kwenda kupambana na kufanya vizuri katika michuano hiyo kwa sababu Wazanzibar wote wanawaangalia wao.

Alisema kuwa wana matumaini na timu hiyo kutokana na hamasa waliyokuwa nayo mwaka huu, ambayo ni tofauti na miaka mingine iliyopita.

" Tunawaomba mkafanye vizuri katika michuano hiyo, kuna zawadi zenu kubwa, na hata mkifanya vibaya si kama hatutawapa zawadi, mtapewa lakini itakuwa ya kawaida ila ninamatumaini makubwa mtawapa Wazanzibar burudani inayostahili ili kuendeleza hamasa hii," alisema kiongozi huyo.

Katika hatua nyingine, Ethiopia, Sudan Kusini na wageni, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), zimeondolewa katika mashindano hayo kutokana na kushindwa kutimiza vigezo vya kushiriki michuano hiyo.

# Mwakyembe awakubali waandaaji Kili Marathon

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, amewapongeza waandaaji wa mbio za Kilimanjaro kwa kukuza utalii wa michezo kwa kupitia mbio hizo na kuwataka wadau wengine nchini kuiga mfano huo.

Mwakyembe alisema hayo jana jijini Dar es Salaam, alipokutana na waandaaji wa mbio hizo baada ya kumaliza uzinduzi wa mashindano ya mwaka huu.

Alitoa wito kwa mikoa yote inayoandaa mbio kuhakikisha wanazingatia faida za kiuchumi kwa kuandaa shughuli mbalimbali za kiutamaduni na kijamii kwa wenyeji na watalii kabla na baada ya mbio ili kuongeza kipato na ajira wakati wote wa mashindano.

"Kilimanjaro Marathon imekuza utalii wa michezo kwa kiasi kikubwa, kwa sababu washiriki wanaweza kutembelea vivutio mbalimbali vya kitalii katika Mkoa wa Kilimanjaro na maeneo mengine nchini ambapo kuna vivutio vya utalii, pia mchezo wa riadha ni mzuri kwa kuimarisha afya, lakini pia ni moja ya chanzo cha fedha za kigeni," alisema Mwakyembe.

Alionyesha pia kufurahishwa na namna mbio mbalimbali zinaanzishwa mikoani ila akatoa tahadhari kuwa ni muhimu kuwapo na miongozo na waandaaji kuzingatia taratibu zilizowekwa ili kufikia malengo.

Pia Mwakyembe ametoa pongezi nyingine kwa waandaaji wa mbio za Kilimanjaro kwa kukubali kusaidia maandalizi ya mbio za John Steven Akhwari ambazo zinatarajiwa kufanyika Juni mwakani.

Katika kikao hicho cha pamoja na Mwakyembe, Kamati ya Maandalizi ya Kilimanjaro Marathon iliwakilishwa na Mratibu Mkuu, John Addison, Mwanzilishi wa mbio hizo, Aggrey Mareale, ambaye ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Executive Solutions na Mkurugenzi wa Taifa, John Bayo.

# SIMBA KIGOGO FRESH YANUKIA

**Na Mwandishi Wetu**

WAPENZI na mashabiki wa klabu ya Simba wa Kigogo Fresh jijini Dar es Salaam wamehamasishwa kufungua tawi rasmi ili kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya klabu yao, hasa wakati huu ambao muundo wa uendeshaji umebadilishwa.

Mashabiki hao pia wametakiwa kuhakikisha wanafungua ofisi ambayo itakuwa na uwezo wa kuwasaidia kufanya mchakato wa kupata uanachama wa kudumu kwa klabu hiyo.

Kauli hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa Matawi ya Simba Wilaya ya Ilala, Ahmed Malaika, ambaye aliongozana na Katibu Mkuu, Yahaya Athumani, katika kuwahamasisha mashabiki hao kwenye ziara maalumu iliyofanyika Jumapili iliyopita.

Malaika alisema kwa sababu Simba sasa imeingia kwenye zama za 'Next Level' kwa maana uwekezaji wa hisa, sasa mashabiki hao wanatakiwa kuanzisha tawi ili kuhakikisha wanapata uanachama wa kudumu.

"Kama ukiwa na tawi leo hapa, itakuwa rahisi sisi ngazi ya wilaya kuwasaidia kupata kadi za uanachama wa Simba, na mtakuwa kati ya watu wenye hisa ndani ya Klabu ya Simba," alisema Malaika.

Aliongeza kusema kuwa uwepo wa tawi la Simba hapo Kigogo Fresh pia itawafanya wanachama wake kujumuishwa kwenye mikakati mbalimbali ya klabu hiyo ambayo kwa sasa ndio mabingwa watetezi na vinara kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Naye Makamu Mwenyekiti wa mashabiki hao, Emmanuel Ruge, alisema kuwa wameamua kufikia hatua hiyo kwa ajili ya kuimarisha ushabiki wao, ndani ya klabu hiyo.

Ruge alisema eneo la Kigogo Fresh kwa muda mrefu lilikuwa halina tawi la Simba hivyo wao wameona ni wakati muafaka kuazisha tawi lao kwa ajili ya kuipa sapoti Simba.

Michezo
Alhamisi Desemba 5, 2019
Nipashe



## Mwakinyo amuangukia rasmi Matumla

HABARI UK 29

SHUTI...



Mshambuliaji wa Manchester City, Gabriel Jesus aliyefunga mabao mawili wakati wakishinda 4-1 dhidi ya Burnley juzi usiku, akiachia shuti langoni mwa wapinzani wao hao, huku akizongwa na mabeki wa timu hiyo kwenye mchezo huo wa Ligi Kuu uliopigwa katika Uwanja wa Turf Moor. **HABARI UK. 28**

# AUSSEMS ASHUKIA 'VIHIYO' WA SIMBA

●●●Aacha ujumbe mzito akitaka watimuliwe klabu isonge mbele, awalilia mashabiki, amtaja Okwi, Kotei...

**Na Somoe Ng'itu**

ALIYEKUWA Kocha Mkuu wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Mbelgiji Patrick Aussems, ameacha ujumbe mzito kwa klabu hiyo, baada ya kuieleza kuwa ili iweze kusonga mbele, ni lazima iwaondoe viongozi "waongo" na wasio na elimu 'vihiyo' ambao wako kwenye Bodi ya Wakurugenzi.

Aussems, ametoa kauli hiyo juzi, saa chache kabla ya kupanda ndege kurejea kwao, kutokana na Simba kuamua kuachana naye kwa madai ya kufanya makosa ya kimaadili.

Mbelgiji huyo alisema anaitakia kila la kheri klabu hiyo, lakini amewakumbusha kubadilika ili kwenda na wakati.

"Asante wachezaji kwa kazi nzuri na ushirikiano tuliofanya pamoja, asante mashabiki kwa sapoti isiyoelezeka, ninawatakia kila la kheri, lakini ili Simba ikue, lazima iwaondoe viongozi waongo na ambao hawana elimu kwenye Bodi ya Wakurugenzi. Sasa ni muda wa mimi kufurahia, kitu ambacho ni muhimu katika maisha yangu na familia. Kwa kheri Tanzania," alisema Aussems.

Aliongeza kuwa baadhi ya viongozi walioko kwenye bodi hiyo, wanachangia kukwamisha maendeleo ya Simba kwa kuweka vipingamizi katika baadhi ya mipango ya klabu na kusisitiza waondolewe mapema ili kupata matokeo chanya.

**Kocha huyo pia amekanusha kufanya mawasiliano na klabu ya Polokwane inayoshiriki Ligi Kuu Afrika Kusini, ikiwa ni moja ya tuhuma aliyokuwa nayo ya kuondoka kwenye kituo chake cha kazi bila ruhusa.**

Mbelgiji huyo pia ameweka wazi kwamba hakuwa radhi kuona baadhi ya wachezaji aliokuwa nao msimu uliopita wakiondoka, akiwamo mshambuliaji Mganda Emmanuel Okwi na kiungo raia wa Ghana, James Kotei. Mbali na kuipa ubingwa wa Bara, Aussems pia aliwapa Wekundu wa Msimbazi Ngao ya Jamii mara mbili huku akiwapeleka kwenye hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Chini ya Aussems, Simba ilipata ushindi katika mechi zake zote tatu za nyumbani za hatua ya makundi ilipowakaribisha JS Saoura ya Algeria, Al Ahly (Misri) na AS Vita kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Wakati Suleiman Matola kutoka Polisi Tanzania akiwa amerejea Simba, makocha mbalimbali wanaendelea kutajwa kuomba kurithi mikoba ya Aussems, ambaye katika mechi 10 za Ligi Kuu Bara ameshinda nane, ametoka sare moja na akufungwa mchezo mmoja wa ugenini dhidi ya Mwadui FC ya Shinyanga.

## Simba kuivaa Arusha, Yanga Iringa FA Cup

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Mabingwa wa Kombe la FA, Azam FC, wakipangiwa kucheza dhidi ya African Lyon kwenye mechi za raundi ya tatu za kinyang'anyiro hicho, Mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, watacheza na Arusha United, huku Yanga ikipambanishwa na Iringa United.

Kwa mujibu wa ratiba ya 64-bora ya michuano ya Kombe la FA iliyotolewa jana na Shirikisho la Soka nchini (TFF), ikirushwa mubashara, timu hizo za Simba, Yanga na Azam zitaanzia nyumbani, zikianza safari ya kusaka ubingwa kwa ajili ya kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika (Caf).

Mechi zote za raundi hiyo ya tatu kutafuta timu 32 zitakazotinga kwenye raundi ya nne, zitachezwa kuanzia Desemba 20 hadi 22, mwaka huu. Kingine kilichovutia wengi walioshiriki kwenye droo hiyo ya upangaji wa ratiba, ni kuwapo kwa mechi kati ya Coastal Union ya Tanga dhidi ya mahasimu wao wa jadi, African Sports ambayo itachezwa kwenye Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

Droo ilizidi kuvutia baada ya Pamba ya Mwanza kupangiwa kucheza dhidi ya Majimaji ya Songea, hivyo mechi zote hizo mbili kukumbusha miaka ya '80 hadi '90 wakati wa Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara ambayo kwa sasa ni Ligi Kuu.

Mechi zingine ni kati ya Lipuli dhidi ya Dar City, Kagera Sugar dhidi ya Rufiji United, Prisons ikicheza dhidi ya Mlale FC. Mtibwa Sugar nayo itakuwa nyumbani dhidi ya Rhino Rangers ya Tabora, Namungo FC dhidi ya Green Warrios, JKT Tanzania ikiikaribisha Boma FC ya Mbeya.

Biashara United itakuwa nyumbani dhidi ya Nyamongo FC zote za mkoani Mara, Mbao FC dhidi ya jirani zao Stand United, Ruvu Shooting itakuwa mgeni wa Milambo FC ya Tabora. KMC itaivaa Mbuni FC, Mwadui dhidi ya Mkamba Rangers, Alliance dhidi ya Transic Camp, Singida United itacheza na Tukuyu Stars, Polisi Tanzania dhidi ya TP Boys na Mbeya City dhidi ya Migombani FC.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >